**29 APRILI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Kumi na Tisa - Tarehe 29 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri.

Katibu.

**29 APRILI, 2026**

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 218

**Miundombinu Wezeshi kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum**

**MHE. AISHA M. MDUYAH** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwawekea Miundombinu wezeshi Wanafunzi wenye mahitaji maalum ili wasome fani wanazozipenda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah, Mbunge wa Viti Malaam, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Mwongozo wa Utekelezaji wa Mkakati wa Elimu Jumuishi wa mwaka 2022 - 2026 na Waraka Namba Tatu wa mwaka 2025 kuhusu mfumo wa Kitaifa wa kuzifanya shule kuwa Jumuishi mwelekeo wa Serikali ni kuzifanya shule zote za msingi na sekondari zilizopo kuwa jumuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali kuzifanya shule za msingi na sekondari kuwa jumuishi, ni pamoja na kuhakikisha kuwa miundombinu inayojengwa inakuwa rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, kuhakikisha kuwa bajeti ya Serikali

inajumuisha fedha ya ununuzi wa vifaa wezeshi na vifaa visaidizi kwa watoto wenye mahitaji maalum, kutoa ajira kwa walimu wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na kutoa mafunzo kwa walimu wa elimu maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kuna shule maalum 44 za msingi na moja ya sekondari, vitengo maalumu 815 kwa shule za msingi na shule za awali na msingi jumuishi 20,889 na sekondari ni 6488. Vilevile, shule jumuishi 53 za sekondari za bweni Kitaifa na tatu za kutwa zinapokea wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambao wana changamoto kubwa zaidi nchi nzima. Serikali itaendelea kuboresha shule za msingi na sekondari ili ziwe jumuishi zaidi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aisha Msantu, swali la nyongeza.

**MHE. AISHA M. MDUYAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze na kuishukuru Wizara ya TAMISEMI, kwa majibu yao mazuri, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na aina nyingi za ulemavu, kuna baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu wanashindwa kufikia masomo yao ya elimu ya juu kutokana na hali zao. Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kuhakikisha kwamba wanafunzi hawa wanapatiwa vitendea kazi pamoja na walimu bobezi kwa masomo ya amali ambayo yataweza kuwafanya wenyewe waweze kujitegemea hapo baadaye? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah, amekuwa msemaji imara sana wa watu wenye ulemavu, lakini na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan imedhamiria kwa vitendo na inatekeleza taratibu, lakini pia miundombinu ya kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata fursa nzuri zaidi ya kusoma na kujifunza ili waweze kufikia malengo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie kwamba suala la watu wenye ulemavu ambao wanahitaji viwezeshi wanahitaji miundombinu yote imewekwa kwenye utaratibu mzuri kuhakikisha kwamba wanafikia kwenye ngazi wanazopenda na kusoma taaluma ambazo wanaweza kuzifikia kwa mujibu wa matakwa yao, na Serikali ikaendelea kuhakikisha pia tunapata walimu na vitendea kazi kwa ajili ya kuwawezesha watu wenye ulemavu kusoma kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 219

**Sheria ya Ugatuzi wa Madaraka kwa Serikali za Mitaa katika Utekelezaji wa Dira ya 2050**

**MHE. MARTHA N. GWAU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka Sheria ya Ugatuzi wa Madaraka kwa Serikali za Mitaa kama hatua ya kutekeleza Dira ya Taifa ya 2050?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuimarisha Mfumo wa Ugatuzi kwa Serikali za Mitaa kama nyenzo muhimu ya kufanikisha maendeleo endelevu ya Taifa, hususan katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tathmini mbalimbali, zilizofanyika Serikali imeandaa mapendekezo ya kutunga Sera ya Taifa ya Ugatuzi ya mwaka 2026 ambayo ipo katika hatua za maamuzi. Kupitia mapendekezo hayo, Serikali inalenga kuweka mfumo wa Kitaifa utakaoratibu kwa ufanisi utekelezaji wa ugatuzi nchini, kuziimarisha Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuongeza ushiriki wa wananchi katika maamuzi ya maendeleo yao, pamoja na kuboresha mgawanyo wa madaraka, rasilimali na majukumu kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa sera hiyo unaweza kuambatana na mapitio ya baadhi ya sheria zilizopo au kutungwa kwa Sheria ya Ugatuzi pale itakapohitajika, kwa lengo la kuondoa changamoto za kiutendaji na kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu ni kuhakikisha kuwa madaraka, rasilimali na maamuzi, vinashushwa kwa ufanisi zaidi katika ngazi za Serikali za Mitaa ili kuongeza tija, uwajibikaji, na kuchochea maendeleo ya wananchi kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele vya maeneo yao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, tunaenda kwenye utekelezaji wa Dira yetu ya mwaka 2050. Je, Serikali za Mitaa zimeanzishwa muda mrefu takribani miaka 44. Sasa kama hauna sera na sheria mpaka sasa uwepo wa mamlaka hizi unatekelezwa kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tunatambua kuna mifumo mbalimbali na kuna aina mbalimbali za uendeshaji wa Serikali za Mitaa. Je, sera inayopendekezwa ya mwaka 2016 itakuwa na mfumo upi? Ninashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tunazo mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zinafanya kazi kwa muda mrefu na kwa kweli zimeendelea kufanya kazi kwa ufanisi mzuri kabisa kutoa huduma, kusimamia miradi ya maendeleo na zinaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetambua kwamba pamoja na kwamba mamlaka hizi zinafanya kazi vizuri kupitia miongozo na sheria mbalimbali, lakini tuna kila sababu ya kuwa na sera mahususi ambayo itakwenda kuzisimamia zaidi shughuli za ugatuzi wa madaraka ili kuzipa nguvu zaidi halmashauri zetu lakini pia na kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, pamoja na kwamba kwa sasa tuna miongozo, sheria na taratibu ambazo zinawezesha halmashauri zetu kufanya kazi, kazi zinakwenda vizuri bila changamoto yoyote. Kinachofanyika sasa ni kutunga sera rasmi ili kuwezesha sasa suala la ugatuzi wa madaraka na majukumu ya mamlaka zetu kuwa wazi zaidi, lakini pia kufanyika kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sera hii ambayo inatarajiwa kuandaliwa ya mwaka 2026, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, mara sera itakapokuwa imeandaliwa, tutaleta kwa Waheshimiwa Wabunge kwa namna yoyote ili waweze kuiona *content* yake ikoje, lakini inapanga kufanya jambo gani ili kuboresha sera hiyo, lakini pia kuhakikisha kwamba inakuwa na tija inayotarajiwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Huko nyuma kulikuwa na miongozo na taratibu mbalimbali za kurudisha mapato ya Serikali za Vijiji kwenye maeneo yao na kwa sheria ya mwaka 1982 Sheria Namba Nane na Namba Saba wanasema kijiji kinapata asilimia tatu, kata inapata asilimia nne na kitongoji 13%, lakini kumekuwepo na maeneo ya minada, kama Mnada wa Mgeta na maeneo mengine Serikali za Mitaa hazirudishi mapato kwenye maeneo hayo. Ni lini Serikali itaweka utaratibu wa mapato hayo yarudishwe kwenye maeneo yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliweka sheria, taratibu, miongozo na nyaraka mbalimbali kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kurudisha sehemu ya makusanyo ya mapato ya ndani kwenye vijiji ambavyo vimekusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili linaendelea kutekelezwa, lakini ni kweli kwamba ufanisi wake siyo mkubwa kwa kiwango kinachotakiwa. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwanza niwasisitize, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri, TAMISEMI, Wakurugenzi wote Mamlaka za Serikali kuhakikisha wanazingatia utekelezaji wa sheria hiyo ambayo inaelekeza sehemu ya mapato ya ndani kurejeshwa kwenye vijiji ili kuweza kusaidia shughuli za maendeleo na za kijamii katika maeneo hayo na sisi Ofisi ya Waziri Mkuu tutasimamia suala hilo kwa karibu ili kuhakikisha kwamba sheria hiyo inazingatiwa ipasavyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge wa Chamazi, sasa aulize swali lake.

Na. 220

**Ujenzi wa Barabara ya Charambe Magengeni – Zahanati ya Kilamba**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Charambe Magengeni hadi Zahanati ya Kilamba ili kuondoa kero kwa Wagonjwa wanaoenda Hospitali ya Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mbunge Jimbo la Chamazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Charambe Magengeni hadi Zahanati ya Charambe (Kilamba) ina urefu wa kilometa 1.3, ambapo hadi sasa mita 590 zimeboreshwa kwa kiwango cha zege na ziko katika hali nzuri kwa gharama ya shilingi milioni 676.9 huku meta 710 zilizobaki bado ni za changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuendelea kuijenga barabara hii kwa tabaka la zege kwa awamu na imeweka katika mpango na bajeti ya mwaka 2026/2027 kwa kutumia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa Temeke. Kiasi cha shilingi milioni 575.9 ambapo barabara hiyo itajengwa kwa urefu wa meta 710. Aidha, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu katika bajeti ili kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali ina mpango gani wa dharura kwa kuirekebisha barabara hiyo ili kuondoa adha kwa wajawazito?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuirekebisha barabara inayotoka Mashine ya Maji – Kanisani mpaka Zahanati hiyo ili kuwa barabara mbadala badala ya barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii nimthibitishie Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, kwamba tunatambua umuhimu wa barabara hii ikizingatia barabara hii inapita kwenye Zahanati ya Charambe (Kilamba). Kwa hiyo, inahitajika sana kwa huduma za afya kwa wananchi katika eneo hilo na ndiyo maana Serikali ilianza kwa kujenga kipande cha mita 590 kiwango cha zege na tunapanga kuendelea kujenga barabara hii kwa mita zilizobaki 710 kiwango cha zege kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo limechukuliwa kwa uzito unaotakiwa. Kwa maeneo ambayo hayapitiki kwa sasa, ninaomba nichukue nafasi hii nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Temeke kwa kushirikiana na Meneja wa *TATURA* wa Wilaya ya Temeke na Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Dar es Salaam, wafike eneo la tukio kuona eneo ambalo halipitiki kabisa ili yafanyike matengenezo ya muda, wananchi waendelee kupita wakati tunasubiri matengenezo ya kudumu ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara aliyoitaja ya Kanisani kuelekea kwenye zahanati hii, ni moja ya barabara ambazo sisi kama TAMISEMI tunazitambua na tunaziweka kwenye mpango kwa awamu kwa ajili ya kuzijenga ili ziweze kupitika vizuri. Kwa hiyo, tutaendelea kutekeleza miradi hiyo kwa awamu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini barabara ya Mbinga - Tanda - Masimeli hadi Miembeni itajengwa kwa kiwango cha changarawe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mpango wa kuhakikisha kwamba barabara zetu zile ambazo zinajengwa kwa kiwango cha udongo zinaanza kujengwa kwa kiwango cha changarawe ili kuanza kuboresha ubora wake, na pia kuhakikisha kwamba zinadumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini kwamba barabara hiyo ni moja ya barabara ambazo tutaendelea kuziewekea fedha kwenye bajeti zetu ili kuhakikisha kwamba zinaanza kujengwa kwa kiwango cha changarawe ili tuweze kuboresha zaidi huduma za usafiri kwa wananchi wa Mbinga Mjini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Ni lini sasa barabara ya Mto Mbozi kwenda Tandali itajengwa? Ni kwa miaka mitatu sasa haijaguswa kabisa. Barabara hii iko katika Jimbo la Morogoro Kusini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro Kusini amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na barabara hiyo na tulikwishawasiliana na Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Morogoro

na Wilaya ya Morogoro na walishawasilisha maombi ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa Serikali iko kwenye taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kufanya matengenezo ya barabara hizo, na barabara hizi nyingi zitatengenezwa baada ya mvua hizi ambazo zinaendelea kunyesha kukatika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini kwamba Serikali hii sikivu inatambua, na italifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ningependa kufahamu nini kauli ya Serikali kuhusiana na barabara inayotoka Segerea Mwisho kupitia kwa Makongoro Mahanga - Sekondari ya Ugombolwa - Zahanati ya Segerea kwa sababu ni mbovu na inasababisha wananchi wa Kata ya Segerea kushindwa kupata huduma. Nini kauli ya Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali ni kwamba Meneja wa *TARURA* wa Ilala afike kwenye barabara hiyo mapema iwezekanavyo afanye tathmini ya hicho kipande ambacho kina uharibifu mkubwa ambao unasababisha wananchi kushindwa kusafiri kutoka Segerea mwisho kwenda Zahanati ya Segerea ili kama inawezekana yafanyike matengenezo ya muda kuwezesha wananchi kupita wakati huo tunasubiri matengenezo yale makubwa ambayo yatafanyika baada ya mvua zinazoendelea kukatika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Sandali katika Jimbo la Temeke limekuwa sasa ni eneo la kibiashara hasa maeneo ya Vetinari. Je, Serikali ina mpango gani

wa kuboresha Barabara ya Tarimo - Vetinari, Tarimo - BMK mpaka Kichangani katika Jimbo Kata ya Sandali? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara alizozitaja Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo la Temeke ni moja ya barabara ambazo zinahudumiwa kwanza na *TARURA*, lakini pia na *DMDP* awamu pili na Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba barabara zile zinaendelea kujengwa na kurekebishwa kwa awamu ili kuhakikisha kwamba zinatoa huduma zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie mama yangu Mheshimiwa Mariam Kisangi kwamba barabara hizo ni kipaumbele cha Serikali na tutahakikisha tunaendelea kuzitengea fedha na kuzirekebisha ili maeneo hayo ya kibiashara, biashara ziweze kufanyika vizuri zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kata ya Ikola na Kata Isengule hazina mawasiliano kwa sababu ya kuvunjika madaraja; na Kata ya Sibwesa inayounganisha Kata ya Katuma ina hali kama hiyo. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuzifanya hizo kata ziweze kuwa na mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zote ambazo zimeathiriwa na mafuriko na kukatika kwa maana ya madaraja, ma-*culvert* na barabara zenyewe, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tumeshatoa maelekezo kwa Mameneja wa *TARURA* mikoa yote na Mameneja wa *TARURA* wilaya zote kwamba kwanza wanatakiwa kufika kwenye maeneo hayo mapema kufanya tathmini na kuona yale ambayo

yanaweza kutengenezwa yatengenezwe kwa haraka katika hali ya dharura ili yaweze kupitika wakati tunasubiri matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kakoso kwamba tutalifanyia kazi suala la madaraja hayo. Ninafahamu Tanganyika bado mvua zinaendelea kunyesha, kwa hiyo, yapo matengenezo ambayo yanawezekana na yapo ambayo yatasubiri mvua zikae sawa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, sasa aulize swali lake.

Waheshimiwa Wabunge, kama hayupo, ninamwita Mheshimiwa Sekiboko kwa niaba ya Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Mashimba Ndaki ninaomba swali lake lipate majibu ya Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko, ni swali namba 221. Ninaomba uulize upya.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Mashimba Ndaki, ninaomba swali lake namba 221 lipate majibu.

Na. 221

**Daraja la Kuunganisha Vijiji Vitatu - Maswa**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Daraja linalounganisha Vijiji vya Wigelekelo Gumali, Masela na Barabara Kuu ya Mwigumbi Maswa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mto Tungu ni mto unaounganisha Kata ya Masela na Kata ya Bugarama katika Barabara ya Mwasayi – Masela - Wigelekelo inayohudumiwa na *TARURA* Wilaya ya Maswa yenye urefu wa kilomita 17.15. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala ya Barabara Vijijini na Mijini uliajiri Mkandarasi kwa ajili ya kujenga daraja la mawe kwa shilingi 87,220,000 ambapo kazi hiyo imeshakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilifanya ujenzi wa daraja dogo la mawe kwa gharama shilingi milioni 67.2 ambapo kazi hiyo imeshakamilika. Mwaka 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa daraja katika Mto huo. Mchakato wa ununuzi kumpata Mkandarasi atakayetekeleza mradi huu unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pindi ujenzi wa daraja katika Mto Tungu utakapokamilika utaunganisha vijiji vyote vitatu vya Mwasayi, Masela na Wigelekelo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ubovu wa barabara katika maeneo ambayo Mheshimiwa Ndaki ameyataja inafanana kabisa na hali ya ubovu wa barabara katika maeneo ya Mkinga, Wilaya ya Muheza na Tanga Mjini. Ni mkakati upi Serikali imeandaa kwa ajili ya kudhibiti hali hiyo katika maeneo yote hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kujenga kukarabati barabara zetu za *TARURA* kote nchini. Hata hivyo, tunafahamu katika kipindi hiki cha msimu wa mvua barabara nyingi za halmashauri zetu zikiwepo Halmashauri ya Maswa, Mkinga, Muheza na maeneo mengi kote nchini zimeharibiwa na mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ambazo Serikali imechukua, moja ni kuendelea na matengenezo ya barabara, madaraja na ma-*culvert* kwa dharura ili kuwezesha shughuli za kiuchumi kuendelea. Pili, tumeendelea kufanya tathmini ya gharama ya fedha inayohitajika kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo zilizoathiriwa na mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkakati wa Serikali uko thabiti kwamba tunaweka utaratibu mzuri baada ya mvua kukatika tutakwenda kuanza kutengeneza barabara hizi, madaraja na ma-*culvert* kwa awamu ili kurejesha hali ya usafiri katika hali yake ya kawaida.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haidary Sumry, swali la nyongeza.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Nswima ambayo inaunganisha majimbo matatu katika Mkoa wa Katavi; Jimbo la Mpanda Mjini, Jimbo la Nsimbo na Jimbo la Tanganyika katika eneo la Mtapenda na Kasokola imekatika kabisa. Nini kauli ya Serikali kurudisha mawasiliano katika eneo hili? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kumwelekeza Meneja wa

*TARURA* wa Mkoa wa Katavi, lakini pia wa Wilaya ya Mpanda, Nsimbo pamoja na Tanganyika wafike katika eneo hilo lililokatika wafanye tathmini na yafanyike matengenezo yatakayowezesha barabara kuendelea kutumika wakati tunasubiri matengenezo makubwa na huduma katika barabara hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Morris Makoi, swali la nyongeza.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Mawasiliano kati ya Kata ya Kirima na Kindi yamekatika tangu mwezi wa Nane mwaka 2025. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za dharura kurejesha daraja la kata hizo mbili ili mawasiliano yaendelee?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea maombi ya Mheshimiwa Makoi, Mbunge wa Moshi Vijijini kupitia Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ya Moshi na Mkoa Kilimanjaro na hivi sasa Serikali inaendelea na taratibu za kupata fedha ili kwenda kufanya matengenezo ya barabara hizo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hilo litatekelezwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Ni lini barabara ya kutoka Ilula kwenda Image mpaka Igumu itajengwa kwa sababu wananchi wamesubiri kwa muda mrefu, na sasa hivi magari yanakwama, nyanya zinaozea barabarani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ilula na ambayo inapita katika maeneo

ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja katika Jimbo la Kilolo ni moja ya barabara ambazo ni kipaumbele na ziko kwenye mtandao wa barabara za *TARURA* katika Wilaya ya Kilolo na Serikali inaendelea kuandaa fedha, lakini tunaendelea kusubiri hali ya hewa ya mvua zipungue ili tuanze matengenezo kwa awamu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwamba barabara hiyo itapewa kipaumbele.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Handeni, sasa aulize swali lake.

Na. 222

**Ujenzi wa Barabara ya Kwedikwazu – Sindeni kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Kwedikwazu - Sindeni inayopitia Daraja la Komdudu ambayo ipo kwenye Mradi wa *World Bank* kwa kiwango cha Lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, Mbunge wa Jimbo la Handeni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Handeni ni miongoni mwa wilaya zilizo kwenye mpango wa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kupitia Programu ya Mradi wa Uibuaji na ufunguaji wa fursa za kijamii na kiuchumi *(RISE)* inayofadhiliwa na Benki ya Dunia.

MheshimiwaNaibu Spika, Kupitia program hii, barabara ya Sindeni – Kwedikwazu yenye urefu wa kilometa 38 itajengwa kwa kiwango cha lami ikijumuisha ujenzi wa Daraja la Komdudu. Zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi mjenzi imeshakamilika na mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 24 Aprili, 2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Charles Jacob Sungura, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri. Kwa kuwa barabara ya Michungwani - Kwadoya yenye urefu wa kilometa 19 nayo ni sehemu ya utekelezaji wa barabara za awamu ya pili *(second road generation)* na zabuni barabara hii ishatangazwa, je, ni lini sasa Serikali itatoa barua ya tuzo *(letter of award)* ili ujenzi wa barabara hii nao uanze kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine la pili. Kwa kuwa barabara ya Mkata kwa Sunga yenye kilometa 21 nayo ni miongoni mwa utekelezaji wa barabara za *third generation road* wa *RISE,* sasa ni lini Serikali itatangaza zabuni ili ujenzi wa barabara hii nao uanze kwa kiwango cha lami? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Sungura, Mbunge wa Handeni, kwamba Serikali inatambua muhimu wa barabara hizo na ndiyo maana tayari tumeanza na hii barabara, na tayari zabuni imeshasainiwa, mkataba ushasainiwa tayari kwa kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunafahamu na hizo barabara nyingine mbili, moja ambayo Mheshimiwa Mbunge angependa ifanyiwe matangazo na mzabuni apatikane. Nimhakikishie tu kwamba suala hilo tumelichukua, tutalifanyia kazi kwa barabara zote mbili ili tuweze kutangaza zabuni kwa kadri fedha zitakavyopatikana kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Exaud Kigahe, swali la nyongeza.

**MHE. EXAUD S. KIGAHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Jimbo la Mufindi Kaskazini tuna mradi huu wa Kata ya Ifwagi, Mdabulo na Ihalimba. Ni lini Serikali itaanza kukamilisha ujenzi wa kilometa 16 kutoka Kata ya Ifwagi mpaka Mdabulo na kilometa 10 kutoka Kata ya Ifwagi mpaka Ihalimba? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kigahe, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, alishawahi kuwasilisha barabara hiyo na tayari Serikali ilianza hatua za ujenzi kwa awamu wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye bajeti kwa awamu kuhakikisha kwamba barabara hiyo inajengwa kwa awamu na kuhakikisha kwamba tunafikisha lengo la wananchi kupata usafiri mzuri katika Jimbo la Mufindi Kaskazini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salehe Muhando, swali la nyongeza.

*(Hapa microphone ilizimika)*

**NAIBU SPIKA:** Basi Mheshimiwa wakati unasubiri, Mheshimiwa Cornel Maghembe, swali la nyongeza.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili kuuliza swali la nyongeza. Katika mji maarufu wa Chato kuna zaidi ya kilomita nne ambazo tayari Serikali ilikuwa ianze ujenzi wake mwaka 2025, lakini mpaka sasa haujaanza kutekelezwa. Pia iko barabara ndogo pale Mji wa Mganza zaidi ya kilomita moja na nusu ambao nao ujenzi wake

haujaanza. Je, ni lini Serikali inakwenda kuanza ujenzi wa barabara hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa barabara hizi unafanyika kwa awamu na Serikali inaendelea kutenga fedha kwenye bajeti zake ili kila mwaka wa fedha tuendelee na hatua moja ya ujenzi ili kukamilisha ujenzi wa barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Chato Kaskazini kwamba Serikali itatekeleza azma yake na hadhi yake ya kujenga barabara hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kija Ntemi, swali la nyongeza.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara inayotoka Mererani kwenda Hospitali ya Wilaya ya Katoro imeharibika sana, siyo kwa sababu ya mvua tu, bali ni muda mrefu. Hata kama nilimwelezea Mheshimiwa Naibu Waziri, haitoshi. Je, yuko tayari baada ya Bunge hili tuambatane sote tukakague zile barabara na kuhimiza ili ziweze kujengwa kutoa huduma nzuri kuelekea katika hospitali ya Wilaya ya Katoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, niko tayari tuongozane na Mheshimiwa Ntemi kwenda Jimbo la Katoro ili tupitie barabara hiyo. Hata hivyo, ninaamini tayari ipo kwenye mipango yetu, tutakwenda kusukuma pia mipango hiyo ili barabara hiyo iweze kupata fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itajenga daraja linalounganisha Mji wa Mpwawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hujawasha kisemeo chako.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itajenga daraja linalounganisha Mji wa Mpwawa na Kijiji cha Iyomo, kwa kuwa kwa sasa hakuna mawasiliano kufuatia mvua kubwa zilizonyesha na kuharibu miundombinu ya daraja hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zetu zinapitika vizuri na madaraja yanajengwa ili kurahisisha huduma za usafiri kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nichukue hoja ya Mheshimiwa Malima, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, na nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mpwapwa wawasilishe tathmini ya mahitaji ya fedha ya daraja hilo ili Serikali iendelee na mipango yake ya kutafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga daraja hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

**29 APRILI, 2026**

Na. 223

**Vivutio vya Uwekezaji kwa Wawekezaji Wazawa**

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE** aliuliza: -

Je, Serikali imeweka vivutio gani vya uwekezaji kwa Wazawa ili kuwahamasisha kuwekeza zaidi nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Namba Sita ya Mwaka 2025, Serikali imeweka vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi kwa wawekezaji wazawa na wageni wenye leseni ya vivutio *(Certificate of Incentives)*. Wawekezaji hao wamegawanywa katika makundi mawili: wa kawaida na mahiri, kulingana na aina na kiwango cha mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wawekezaji wa kawaida, kiwango cha chini cha mtaji kwa wazawa ni dola 50,000 na kwa wageni dola 500,000. Kwa wawekezaji mahiri, kiwango cha chini ni dola milioni 20 kwa wazawa na dola milioni 50 kwa wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipunguza pia kiwango cha chini cha mtaji kwa wazawa kutoka dola 100,000 hadi 50,000, hatua inayolenga kuongeza ushiriki wa wazawa na kupunguza vikwazo vya kuingia kwenye sekta rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji hunufaika na urahisishaji wa huduma kupitia kituo cha pamoja, upatikanaji wa

ardhi, na miundombinu kama umeme, maji na barabara. Pia hupata vivutio vya kikodi kama punguzo au msamaha wa kodi kwa mitambo na vifaa vya uzalishaji, pamoja na ulinzi wa uwekezaji kwa mujibu wa sheria na mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mikubwa hupata vivutio maalum kupitia Kamati ya Kitaifa ya Uwekezaji *(National Investment Steering Committee - NISC)* ambayo ipo chini ya Waziri Mkuu, ikiwemo makubaliano ya kikodi na huduma za haraka za vibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inatoa vivutio vya ziada kwa wazawa, ikiwemo kipaumbele cha ardhi nafuu, fursa za mikopo na programu za kuwezesha biashara ndogo na za kati. Wazawa pia huhamasishwa kuingia ubia na wawekezaji wa kigeni na kunufaika na sera za *local content*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mshauri *Gatsby Africa,* Serikali inaandaa mwongozo wa Kitaifa wa vivutio vya uwekezaji ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongeza ushindani wa wawekezaji wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Neema, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pia kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, kuhusu vivutio ambavyo Serikali imevi-*identify* kabisa kwa ajili ya wawekezaji hasa wazawa, lakini kuna sheria za *TRA* ambazo bado zinakinzana na hivyo vivutio, ikiwepo hiyo *tax exemption* katika *import duty,* bado kuna shida lakini pia hiyo *tax holiday* ambayo amesema kuna *grace period,* inabidi wasubiri, bado kuna shida. Wenyewe *TRA*, wanaongozwa tu na sheria zao. Niulize sasa, je, Serikali imejipangaje ku-*harmonize* vivutio vyake na sheria za *TRA*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wawekezaji wengi wageni wameingia hapa kwetu na hivyo wawekezaji wazawa

wakiwepo wawekezaji wa kati na wadogo wanashindwa kuhimili ushindani wa uwekezaji wa nje. Je, Serikali imejipangaje kuwaandaa wawekezaji wetu wa ndani, wengi wao wakiwa ni wanawake na vijana, kuhimili ushindani wa kibiashara na wale wawekezaji wa nje? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Neema Peter Majule, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Mara kwa mara amekuwa akichangia sana kwenye suala la uwekezaji na hususan kuwatetea wanawake wa Dodoma kwenye masuala ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, hivi vivutio vimepitishwa na wenzetu wa Wizara ya Fedha, na *TRA* wamehusika katika kuvipitisha, lakini ninatambua kuna changamoto za hapa na pale katika *administration* ya hii *certificate of incentives* ambayo kimsingi sisi kama Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, vilevile tumekuwa tukipokea hiyo changamoto kutoka kwa wawekezaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, tumekuwa tukitatua hizi changamoto, na hivi tunaenda kutengeneza Muswada mwingine wa ile *Finance Bill* ambayo kimsingi tunakuja kutatua changamoto ambayo kimsingi inawakumba sana wawekezaji wetu hususan wale wanaopewa vile vivutio kwa kupitia ile *certificate of incentives*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kweli wawekezaji wetu wa ndani hususan akina mama wa Mkoa wa Dodoma na vijana wakati fulani wanashindwa kushindana kwenye soko la uwekezaji, kwa sababu mbalimbali ikiwepo mitaji na kadhalika. Sisi kama Serikali, sasa hivi tunaenda kuandaa mwongozo mahususi wa *incentives* kwa ajili ya wazawa tu ambao utatupa *way forward* ni jinsi gani sasa tunaweza tukawafanya wakawa *competitive* na

vilevile kuweka mazingira rafiki ya wao kupata mikopo na hata ardhi ili waweze kushindana na wawekezaji wanaotoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Feruz, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA J. FERUZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Je Serikali ina mkakati gani mahususi wa kuchukua hatua kwa wawekezaji ambao hawarudishi hii *CSR* katika maeneo yetu? Maana wapo wawekezaji ambao hawarudishi kabisa na wameshawekeza kwa muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Asha Feruz, kwa kuwatetea wananchi ambapo wawekezaji wetu wameweka miundombinu au uwekezaji kule wa kupitia *CSR (Corporate Social Responsibility)*. Ni kweli tunapokea changamoto kutoka kwa baadhi ya wawekezaji ambao hawa-*comply* na ile sheria yetu ya *local content* na tumekuwa tukishirikiana na Wizara za Kisekta, kwa sababu hii miradi ipo kwenye sekta mbalimbali; kwa watu wa ujenzi, kuna miradi kama hii, watu wa uchukuzi, watu wa kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali tupo *on top of that* na tutahakikisha tunashirikiana na Wizara nyingine ku-*address* haya matatizo tuhakikishe ile *CSR* sasa inalipwa kulingana na sheria ambayo imetungwa, ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Ofisi ya Makamu Wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 224

**Matokeo ya Katazo la Mifuko ya Plastiki**

**MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM** aliuliza: -

Je, Serikali imepata matokeo gani katika kupunguza uchafuzi wa mazingira tangu kuanza kwa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki mwaka 2019?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto za uchafuzi wa taka za plastiki na athari zake, Serikali ilipiga marufuku uingizaji nchini, uzalishaji, usambazaji, uhifadhi, usafirishaji nje ya nchi na matumizi ya mifuko ya plastiki kuanzia tarehe 01 Juni, 2019. Matokeo ya katazo hilo ni pamoja na:-

(i) Kupungua kwa zaidi ya 95% ya uzalishaji na uingizaji wa mifuko ya plastiki nchini, ambapo imechangia kupungua kwa uzalishaji wa taka za plastiki katika maeneo mbalimbali nchini;

(ii) Kuongezeka kwa kiwango cha uelewa wa wananchi kuhusu madhara ya plastiki kutoka chini ya 40% mwaka 2018 hadi kufikia zaidi ya 85% mwaka 2026;

(iii) Kupungua kwa takribani 60% ya taka za plastiki katika maeneo ya fukwe za bahari na maziwa ambapo hatua hii imepunguza hatari kwa viumbe wa majini;

(iv) Kupungua kwa gharama za kuzibua mitaro ya maji machafu kwa wastani wa 30% mpaka 40%, kwani mifuko ya plastiki ilikuwa chanzo kikuu cha uzibaji wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba nitoe rai kwa wananchi kuendelea kuzingatia katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki la mwaka 2019 kwa ajili ya kulinda afya na kuhifadhi mazingira yetu kwa maendeleo endelevu ya kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Catherine Canute Joachim, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CATHERINE C. JOACHIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuainisha mafanikio ambayo yamepatikana katika udhibiti wa taka za plastiki. Nina maswali mawili ya nyongeza ambayo yatajikita katika eneo namba nne, lililosemwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, kuhusiana na gharama za kupunguza udhibiti wa taka za plastiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza. Kwa kuwa miundombinu ya kukusanyia takataka pamoja na vile vituo vya urejelezaji wa taka za plastiki ni vichache, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza miundombinu hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili litajikita katika ongezeko la viwanda, ambalo tumeona linakwenda sambamba na ongezeko la vifungashio vya plastiki pamoja na chupa ambazo hutumika mara moja. Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti ongezeko hili la vifungashio vinavyotumika mara moja bila kuathiri ukuaji wa viwanda hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa maswali haya ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Catherine Joachim, Mbunge anayetokana na Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi. Ninatambua kwamba Jumuiya ya Wazazi moja ya kipaumbele chake ni kulinda na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yake ya nyongeza ninaomba niyajibu yote kwa pamoja. Sheria yetu ya Mazingira Sura 191, tuliitungia kanuni Kifungu kile cha 230, kifungu cha 2(f). Kanuni zile ndiyo zilihusu haya makatazo ya matumizi ya mifuko ya plastiki na hususan vifungashio vya plastiki, kwa kutambua umuhimu wa sekta za kilimo ambazo zina mahitaji makubwa ya matumizi ya plastiki, vilevile sekta za ujenzi ambazo zina matumizi makubwa ya mahitaji ya plastiki, sekta za vyakula kwa maana ya vifungashio, viwandani kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa Mbunge, lakini vilevile sekta za afya, pamoja na kwenye usimamizi wa taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni zile ambazo tulizitunga chini ya kifungu hicho cha Sheria ya 230, ziliweza kuruhusu maeneo haya baadhi ya wazalishaji kupewa kibali kwa ajili ya kuzalisha plastiki hizo kwa matumizi hayo ambayo ni muhimu ndani ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho tumekifanya kama Serikali kwenye kanuni zile ambazo tumezitunga, tumeweka pia na wajibu wa wazalishaji wa plastiki hizo, wasafirishaji, wanaohifadhi, wanaosambaza na wanaotumia, tumewapa wajibu wa kuhakikisha pia wanashiriki kwenye kukusanya na kuteketeza taka hizo ambazo zinakuwa zimetokana na bidhaa ambazo wamehusika nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kuimarisha pia miundombinu ya ukusanyaji wa taka hizi. Sheria ile ambayo tuliitunga, Sheria ya Mazingira Sura 191 imezipa Mamlaka za

Serikali za Mitaa jukumu la kusimamia taka ngumu. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, pia tunahakikisha pana miundombinu kila mahali, kwenye miji yetu na kwenye majiji yetu kwa ajili ya uhifadhi wa taka hizi ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Kapoma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninataka niulize swali dogo la nyongeza. Nchi nyingi kwa sasa zimeshapiga hatua kubwa sana katika kubadilisha taka kuwa fursa za kibiashara. Je, Serikali ina mkakati gani wa kujielekeza katika mlengo huu ili kutokomeza hili suala la uchafuzi wa mazingira? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mbunge wa Mkoa wa Morogoro kwa swali lake zuri, na amekuwa msemaji mzuri sana kuutetea Mkoa wa Morogoro pamoja na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuweka jitihada kubwa katika kuhakikisha kwamba taka zinazozalishwa kwenye mazingira ya shughuli zetu za kiuchumi kwenye miji yetu, kwenye majiji na maeneo mbalimbali zinakuwa *recycled*, yaani zinarudishwa kutumika kwa ajili ya kuzalisha bidhaa ambazo zitatumika tena kwenye mzunguko wa uzalishaji kwenye maeneo mbalimbali ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali inahakikisha kwenye majiji makubwa, mathalan kama ilivyo Dar es Salaam inajenga madampo makubwa na ambayo yataambatana na miundombinu ya viwanda vitakavyoendelea kufanya *recycling*, yaani marejeo na marejesho ya hizo taka ili ziweze kutumika tena

kwa ajili ya kuzalisha bidhaa zitakazotumika kwenye maeneo yetu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mbunge wa Kibiti, sasa aulize swali lake.

Na. 225

**Kukamilisha Ujenzi wa Chuo cha *VETA* Kibiti**

**MHE. AMINA M. MKUMBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* katika Jimbo la Kibiti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Wanu Hafidh, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Kibiti ni miongoni mwa ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi 65 vinavyoendelea kujengwa katika wilaya 64 na Mkoa mmoja wa Songwe. Ujenzi huo unafanyika katika wilaya au mkoa ambao hauna Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Kibiti ambacho kinatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2026. Hadi sasa Serikali imeshatumia jumla ya shilingi bilioni 1.1 kati ya shilingi bilioni 1.6 zilizotengwa

kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza. Mpaka sasa ujenzi huo umefikia 69% ya utekelezaji wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA M. MKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, na pia ninaipongeza sana kwa mpango wake wa ujenzi wa vyuo vya *VETA* katika wilaya 64 ikiwemo Wilaya ya Kibiti. Nina imani kubwa na Mheshimiwa Naibu Waziri na ninaamini ujenzi wa chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Kibiti utakamilika katika muda uliopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina swali la nyongeza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge, nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri kama una la kusema au umemaliza? Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, samahani kuna swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Charles Njama, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Chuo cha Ualimu Korogwe ni chuo kikongwe na cha muda mrefu, lakini hadi leo hakina uzio. Je, yupo tayari kwenda kutembelea chuo kile na kuanza ujenzi wa uzio katika chuo cha ualimu Korogwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa kufuatilia maendeleo ya Chuo cha Ualimu cha Korogwe na nimwambie kwamba nipo tayari kwenda kutembelea chuo hicho na kuona namna gani tutaweza kusaidia kujenga uzio wa chuo hicho.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea Wizara ya Maji, Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, Mbunge wa Kakonko, sasa aulize swali lake.

Na. 226

**Utekelezaji wa Mradi wa Kisima Kijiji cha Kihomoka**

**MHE. ALAN T. MVANO** aliuliza: -

Je, lini Mkandarasi atakamilisha kuchimba na kujenga kisima cha maji katika Kijiji cha Kihomoka kama ilivyo kwenye mkataba wake?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, Mbunge wa Jimbo la Kakonko, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipanga kuchimba visima vitano katika Wilaya ya Kakonko kupitia programu maalumu ya uchimbaji wa visima 900. Hadi sasa jumla ya visima vinne kati ya vitano vimechimbwa katika Kijiji cha Ruhuru viwili, Kihomoka kimoja, na Nyamtukuza kisima kimoja, ambapo kwa pamoja vina uwezo wa kuzalisha jumla ya maji lita 55,500 kwa saa.

Mheshimiwa Naibu Spika, visima hivyo baada ya kupata maji vimeendelezwa kwa kujengewa miundombinu rahisi ya kutolea huduma kwa wananchi *(point source)* na vinaendelea kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wakazi wa vijiji hivyo. Hata hivyo kisima kimoja kilichokuwa kimepangwa kuchimbwa katika Kitongoji cha *Centre B* kilichopo Kijiji cha Kihomoka hakikuweza kuchimbwa. Hivyo, Serikali imekiingiza kisima hicho kwenye mpango wa programu ya vijiji 1,575 visivyokuwa na huduma ya

maji ambayo inaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, swali la nyongeza.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali na jitihada hizo, ninaamini Waziri atakuwa tayari kuongozana na mimi kwenda Kakonko ili aweze kujionea hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ilivyo, lakini pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Katika Kijiji cha Kihomoka wapo wananchi wanaishi eneo linaitwa Nabulilije na wanatembea kilometa 10 kufuata huduma ya majisafi na salama. Sasa ni upi mpango wa Serikali wa dharura kuhakikisha kwamba wananchi hawa sasa wanapata huduma hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Wafanyakazi wa Serikali, wa *RUWASA* pamoja na Mamlaka ya Maji wamekuwa wakipata shida sana kutembea katika Wilaya ya Kakonko katika kushughulikia changamoto za maji. Ni upi mpango wa Serikali kuhakikisha sasa wanapelekewa gari ili waweze kufanya shughuli zao vizuri na wananchi wapate huduma ya maji? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninakubaliana na ombi la Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, Mbunge wa Kakonko. Niko tayari kuongozana naye kwenda Kakonko, ili kujionea hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Sana Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi na ufuatiliaji wa miradi, kwa ajili ya wananchi wake waliomtuma kuhakikisha kwamba, tunamtua mama ndoo kichwani. Sisi Serikali tunaahidi kumpa ushirikiano

mzuri kabisa kuhakikisha kwamba anatimiza azma yake ya kuwatumikia Wanakakonko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ambao Mheshimiwa Mbunge amesema, ni kweli kabisa Kijiji cha Kihomoka kina *centre* mbili. *Centre* ya kwanza tulichimba kisima, tukajenga miundombinu na tayari wanapata huduma nzuri kabisa, lakini *Centre B* ambayo ni kilometa 10 kuna wafugaji zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyojibu katika jibu la msingi, tunaiingiza kwenye programu ya vijiji 1,575 katika mwaka wa fedha 2026/2027, ili sasa tuchimbe kisima kwa kutumia mitambo ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alinunua katika mikoa yote 26. Itaenda kufanya hiyo kazi bila kuwa na changamoto yoyote na wananchi wa Kakonko watapata huduma ya majisafi na salama, hasa katika eneo la Kihomoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kulitazama suala la vitendea kazi. Vitendea kazi hivi vinasaidia sana watendaji wetu katika utekelezaji wa miradi, katika usimamizi wa miradi na katika shughuli mbalimbali za kiofisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua umuhimu huu na Mheshimiwa Mbunge amefika mpaka kwa Mheshimiwa Waziri na ameongelea kuhusu hili suala. Ninataka nimpe Mheshimiwa Mbunge habari njema, kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupatia fedha kwa ajili ya kununua magari 29 mapya ili kwenda kuwasaidia watendaji wetu kutekeleza majukumu yao. Ninamtoa hofu *DM* wa Kakonko, yupo kwenye orodha hiyo ya kupatiwa gari, ili aweze kusimamia miradi vizuri na iwe na tija kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Baraka Ulimboka, swali la nyongeza.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa Miradi

ya *Angana Group*, Miradi ya *Mbambo Group* ndani ya Jimbo la Kyala ambayo imekwama kwa muda mrefu wakandarasi hawajalipwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamtoa hofu Mheshimiwa Mbunge, tunao mpango, tumepanga vipaumbele na miradi ambayo ipo katika utekelezaji tunayo. Tunayo maelekezo ya kuhakikisha kwamba, tunakamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutaongeza nguvu ya kupeleka fedha ili wakandarasi warudi, ambao wamekuwa wanasuasua, waweze kuongeza *speed* ya utekelezaji wa miradi hiyo, ili iweze kukamilika na wananchi waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edward Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumewaeleza Vijiji 12 vya Kiteto ambavyo havina majisafi na salama. Ninajua bajeti yetu inakuja, sasa ni nini kauli ya Serikali kwa Vijiji 12 vya Kiteto ambavyo havina maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika majibu mengine kuhusiana na vijiji katika vijiji 12,318 nchi nzima, tunavyo vijiji 1,575 tu vilivyobaki. Hivi vijiji 1,575 tunaweka programu maalum ya utekelezaji kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, hivi vijiji 1,575 tumevigawa kwa awamu na kila awamu itagusa kila jimbo na kila mkoa kuhakikisha kwamba, tunaendelea kutekeleza awamu kwa awamu, lakini kila jimbo

linakuwa linaguswa kila awamu, ambayo tunakuwa tunaitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamtoa hofu Mheshimiwa Mbunge, vijiji hivyo 12 tutavigawa kwa awamu, kama viko 12, basi tutaviweka viwili vitatu kila awamu, mwaka wa fedha, tunapokamilisha tunaingia awamu nyingine. Tuna uhakika itakapofika mwaka 2030 vijiji vyote 1,575 kuweka *total* ya 12,318 vitakuwa vimekamilika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, Mbunge wa Rungwe, sasa aulize swali lake.

Na. 227

**Mradi wa Maji Kijiji cha Mpandapanda, Kata ya Kiwira**

**MHE. ANTON A. MWANTONA** aliuliza: -

Je, lini Mradi wa Maji katika Kijiji cha Mpandapanda, Kata ya Kiwira, utaanza kutekelezwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Mpandapanda kilichopo Kata ya Kiwira kinapata huduma ya majisafi na salama kupitia mradi uliotekelezwa kijijini hapo mwaka 2021/2022 kupitia fedha za UVIKO 19. Kiasi cha shilingi milioni 306.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha zaidi huduma ya maji Kata ya Kiwira, Serikali imekamilisha usanifu wa mradi mkubwa utakaotumia chanzo cha maji cha Mto Katalifu unaolenga kunufaisha vijiji vyote vinne vya Mpandapanda, Kikota, Ilundo na Ibula. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 5.2.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anton Albert Mwantona, swali la nyongeza. Ninaomba mliowasha kisemeo mzime kwanza, ili Mheshimiwa mwenye swali la msingi aweze kuuliza swali la nyongeza.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa majibu ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mradi wa Masoko, Awamu ya Pili, ambao ulikuwa unahudumia Vijiji vya Irima, Ndulu pamoja na Omburi. Mradi huu ulianza, lakini kwa bahati mbaya sana mkandarasi ameondoka kwa sababu ya kutolipwa fedha za awali. Je, ni lini mtamlipa mkandarasi fedha za awali, ili mradi huu uendelee kutekelezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kuna miradi sita katika Jimbo la Rungwe, ambayo imesimama kutokana na wakandarasi hajalipwa fedha zao. Ninaomba nijue Serikali inakwenda kuwalipa lini wakandarasi fedha hizo, ili miradi iweze kuendelea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninampongeza sana Mheshimiwa Anton Albert Mwantona kwa kazi nzuri anayoifanya kwa kuwasemea wananchi wa Rungwe, ili wapate huduma ya majisafi na salama, lakini yaliyo toshelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote, upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama Jimbo la Rungwe kwa sasa ni 76.5%, lakini pia, pamoja na miradi ambayo amesema iko sita, ndani ya Jimbo la Rungwe tunayo miradi 10. Kuna uwekezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita wa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 12.9 kwa hiyo, ninamtoa hofu katika eneo hilo, sisi tumejizatiti, tumejipanga kwenda kuhakikisha kwamba, miradi yote ambayo imeanza tunaenda kuhakikisha inakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa ambayo sasa tunaifanya ni kuangalia vipaumbele. Tunapoangalia vipaumbele vya Kitaifa, tunapokuja kwenye jimbo, tunaangalia mradi upi tuanzenao, ukamilike, utoe matokeo, halafu tufuate mradi mwingine kwa hiyo, tutakaa Mheshimiwa Mbunge, ili tuweze kupanga vipaumbele vya jimbo lake na ili tuweze kuweka msukumo wa kupeleka fedha miradi ikamilike kwa hatua kwa sababu, hatuwezi kukamilisha kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, suala la Mradi wa Masoko, Awamu ya Pili, mradi huu tunatambua kwamba ni msingi wa uchumi wa eneo la Rungwe. Tunauchukua kwa uzito mkubwa sana. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea kuandaa malipo kwa ajili ya mkandarasi ili apatiwe hizo fedha akaanze huo mradi haraka sana. Lengo ni kwamba, wananchi wa Rungwe wapate huduma ya majisafi na salama. Tunavyo vipaumbele hivyo, kwa ajili ya wananchi wake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona muda wetu umekwenda sana. Mheshimiwa Kakulu Kakulu, swali la nyongeza.

**MHE. KAKULU B. KAKULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu linahusiana na Jimbo langu la Mbagala. Ziko kata kadhaa ambazo zilikuwa na miradi ambayo wananchi walianzisha wenyewe na wakati ikiwa mikononi mwa wananchi, imefanya kazi nzuri sana. Baada ya kuchukuliwa na *DAWASA* kumekuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya Kata ya Kijichi, Kata ya Mbagala na Kata ya Mbagala Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Naibu Waziri atupe hakikisho, je, Serikali iko tayari kuirejesha hiyo miradi kwa wananchi ili tui-*manage* wenyewe na tuendelee kupata maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nisiwe mwongo, kwa usimamizi wa miradi ya maji na huduma ya maji tunaenda sambamba na maelekezo ya sera yetu. Sera yetu inaturuhusu, kwanza Serikali kusimamia miundombinu na pia, kuhakikisha maji yanatoka na ni salama *(secure of water)*, lakini pia, yawe toshelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, tunapoongelea maji, ni usalama wa Taifa, tunaangalia namna ambavyo tunaweza kushirikisha wananchi kwenye *ownership* ya kujua mradi ni wa kwao, lakini usimamizi wa mradi bado utabaki katika mamlaka ambayo imetamkwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamtoa hofu, kama kuna jambo na changamoto za usimamizi wa miradi hiyo, sisi tutatuma timu yetu, itaenda kufanya tathmini na kuangalia wapi kuna tatizo ili tuweze kutatua, lakini siyo kurudi kule ambako hatuwezi kufika tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ina *sensitivity* yake, kwa hiyo, tukisema kwamba, kwa mujibu wa Sheria yetu Na. 5 ya Mwaka 2019, ambayo ndiyo ilianzisha Wakala wa Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira, ndiyo yenye jukumu la kisheria la kusimamia na kuendeleza huduma za maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye hili naomba nisiseme uongo kwamba tutawarejeshea wananchi, hilo tutakuwa tunavunja sheria. Kikubwa ni kwamba tutawashirikisha wananchi kwenye kuelewa na kuwa na upana wa kujua nini maana ya miradi ya maji na nani anatakiwa kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza, ninaipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyoifanya kuhakikisha Wilaya ya Karatu inapata majisafi na ya

uhakika. Natambua kesho Mheshimiwa anaenda kufanya uzinduzi wa Mradi wa Maji wa Joba Chibumbe Chani, pale Karatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba, kuna Vijiji vya Apakitete na Tahamo katika Kata ya Mbulumbulu, Wilayani Karatu, pamefanyika majaribio kadhaa ya kuchimba maji bila mafanikio kwa hiyo, inahitajika fedha kwa ajili ya kufanya utafiti maeneo ya mbali kama kuna maji ili waweze kuchimba. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo kwa ajili ya utafiti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Serikali inapochimba visima inafanya majaribio. Sehemu nyingi tumepata changamoto. Tunachokifanya ni kwamba tunatafuta miradi iliyoko karibu na vijiji husika, tunafanya stadi, tunafanya usanifu na tunafanya *cost benefit analysis* ya kuangalia eneo lingine ambapo tunaweza tukachimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeweka mpango mzuri na tunauingiza kwenye Mpango huu wa Bajeti wa Mwaka 2026/2027, ili sasa tupeleke fedha, Serikali ikaangalie eneo lingine la kuchimba ama kutengeneza mradi uliopo karibu na vijiji hivyo, uwekewe miundombinu ya kufikisha huduma ya majisafi na salama katika vijiji ambavyo havina maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lengo ni jema kabisa na ninakushukuru sana kwa swali hili zuri kabisa ambalo linalenga kuwasaidia wananchi wake, na kweli, kesho ni juhudi zake pia, pamoja na Wabunge wenzake katika eneo ambalo tunaenda kuzindua mradi huo ambao tunaamini kwamba atakuwa ni *game changer* katika eneo la Karatu, asante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Marirta Gido Kivunge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

No. 228

**Kukamilisha Ujenzi wa Miradi ya Maji, Arusha**

**MHE. MARIRTA G. KIVUNGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Miradi ya Maji iliyosimama kwenye Halmashauri za Wilaya ya Meru, Longido na Monduli?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha inakamilisha utekelezaji wa miradi ya maji yote inayoendelea na ile iliyosimama kote nchini, ikiwemo miradi sita inayoendelea katika Halmashauri za Wilaya za Meru, Longido na Monduli. Miongoni mwa miradi inayoendelea katika wilaya hizo ni pamoja na Mradi wa Maji Kikatiti, Samaria; Mradi wa Maji Kata ya Uwiro iliyopo Wilaya ya Meru; Miradi ya Maji Tingatinga na Ketumbeine, Wilaya ya Longido, sambamba na mradi wa maji unaolenga kunufaisha vijiji 13 vya Wilaya ya Monduli.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo yote kwa pamoja inagharimu zaidi ya shilingi bilioni 38.7, ambapo hadi mwezi Machi, 2026 zaidi ya shilingi bilioni 5.8 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji. Mpango wa Serikali ni kuendelea kutoa kipaumbele cha kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kadiri zinavyopatikana, ili iweze kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, swali la nyongeza.

**MHE. MARIRTA G. KIVUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Serikali imekiri miradi hiyo imesimama. Je, haioni haja ya kutoa fedha za dharura kwa ajili ya kukamilisha miradi hii, ikiwemo Miradi ya Sepeko, Meserani Wilayani Monduli na Miradi ya Maji ya Chai, Kikatiti, Wilayani Arumeru na Mradi wa Maji Tingatinga, Wilayani Longido?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni nini mpango wa Serikali, Mkoani Arusha, kuwapatia mipango ya kuchimba visima na mabwawa, hususan kwenye Wilaya kame za Monduli, Longido na Ngorongoro, kwani mtambo mmoja uliotolewa hautoshelezi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Marirta Gido Kivunge, kwa kuendelea kuwasemea wananchi wa Mkoa wa Arusha, hasa akinamama. Pia, ninampongeza sana kwa kushirikiana na Wabunge wa Majimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika swali lake la nyongeza amegusa karibia majimbo matatu, kwa Mheshimiwa Isack Copriano, kwa Mheshimiwa Nassari pale na naona amegusa kwa Mheshimiwa Dkt. Kiruswa. Maeneo haya yote tumeyaona na kwamba, hata kwenye ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mbunge alisimama na kuonesha umahiri kabisa kuwasemea wanawake wa Mkoa wa Arusha. Kwa hiyo, ninampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, tunayo mambo matatu, miradi karibia mitatu. Mradi wa Vijiji 13 kutoka Ngaramtoni kwenda Monduli, una gharama ya shilingi bilioni 20.3 ambapo Mheshimiwa Copriano ni shahidi. Serikali tayari tumeingia *tripartite* kati ya Serikali, *Pipe Industry* pamoja na mkandarasi, ambaye ni *Jandu Plumbers,* ambapo sasa tumekubaliana kwamba, waanze kuzalisha mabomba ya chuma. Lengo ni kwamba, mradi usisimame.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge tulimwalika akaenda kukagua mabomba, na yeye tunamwalika, akipata nafasi akashuhudie mabomba ambayo yataenda kulazwa kutoka Ngaramtoni mpaka maeneo ya Monduli. Kwa hiyo, mradi huo umeshafikia asilimia nzuri kabisa ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Mradi wa Kikatiti, kwa Mheshimiwa Nassari pale, wenye gharama ya shilingi bilioni nne, mpaka sasa mradi huu umefikia 40% ya utekelezaji wake na mkandarasi yuko *site* anaendelea na kazi. Mradi huu unatakiwa kukamilika Disemba, 2026. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, tuko ndani ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ameongelea kuhusu eneo la Tingatinga, kwa Mheshimiwa Kiruswa kule. Eneo hili mradi huu umefikia 56%.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua tunaye Mkandarasi anaitwa Serengeti, kidogo alisuasua japo amelipwa fedha, tumeshamwandikia barua ya onyo ili ahakikishe kwamba anaongeza *speed* ili mradi huu uweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge amegusia kuhusu Halmashauri kame, tunayo mitambo ya aina mbili. Tunayo mitambo ya kuchimba visima ambayo ni seti 26 ambazo Rais alinunua, na pia tunayo mitambo ya kuchimba mabwawa. Mitambo hiyo imeshaanza kufanya kazi na hata Monduli kuna bwawa ambalo limetumia mitambo ya Rais, ile seti ya kuchimba mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kuhakikisha kwamba kwenye programu ya vijiji 1,575 mitambo hii ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliinunua kwa dhamira ya kumtua mama ndoo kichwani, tunaenda kusimamia utekelezaji wake ili wananchi wa Mkoa wa Arusha ambao yeye amekuwa sauti yao pamoja na Wabunge wote, tutahakikisha tunawapelekea neema ya tabasamu ambayo Rais aliahidi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Jasmine Chesco Ng'umbi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 229

**Mafunzo ya Kitaalam katika Sekta ya Uchukuzi kwa Vijana**

**MHE. JASMINE C. NG'UMBI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mafunzo ya kitaalamu wahitimu wapya katika sekta ya uchukuzi ili kuongeza ajira?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasmine Chesco Ng'umbi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi na taasisi zake, inao utaratibu wa kuwapatia vijana wanaohitimu elimu ya juu mafunzo ya vitendo kupitia utaratibu wa ajira za muda mfupi za miezi sita hadi 12 baada ya kuhitimu, yaani *(internship)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia *LATRA,* Wizara imeanzisha utaratibu wa kusajili mawakala wa kutoa leseni za usafirishaji kwa pikipiki za magurudumu mawili na matatu nchi nzima, ikiwa ni njia mojawapo ya kuongeza ajira kwa vijana. Hadi sasa, jumla ya mawakala 15 wamesajiliwa, wakiwemo vikundi vya kijamii, vyama vya ushirika na makampuni ambayo kwa pamoja yameajiri vijana zaidi ya 315.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, upo utaratibu unaotekelezwa na *LATRA* tangu mwezi Juni, 2022, kwa ushirikiano na vyuo mbalimbali kama Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT)*, Chuo cha Ufundi Arusha, Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* na Vyuo vya *VETA* kutoa mafunzo ya uhudumu wa mabasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia mwezi Februari, 2026 wahudumu 6,123 walishapewa mafunzo ambapo kati yao wanawake walikuwa 3,303 na wanaume walikuwa 2,820. Kati yao, wahudumu 3,722 walishapata usajili wa *LATRA* kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii imewaongezea thamani ya ajira zao waliokuwa kazini, kutoa ajira mpya na kuboresho vipato vyao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jasmine, swali la nyongeza.

**MHE. JASMINE C. NG'UMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kumekuwa na tatizo kubwa la ajali za bodaboda kutokana na hawa vijana wetu. Sasa ningependa kujua, Serikali haioni haja ya kutenga dawati maalum au kitengo maalum katika hospitali zetu, kuwasaidia hawa vijana wanaopata ajali za bodaboda ili wawe wanapewa kipaumbele au wanapata huduma za haraka wanapopata ajali hizi, kwani hawa vijana vifo vyao vimekuwa ni vingi sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Tunaelewa kama sasa Tanzania yetu imekumbwa na teknolojia, na vyuo vyetu vinavyotoa elimu juu ya udereva vimekumbwa na teknolojia. Sasa kutokana na ukuaji wa teknolojia, ningetamani kujua, je, Serikali haioni haja ya kuwasaidia hawa wahitimu wanaomaliza kila siku kwenye vyuo vyetu, kuwapatia elimu ya kisasa zaidi ili wanapopata ajira baada ya kuhitimu katika vyuo vyao, kuweza kuwa madereva mahiri na kuweza kuutumia ujuzi huo walioupata kwa umahiri zaidi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Jasmine Chesco Ng'umbi kwa jinsi ambavyo amejitoa kuamua kuwasemea vijana wenzake wa nchi hii haswa kundi la bodaboda. Ninakubaliana na ushauri wake kuhusu umuhimu wa kuweza kuwa na mkakati maalum wa kuwatazama hawa vijana wanaopata ajali, kwa sababu ni nguvu kazi ya Taifa. Wanapata ajali wakiwa wanakwenda kuhangaika kutafuta riziki za familia zao na kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kupitia Wizara yetu ya Afya, ninaamini jambo hili wamelipokea, wataona namna bora ya kuweza kulifanikisha, na sisi kama Sekta ya Uchukuzi tutakuwa tupo tayari kwa ajili ya kulifanikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mheshimiwa Mbunge amezungumza kuhusiana na teknolojia namna gani ambavyo tunaweza kushiriki kikamilifu kuhakikisha kwamba vijina wetu mafunzo tunayowapatia, yanakuwa yanakidhi teknolojia ya sasa. Ni kweli hata hivi karibuni tumeshuhudia baadhi ya madereva wakipelekwa nje ya nchi. Teknolojia waliyojifunzia hapa kwetu wakienda huko inakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea ushauri huu, tunauingiza Serikalini kuanza kuuchakata. Nitumie nafasi hii kutoa maelekezo kwa Chuo chetu cha Taifa cha Usafirishaji ili waendelee kutoa mafunzo ambayo dereva au kijana akipata mafunzo huku kwetu, akienda mahali pengine popote duniani, aweze kufiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe rai na maombi kwa vyuo vingine na taasisi nyingine ambazo zinatoa mafunzo ya namna hiyo, ili kuweza kutazama mabadiliko ya teknolojia. Wahitimu mnaowatoa hapa waweze kuwa *competitive* mahali popote wanapokwenda duniani.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Shangazi Rashid, swali fupi la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la udereva ni taaluma kama zilivyo taaluma nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, madereva wengi wanapata mafunzo kabla ya kupata leseni, lakini sasa hivi kumekuwa na usumbufu sana kwamba, madereva wa magari ya mizigo, lakini pia na magari ya abiria wanapokwenda ku-*renew* leseni zao wanalazimika tena kurudi darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kujua, Serikali haioni kwamba hii taaluma ya udereva ni kama inapata changamoto ya unyanyasaji hasa wakati wanapo-*renew* leseni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwenzangu wa Wizara ya Mambo ya Ndani atalielezea kwa kina, pengine jambo la leseni, lakini sisi kwetu Sekta ya Uchukuzi tunathibitisha madereva. Tumeweka utaratibu kufuatia ajali nyingi nchini ambapo Watanzania wengi wanakufa pia wakiwa hawana makosa. Tumeamua kufanya utaratibu wa kuthibitisha madereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili limepitisha Sheria Sura ya 413 ya Kifungu cha 5(1)(d) kuhakikisha kwamba *LATRA* imepewa mamlaka, dereva anarudi anafanya mtihani na kisha akithibitishwa anakwenda kuendelea kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuhakikisha kwamba wale madereva wanakuwa *competitive,* tunawapima. Utaratibu huu kwa wanaotoa huduma mbalimbali kwenye nchi yetu, hufanya hivyo. Kwa mfano, madaktari pamoja na kusomea kwa miaka mitano, bado wanapata leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda hata kwa wanasheria, wanasimama Mahakamani, pamoja na kusoma vizuri, bado wakienda Mahakamani kule kila mwaka wanapata leseni ili waweze kuthibitishwa. Hata ukienda kwa Wahandisi, pamoja na

kusoma, lakini bado wanapata vyeti vyao vile vya kutambulika rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lengo letu ni jema ili kuona yule dereva je, kweli taaluma hiyo anayo? Alipata leseni kwa namna ambayo iko sahihi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa madereva wanapokuja wameshawekewa *LATRA* imejenga mfumo, imeweka maswali karibu 1,000 wanayasoma mara kwa mara, kisha anapewa masaa matatu anafanya. Akipata 70% *automatically* sasa anaweza kuthibitishwa na kuendelea na kazi yake. Akifeli mara tatu, huyo dereva anarudishwa kwenda kujifunza upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tumeanza mfumo huu takribani madereva 7,599 wamefanya mitihani na 54% wamefaulu, wale ambao hawakufanya vizuri tayari wanaelekezwa namna ya kufanya. Sasa wanaweza kufanya mitihani hii nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba taaluma hii ya madereva wanaobeba abiria 60 wanakuwa ni watu wenye weledi, wenye uwezo ili kulinda uhai wa watu wetu kama ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita ilikuwa imeahidi kulinda raia na mali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi sasa aulize swali lake.

Na. 230

**Kufufua Mashamba ya Ngano Nchini**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua mashamba yaliyokuwa ya ngano nchini ili kuweza kukidhi mahitaji ya ngano nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais, Uwekezaji na Mipango na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeandaa mpango wa uendelezaji wa mashamba ya kilimo ikiwemo yale yaliyokuwa ya *NAFCO* yanayojumuisha mashamba ya ngano ya Basutu. Kupitia mpango huo, miongoni mwa hatua zilizopangwa ni kutafuta wawekezaji mahiri *(strategic investors)* wenye uwezo wa kuendeleza mashamba hayo kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali imepanga kufanya ufuatiliaji wa wawekezaji waliobinafsishwa mashamba yao ya Ngano ya *Setchet, Gidagamowd* na *Murjanda* chini ya kampuni ya Ngano *Limited* ili kubainisha changamoto na kutoa mapendekezo ya kisera yatakayowezesha uendelezaji endelevu wa mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji wa ngano nchini kupitia mikakati mbalimbali ikiwemo kubainisha maeneo mapya ya uzalishaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Ingawa leo ni mara yangu ya pili nauliza swali kuhusu kufufua mashamba yaliyokuwa yanazalisha ngano, lakini ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri. Sasa nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa, ngano inaonekana ni moja ya mazao muhimu ya chakula nchini na tunahitaji takribani tani 1,000,000 kwa mwaka na uzalishaji wetu

wa ndani ni chini ya tani 200,000, kwa maana hiyo karibu 90% ya ngano tunaagiza nje kwa fedha za kigeni; sasa pamoja na mikakati mizuri ambayo Serikali imetueleza, haioni sasa umuhimu wa kuifanya ngano kuwa moja ya mazao ya mkakati nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wakati wa ziara ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkoa wa Manyara, Wilayani Hanang', tarehe 3 Oktoba, 2025 aliwaahidi Wanahanang kupitia upya mikataba ya wawekezaji katika mashamba ya ngano ili kubaini changamoto na wale ambao hawaendelezi wachukuliwe hatua. Je, ni lini ahadi hii ya Rais itatekelezwa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Yustina Rahhi kwa maswali mazuri ya ngano, bahati nzuri amekuwa ni mfauatiliaji mzuri hata kuanzia katika *level* ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja tu ambalo ninaweza kumweleza yeye na wakulima wa ngano kwamba Serikali imeweka miongoni mwa mazao ya kimkakati ambayo tunakwenda kutekeleza katika mwaka huu wa fedha 2026/2027 ambao ndiyo tunaendelea kuupitisha hapa, ni pamoja na zao la ngano. Kwa hiyo, tayari tumeshaliweka katika bajeti, na yale mazao manne ambayo mwaka 2026 tutayapa msukumo mkubwa, ngano ni miongoni mwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wetu wa kwanza ni kweli tutazalisha kama wastani wa tani 110,000, tunataka katika mwaka huu wa kwanza tufikishe walau tani 200,000 na tutaendelea kutoa ikiwemo mbegu za ruzuku bure katika maeneo yale ambayo wanazalisha ngano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tutaainisha maeneo mapya yakiwemo maeneo ya Njombe, Iringa na tutafanya tafiti katika maeneo ya Tanga na Morogoro ili kuongeza eneo ambalo

litafaa kwa ajili ya uzalishaji wa ngano. Kwa hiyo, lipo na tumelipa kipaumbele kikubwa ikiwemo katika bajeti hii ambayo tunakwenda kuipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu maelekezo ya Rais, ndiyo maana nimeeleza katika jibu la msingi tunaendelea na tathmini na tukishamaliza tutatoa majibu na tutafikisha vilevile kwa wananchi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa mwaka wa 2025 nchi yetu imeagiza ngano kiasi cha shilingi milioni 377 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 980. Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kodi kwenye mashine na *increment* zote zinazotumika kwenye zao la ngano ili kuweza kuchochea wawekezaji hawa kuweza kulima kwa urahisi? Yaani kufuta kodi zote kwenye mashine ambazo zinatumika kwenye kilimo cha ngano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimshukuru kaka yangu, Mbunge wa Jimbo la Bahi kwa swali lake. Nimwammbie tu jambo moja, moja ya jitihada ya kwanza ya Serikali kwa sasa ni kuongeza tija kwa maana ya uzalishaji, halafu baada ya hapo ndiyo nafikiri hatua inayofuatia itakuwa ni hiyo kusaidia watu ambao wataleta viwanda ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tunaagiza ngano, tunaweza tukasema karibia 95% ya ngano yote inatoka nje kwa sababu uzalishaji ndani ni mdogo sana. Kwa hiyo, kuhusu kupunguzwa kwa kodi maana yake Wizara ya Fedha wanaweza wakalipokea hilo jambo na kuangalia namna bora ambayo itaweza akasaidia katika nyakati zijazo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, sasa aulize swali lake.

Na. 231

**Ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, lini barabara ya Mlowo – Kamsamba itaanza kujengwa kwa kuwa ni zaidi ya mwaka tangu mkandarasi asaini mkataba?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mlowo - Kamsamba yenye urefu wa kilomita130 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo Serikali tayari imekamilisha ujenzi wa Daraja la Momba na Daraja la Mpapa. Aidha, Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa tano kuanzia Mlowo kuelekea Kamsamba na kilometa nyingine tano kuanzia Kamsamba kuelekea Mlowo amepatikana, ambapo taratibu za malipo ya awali ya kumwezesha kuanza kazi, zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sehemu zilizobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Condester, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Nimeyasikia majibu ya Mheshimiwa Waziri Mzee wangu, kutoka kule Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2025 mwezi wa Tatu, Naibu Waziri kwa kuongozana na wataalam kutoka *TANROADS* alifika kwenye Jimbo la Momba na Jimbo la Mbozi na kusaini mkataba mbele ya wananchi wa Majimbo hayo mawili, na tukafanya sherehe kubwa sana kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hiyo kilomita tano kama ambavyo amesema Momba na Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tena kwenye majibu yake ya msingi Mheshimiwa Waziri, Mzee wangu anasema bado wapo kwenye hatua za kumtafutia mkandarasi fedha. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, aseme hapa ya matumaini, wananchi wa Momba, Mbozi na Songwe wanamsikia? Ni lini mkandarasi ataanza kutekeleza barabara hii kwa kiwango cha lami, kwa hizo kilomita tano tu ambazo alituahidi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge rudia swali, Waziri hajasikia.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hajasikia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge samahani. Waheshimiwa Wabunge, mkipiga makofi ya kutosha, Naibu Waziri hatasikia swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mbunge endelea.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, amesikia au nirudie?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umesikia?

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mzee, umesikia au nirudie?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naenda swali la pili. Barabara ya Kakozi - Ilonga ambayo inapita kwenye Vijiji vya Chisitu, Chipumpu, Kapele na Mchinga kuelekea Tunduma ambako wananchi wanajipatia mahitaji yao ya msingi, imeharibika sana na inachukua karibu masaa 12 ili waweze kupata huduma hizo, wakati ni kwa mwendo wa masaa manne. Vilevile, barabara ya kutoka Vwawa kupita Isalalu, Msangano mpaka Chitete na yenyewe imeharibika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni ipi kauli ya Mheshimiwa Waziri kumwelekeza *TANROADS* wa Mkoa aweze kufanya maboresho ili wananchi wasiendelee kulala njiani kwa barabara ya masaa manne tu kufika mjini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tulishasaini mkataba wa kujenga barabara ya Mlowo - Kamsamba kilomita kumi, kuanzia upande wa Mlowo na kuanza upande wa Kamsamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pia na wananchi wa Jimbo la Momba kwamba, kwa hatua tu hizo kupata Mkandarasi na kusaini ni kuonyesha kwamba Serikali imedhamiria kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami na ndiyo maana tumesema tumeshaanza kwa awamu. Pia, Mheshimiwa Mbunge akumbuke tuna madaraja ambayo yalikuwa na changamoto, na ambayo yalikuwa ni kikwazo kikubwa, tumeendelea kuyajenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema katika jibu la msingi, bado mkandarasi yupo, na Serikali inajipanga kupata fedha ili tuweze kuanza kujenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami kama ambavyo tulikuwa tumeahidi kwenye mkataba; na kama tulivyokubaliana na mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili ambalo ametaja barabara kama mbili au tatu, ninadhani hili ni suala tu la utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Songwe kwamba nina uhakika mvua zimeshaanza kupungua na wakandarasi ambao walikuwa wamepewa kazi ya kuhakikisha kwamba wanakwamua maeneo yote yaliyokwama, basi ahakikishe kwamba wanapelekwa katika barabara hizi na kurekebisha barabara hizo, ambapo tayari msimu wa mavuno umeanza, wasiweze kukwama; aweze kuwaelekeza hao wakandarasi wakakwamue maeneo yote yaliyokwama na wananchi waendelee kupata huduma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mbunge wa Hanan'g sasa aulize swali lake.

Na. 232

**Kuanzisha Kiwanda cha Kuchakata Mazao katika Jimbo la Hanang**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha kiwanda cha kuchakata mazao katika Jimbo la Hanang?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia

Abdulkarim Halamga, Mbunge wa Jimbo la Hanang kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Hanang huzalisha mazao mbalimbali ikiwemo mahindi, alizeti, ngano, dengu na mbaazi. Mwaka 2024/2025 wilaya hii ilizalisha mahindi tani 130,980.3, alizeti tani 30,732.3, mbaazi tani 19,173.6, dengu tani 30,960.2, na ngano tani 12,600. Wilaya hii ina jumla ya viwanda 1,226, ambapo kati ya hivyo viwanda vya kuchakata mahindi ni 346 na viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti ni 69. Viwanda 811 vinavyobaki ni vya matofali, mbao, kushona na mikate.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Kilimo pamoja na Mkoa wa Manyara tunaendelea kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kujenga viwanda vya mazao ya dengu, ngano na mbaazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa ni agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba kila wilaya kuanzishwe kongani ya viwanda ili kuweza kukuza thamani ya mazao ya wananchi na pia kupata masoko ya uhakika, na kwa kuwa, wananchi wa Jimbo la Hanan'g tayari Mheshimiwa Waziri katika jibu la msingi anaona namna gani ambavyo wamejikongoja wao wenyewe kuweza kuweka viwanda, je, Serikali haioni haja sasa ya kuanzishwa kwa kongani ya viwanda kwa Jimbo la Hanan'g?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa Wilaya ya Hanan'g, Kata ya Gendabi tunazalisha zaidi ya tani 100,000 ya chumvi, na jambo hili nimeshaliongelea hapa mara kadhaa, pia katika kata nyingine tunazalisha tani 30 mpaka tani 40, je, Serikali haioni haja sasa ya kuweza kutupatia vifaa vya

uchimbaji ili tuweze kuchimba kisasa na tuzalishe zaidi ya hizi tani nilizozitaja?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali haioni haja ya kutuongezea na kututafutia wawekezaji wa uhakika ili rasilimali hii muhimu iweze kutoa ajira kwa wanahanang, na pia kuliingizia Taifa mapato kwa maana ya fedha za ndani na fedha za kigeni?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mbunge wa Jimbo la Hanang kwa kuwatetea wananchi wake wa Jimbo la Hanang, hususan kuhusiana na suala la kuanzisha viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais alituelekeza, na hata alipokuja hapa kuzindua Bunge na katika zile ahadi zake za siku 100 mojawapo ya ahadi ambayo aliitoa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha tunaanzisha kongani za viwanda kila wilaya. Lengo ni kuhakikisha tunasogeza huduma za uzalishaji karibu na wananchi, hususan wakulima wakiwemo wakulima wa Hanang. Sisi kama Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara tumeshaanza huu mchakato kwa kushirikiana na wenzetu wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwishatoa maelekezo, na sasa hivi tunaandaa mwongozo wa Kitaifa wa usimamizi wa kongani za viwanda. Nina uhakika ifikapo mwaka huu tunapoanza utekelezaji wa Dira 2050 tutahakikisha sasa kila wilaya ikiwemo Wilaya ya Hanan'g inakuwa na kongani ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa yako, tayari Wilaya ya Hanan'g wameshatenga zaidi ya ekari 50 ambazo wametenga kwenye hii bajeti kwa ajili ya kuanzisha kongani za viwanda. Lengo ni kuhakikisha kwamba, tunaweka mazingira rafiki tunapovutia wawekezaji kwenye viwanda mbalimbali vya ngano,

dengu na kadhalika, wawe na maeneo ambayo wanaweza kuweka viwanda vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili. Ni kweli Hanang ni mojawapo ya maeneo ambayo kuna *deposit* za chumvi, kuna mashapo ya chumvi. Niseme kwamba tunahitaji kujiridhisha zaidi kabla hatujatangaza kama ni eneo *potential* kwa ajili ya uwekezaji, kwa sababu tunapotaka kuwavutia wawekezaji wakubwa lazima tufanye utafiti tujue *concentration* ya *ores* za *salt* kwenye yale mashapo ili tujue kwa kiasi gani tunaweza tukawaita wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi kwa kupitia Shirika la *SIDO* tumeendelea kuwasaidia wachimbaji wa Hanang. Mheshimiwa Mbunge ameomba tuendelee kuwasaidia, ninaomba nilipokee hili. Sisi kama Wizara ya Viwanda na Bishara tutahakikisha tunaendelea kuwasaidia wachimbaji wadogo wa chumvi kwa kupitia *SIDO* ili wakuze kipato chao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwetu na majibu kutoka upande wa Serikali. Ninaomba kuwaletea matangazo yaliyopo Mezani. Tangazo la wageni lililopo Bungeni: -

Kuna mgeni mmoja wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye ni Mhandisi Geremano Barnabas Ngusa kutoka Mkoani Tabora. Karibu sana. *(Makofi)*

Katika Jukwaa la Spika tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, ambao ni Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kutoka nchini Somalia nao ni kama ifuatavyo:-

Tunaye ndugu Xavier Daudi, Naibu Katibu Mkuu Utumishi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora ameambatana na wageni. Karibuni sana.

Tunaye Dkt. Ernest Mabonesho, Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania ameambatana na wageni pia. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye ndugu Abdirisak Ali Ibrahim, Naibu Katibu Mkuu wa Baraza la Mawaziri la Serikali ya Jamhuri ya Somalia na Kiongozi wa Msafara, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Mohamed Abdirahaman, ni Mkurugenzi wa Baraza la Mawaziri la Serikali ya Jamhuri ya Somalia. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo Wakurugenzi na Maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri la Serikali ya Jamhuri ya Somalia. Ahsante sana, karibuni sana Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana kwa makofi hayo.

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri Kilimo, Wakulima kutoka Mkoani Morogoro. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Tarimba Gulam Abbas, ni Ndugu Mwanne Othuman, Mtangazaji *East Africa TV* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Wafanyabiashara kutoka Jijini Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Yohana Stephen Msita, ni wapiga kura wake kutoka Manyoni Mkoani Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, ambao ni familia yake kutoka Chake Chake Pemba. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Sylivia Francis Sigula, ni Ndugu zake kutoka JIjini Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni 100 wa Mheshimiwa Muhsin Haji Ussi, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kutoka Mkoani Morogoro. Karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi sita kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 54 na walimu watano wa Shule ya Awali Bonjuu kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana hapa Bungeni walimu na wanafunzi. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 80 na walimu wawili kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanafunzi na walimu katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa siku ya Jumanne tarehe 5 Mei, 2026 Mheshimiwa Dkt. William Samoei Ruto Rais wa Jamhuri ya Kenya atalihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia saa 5.00 asubuhi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tukio hili muhimu na la kihistoria ambalo pia litafuatiliwa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa linalenga

kuimarisha ushirikiano na undugu kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Kenya.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnahimizwa kuhudhuria bila kukosa siku hii muhimu ili kumsikiliza mgeni huyo wa Kitaifa akilihutubia Bunge na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Sasa ninampisha Mwenyekiti wetu wa Bunge aendelee na ratiba inayofuata.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu, tuendelee.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela; Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo na Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, wajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uhai. Niwapongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa kutuletea hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia nizungumze kitu kidogo. Mimi ninasema kwa moyo wangu wa dhati kabisa, ninawapongeza sana wakulima wa Tanzania wote kwa ujumla wao. Hakuna Taifa ambalo linapaswa kujivuna kama Taifa linalojitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunajitosheleza kwa chakula kwa sababu wakulima wamesimama imara, na wanafanya kazi bila kuchoka. Ninamwomba Mheshimiwa Rais akisimama, anapoongea, ajivunie kwamba anaongoza Taifa ambalo linajitosheleza kwa chakula 128% na linalisha na nchi nyingine jirani ambazo hazina chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe, sasa nianze kuchangia hotuba hii ya kilimo kwa vipande viwili. Nitaanza kwa umuhimu wa sekta ya kilimo nchini. Kwanza, kilimo ndicho kinachotupatia chakula Watanzania. Kwa hiyo, umuhimu wa kilimo ni kwamba tunapata chakula cha uhakika. Kama sasa hivi nimetoka kusema kwamba kilimo kimetupatia chakula takribani 128% hadi asilimia 130.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kilimo, kidogo jamani tunachangia, watu msubiri kidogo, kilimo ndicho kinachosaidia sekta ya viwanda ikue kwa sabbau kinahakikisha kwamba kinatoa malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kilimo kinachangia takribani 30% ya pato la Taifa. Kilimo kinatoa ajira kwa 65.5%. Sekta ya kilimo inatoa 65% ya malighafi inayotumika kwenye viwanda. Kilimo ni uti wa mgongo, kwa sababu kinachangia takribani 56% ya fedha za kigeni katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaiomba Serikali, kwa sababu ya umuhimu wa kilimo, yote hayo niliyozungumza sasa ninaiomba Serikali ifanye jitihada ya kupima ardhi ili ijue mbolea ya kutumia isitumie mbolea tu ambayo Jimbo langu la Same Mashariki ni Jimbo la Kilimo lakini wakati mwingine niseme ukweli, kwamba, Serikali wanapeleka mbolea sehemu ambazo hiyo mbolea haihitajiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Serikali wawe wanapima ardhi ndipo wapeleke mbolea. Pia, Serikali ifanye jitihada sana ya kuwafikishia wakulima mbolea kwa wakati, hili ni tatizo. Serikali haifikishi mbolea kwa wananchi kwa wakati, na wakati mwingine wanapeleka ya kupandia, wananchi hawahitaji

ya kupandia. Pia Serikali wahakikishe wananchi wanapata mbegu nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upajikanaji wa pembejeo ni kitu muhimu sana. Sasa, ili wananchi waweze kulima vizuri na wapate asilimia kubwa watulishe Watanzania na nchi Jirani, lazima Serikali nao wajitahidi sana kuhakikisha kwamba vile vyote vinavyohitajika wanavipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kwenye suala la umwagiliaji. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Mimi jimbo langu linalima mazao makubwa mawili; linalima tangawizi, pia linalima mpunga na mahindi. Mazao yote niliyoyazungumza yanahitaji umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata fedha za umwagiliaji. Kwanza ninaishukuru Serikali, fedha za kwanza ambazo wameniletea nimepata mradi wa shilingi bilioni 1.7. Huu ni mradi wa Kata ya Myamba na sasa hivi upo kwenye matazamio. Mradi wa pili wa umwagiliaji ni mradi wa shilingi bilioni 6.9 ambazo zimekwenda Ndungu na Kihurio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa ninamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan, ninaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Sasa hivi tunamalizia Aprili, mwezi Januari Serikali imenipatia shilingi 44,159,672,317.40. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri sana, ninamshukuru mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimeletwa jimboni kwangu kujenga bwawa la umwagiliaji, kwa sababu sasa wanaolima tangawizi ni Tarafa ya Mamba Vunta na Tarafa ya Ndungu, wao ndio walioko milimani na ndiyo chanzo kikubwa cha mito. Wao kwa sababu wanalima tangawizi sana, yale maji ya kule juu yote wameyachukua. Wananchi wanaolima mpunga tarafa ya chini wanakuwa hawana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikaona, ikaja ikanipa shilingi bilioni 44, inanijengea sasa bwawa kubwa sana. Bwawa hili

linajengwa kwenye Kata ya Lugulu Kijiji cha Vumba. Bwawa hili litahudumia takribani wakulima 21,523. Bwawa linatarajiwa kuanza kuhifadhi takribani lita bilioni 5.84, na bwawa hili litahudumia Kata ya Ndungu na Maore. Mkandarasi ameanza ujenzi tarehe 11/2/2026. Niliondoka kama siku nane hivi kwenda kumwona mkandarasi. Bwawa hili linatarajiwa liwe limekamilika tarehe 10/2/2029. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Same Mashariki, nasimama hapa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wakulima wanahitaji umwagiliaji sana, na 100% ya wananchi wa Same Mashariki ni wakulima. Ni kweli tunapata mvua, lakini mvua haitoshelezi, tunahitaji sana umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa fedha hizi na bwawa hili ambalo linakwenda kujengwa sasa, ni lazima wananchi wale wamechanganyikiwa niseme ukweli. Ndiyo Waheshimiwa Wabunge niwaambie, watu hamjui ni kiasi gani Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anapendwa na wananchi. Wananchi wanampenda Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan sana kwa sababu anajali wakulima mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kusema zaidi, niseme Mheshimiwa Waziri wa Kilimo apokee shukurani kutoka kwa wananchi wangu, japo Mheshimiwa Waziri hanitazami, lakini naomba anitazame kujua kweli kwa unyeyekevu mkubwa, namshukuru sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais, ninamshukuru Naibu Waziri wake, ambaye ninamwomba baada ya kumaliza bajeti hii, tusafiri naye twende akamwone mkandarasi yule, akauone na Mto wa Saseni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi sina cha kulalamika, ninaishukuru sana Serikali, upande wa kilimo jimboni kwangu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia muda wa kuchangia. Waheshimiwa Wabunge, safari yetu ya mwaka 2050, gari au injini kubwa itakayotufikisha huko ni kilimo, lakini kufika huko lazima uchumi ukuwe kwa kiasi cha 10% kufikia ile dola trilioni moja, na ile fedha ya mtu mmoja mmoja dola 7,000, ni kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kama mnakumbuka mwezi Februari nilitoa mchango wangu hapa nikasema, kufanikiwa *vision* 2050, kilimo kichangie 35% ya *GDP,* halafu uchumi wa gesi uchangie 25%, halafu uchumi wa madini 20% na utalii 15%. Sasa nitatoa mapendekezo, lakini kwanza nianze kwa kusema kwamba, kwa niaba ya wananchi wa Musoma Vijijini naiunga mkono hii bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Wizara inafanya vizuri na viongozi wa Wizara wanafanya vizuri, na isitoshe tarehe tisa mwezi wa Tano, 2026 tunaenda kumkabidhi mkandarasi mradi mkubwa ambao ulianzishwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1974. Tumekaa miaka 52 mradi umesimama. Shukrani za kipekee sana apelekewe Mheshimiwa Rais, kwa sababu amefufua kitu ambacho kilikuwa kimesimama toka mwaka 1974 mpaka leo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, mafanikio ya kilimo ni lazima tuwe tunayatathmini kama kweli tunaenda vizuri, na tathmini ya kwanza kabisa ni mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei, mchango mkubwa ni bei ya chakula sokoni. Mataifa yenye uchumi mkubwa, mfumuko wa bei ukifikia asilimia mbili wanalalamika sana. Uchumi mdogo unaoendelea kama wa Tanzania haupaswi kupata mfumuko wa bei zaidi ya 5% kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunafanya vizuri, tuko chini ya 3.5%, kwa hiyo, pongezi kubwa sana Wizara ya Kilimo, kwa sababu mmeweza kudhibiti mfumuko wa bei kwa kuhakikisha chakula kipo kingi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo kingine cha mafanikio ya kilimo chetu ni *food security*. Tuna akiba ya chakula. *NFRA* inafanya vizuri, kwa hiyo inamaanisha Wizara inafanya vizuri na Serikali inafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini nyingine ni sera tulizojiwekea, zipo za hapa nchini. Ninachukua hizi kubwa kubwa kidogo; kwanza ya *AU*, Julai, 2003, palikuwa na *Maputo Declaration*, Marais wetu walionana Maputo, wakakubaliana kwamba nchi za Kiafrika, kwa kila mwaka angalau tutumie siyo chini ya 10% ya bajeti ya Taifa iende kwenye kilimo. Sasa bajeti aliyosoma Mheshimiwa Waziri ni shilingi trilioni 1.1 na ya mwaka 2025 ilikuwa ni trilioni 1.2. Sasa na ninyi Wabunge nawaachia zoezi la kufanya hesabu rahisi, chukua bajeti hii tuliyosomewa na bajeti ya 2025. Je, tumefika 10% kila mtu atapata jibu lake hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya pili, vilevile ya *AU* 2014, *Malabo Declaration*, *Equatorial Guinea*. Marais walikaa wakasema tuongeze kasi kwenye ukuaji wa kilimo. Huwezi ukakua kati ya asilimia sita mpaka 10% kwa kila Taifa, halafu tuwekeze uwekezaji mkubwa. Hii *Public Private Partnership* haikuanza leo. Hata Marais wetu walisema tuwekeze kwenye kilimo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kigezo kingine ambacho ni muhimu cha *UN*, *SDG's (Sustainable Development Goals)*. *Goal* namba mbili, inasema *zero hunger by the year 2030*. Yaani dunia nzima ikifika mwaka 2030 pasiwe na njaa, lakini tathmini imefanyika, dunia haijafanikiwa, kwa sababu mwaka 2025 karibu 23% ya wakazi wa duniani hapa walikuwa na misukosuko mikubwa sana ya upatikanaji wa chakula, ambayo imeongezeka kutoka 13% mwaka 2013. Kingine ni kwamba mwaka 2025, vijana, watoto milioni 35.5 walikuwa na utapiamlo. Kwa hiyo, hatujafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ninayaweka, unilindie muda wangu, kwa sababu nakuja kutoa mapendekezo kwa nini ninaweka nguvu tuweke nguvu kwenye kilimo cha mazao ya chakula, ndiko ninakoelekea huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, binadamu, yaani tuna Mataifa yote duniani, ni Taifa moja tu ambalo haliagizi chakula, linajitegemea. Binadamu anahitaji virutubisho saba *(seven nutrients)*. Nchi pekee ambayo haiagizi, (hii ni ripoti imetoka mwaka huu) ni nchi ya Guyana, iko *Latin America*, kaskazini mwa Brazil. Guyana ndiko ilikuwa kwao Prof. Walter Rodney kwa wale waliosoma kitabu chake. Hiyo tu, ndiyo haiagizi chakula. Kwa hiyo, inamaanisha hata Mataifa makubwa yote yanahitaji kuagiza chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu sasa, uchumi kufikia tulioupanga 2050 na sekta ya kilimo kuchangia 35%, cha kwanza, tuongeze utafiti mkubwa sana kwenye mbegu, *seed research* na utafiti mkubwa kwa kilimo kwa ujumla. Kama ambavyo huwa nawatolea mfano wa India na China, kwa mwaka China wanatumia dola bilioni 10 kufanya utafiti. India wanatumia shilingi bilioni sita kufanya utafiti. Kwa hiyo, sisi kufanikiwa Sekta ya Kilimo lazima tuongeze utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, kilimo cha umwagiliaji. Tunaenda vizuri, lakini lazima tupanue umwagiliaji mkubwa na mdogo. Mkubwa ni kama huo unaoenda kufanyika Musoma Vijijini, lakini hapo sikia, umwagiliaji mkubwa; lile Bwawa langu la Bugwema, umwagiliaji wa Bugwema tunaoenda kumkabidhi mkandarasi tarehe tisa mwezi ujao, gharama yake ni shilingi bilioni 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na *schemes* kama hizo 10 karibu ni shilingi bilioni 500. Ninawaeleza, bajeti tu tunayoisoma hapa haiwezi kufanya mapinduzi makubwa ya kilimo cha umwagiliaji, haiwezi. Kwa hiyo, badala yake ni kama Wabunge wengine nimewasikia jana wanaongea. Ni lazima tutafute fedha za pembeni. Mataifa yote, hata waliofanya kazi kwenye mashirika makubwa wanajua. Kuna kitu kinaitwa *extra budgetary funds*, haziji kusomwa humu, lakini zinatafutwa kwa kazi mahususi na huko ndiko tuelekeze kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni kwamba, ukilima ngano kwa kutegemea mvua ya kawaida unavuta tani moja kwa ekari

moja, lakini ikiwa ya kumwagilia ni kati ya tani tatu mpaka tano kwa ekari moja. Nchi inayofanya vizuri sana kwa ngano Afrika sasa hivi ni Ethiopia, kwa sababu ya umwagiliaji mkubwa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la tatu, Tanzania lazima tuwe na viwanda vya zana za kilimo. Kilimo cha jembe la mkono hakiwezi kutekeleza *vision* 2050, hata cha mkokoteni. Kwa hiyo, zana za kilimo ni kwamba, nina mfano mzuri, sisi tuko chini sana, lazima tuongeze. Ukichukua trekta nchini Tanzania kwenye kila hekta 1,000, Tanzania tuna trekta 3.6, lakini India kwenye hekta 1,000 wana trekta 20, China hekta 1,000 wana trekta 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha nne tuwekeze kwenye viwanda vya mbolea. Kwa ile *urea*, kiwanda tunachotaka kukijenga kutokana na gesi yetu, hesabu zimeshapigwa, yaani *TCF* moja *(One Trilion Cubic Feet) of natural gas* inaweza ikazalisha tani milioni 28 za *urea*. Kwa hiyo, tuna gesi ya kutosha, hatuna sababu kwa nini tusiwe na viwanda vya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwamba Watanzania tunatumia mbolea kwa kiasi cha chini sana. Tunatumia wastani wa kilo 20 kwa hekta moja, lakini wataalamu wa kilimo na *FAO* inasema angalau tutumie kilo 50 kwa eka moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho natoa maoteo ya biashara duniani, kwa nini twende kwenye mazao? Hili ndiyo la mwisho sasa wa maoteo. Soko la Dunia, kwa hiyo hakuna kusema kwamba hatuna masoko, dunia nzima ni soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2030 tutakuwa watu bilioni 8.5 duniani. Mahitaji ya chakula yanapaswa kuongezeka kwa *percent* kati ya 30 na 40 ya uzalishaji wa sasa. Mwaka 2050 tutakuwa watu duniani bilioni 9.7, mahitaji ya chakula yataongezeka kwa kati ya 50% na 70% ya uzalishaji wa sasa. Kwa hiyo, dunia inahitaji chakula, na Tanzania tuwekeze kwenye chakula, na thamani ya masoko nayo itaongezeka ndiyo pointi ya mwisho hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tulime mpunga mwingi? Mwaka 2033 thamani ya soko la mchele au mpunga duniani litakuwa la shilingi bilioni 392 na watu duniani 50% ya wakazi wa dunia hii wanatumia mchele, mpunga, utakavyouita kama chakula kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2033 soko la ngano duniani litakuwa la shilingi bilioni 270 na watu 40% ya wakazi wa dunia hii wanatumia ngano kama chakula kikuu. Hata kahawa, mikoa inayolima kahawa, soko la dunia mwaka 2034, kahawa itakuwa na thamani ya shilingi bilioni 380. Wale wa maua ifikapo mwaka 2030 Soko la Dunia litakuwa na thamani ya shilingi bilioni 52.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ninadhani nimeweza kuwashawishi kwa nini tujikite sana kwenye kilimo cha chakula kwa ajili yetu na kwa ajili ya dunia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, na Mheshimiwa Charles Mhando Njama ajiandae.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii. Ni neema ya Mwenyezi Mungu amenijalia kuwa sehemu ya Bunge hili, tangu Bunge la Kumi na Moja na Bunge la Kumi na Mbili, lakini kwa mara ya kwanza tangu Mwenyezi Mungu anipe fursa ya kutambulika humu Bungeni na cheti na siyo orodha ya majina, ndiyo nimesimama hapa kuweza kutoa mchango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini kukishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi, chini ya Jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kipekee ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Kondoa Mjini, haikuwa rahisi, lakini yametimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawatoa hofu, watu wafupi hatuna maneno mengi, lakini huwa tunaonekana kwa vitendo.

Wawe na moyo wa subira, Ilani imeeleza vizuri, katika maendeleo, tunamwona Mheshimiwa Rais na Baraza alililoliteua wanaofanya kazi, basi mimi kiraka wao waje wanipime 2030 kwa maendeleo yatakayoonekana ndani ya Jimbo la Kondoa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii, kama nilivyosema hiki ni kipindi cha tatu, na kila mtu anajua mimi ni mkulima kweli kweli. Ninaweza nisichangie hoja yoyote ndani ya mjadala wowote ama Mkutano wa Bunge, lakini sitaacha kuchangia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua, yako mambo huko nyuma tulikuwa tunashauri, lakini hayafanyiwi kazi mpaka yakatugusa. Kipekee ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kweli mwanamama huyu tangu ameingia madarakani amekuwa *pioneer* wa namna ya kuwekeza fedha na vitendo kwenye Sekta ya Kilimo. Makofi mengi kwake Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niongee. Kuna wenzangu waliopata kuchangia jana walisema hatuna kipimo. Mimi ninaomba niwaambie, wakati anaingia madarakani Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, bajeti alikuta ilikuwa shilingi bilioni 294, lakini bajeti iliyomalizika kutekelezeka 2025/2026 ilikuwa shilingi trilioni 1.19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape hesabu rahisi kabisa, ingekuwa basi katika bajeti hizi mbili, tumepokea asilimia moja ya matoleo, kule 294 tungekuwa tumepokea shilingi bilioni 2.94. Kwenye hii shilingi trilioni 1.19 tungekuwa tumepokea matoleo ya asilimia moja tu, basi ingekuwa shilingi bilioni 11.9. Kwa hiyo, mwenye macho haambiwi tazama. Leo ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuwa na jicho la maono la viongozi wa kufanya nao kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina-*declare interest*, mimi ni Makamu Mwenyekiti, na nimefanya kazi na Mawaziri wawili. Nimpongeze sana aliyempa kijiti Mheshimiwa Chongolo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe. Yeye wakati anapewa

jukumu hili akisaidiwa na Mheshimiwa Mavunde waliweka *document* ya kuweza kupeleka kilimo kuchangia 10% itakapofika 2030. Pia ninampongeza zaidi Mheshimiwa Chongolo, huyu ni kiongozi na ni kiongozi mahiri kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wengi hawana *continuity* wakiingia kwenye Wizara, wanaanzisha mambo mapya. Alikuja kwenye Kamati kutueleza mipango yake, anaanza pale wenzake walipoishia. Uzuri anayo majembe; Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde msikivu, anafuata yale maelekezo anapopewa, nawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa watendaji, yupo kiongozi wao Katibu Mkuu Dkt. Mweli. Haki ya Mungu huyu jamaa hana maneno mengi kama watu wafupi. Yeye ni vitendo na utendaji. Kwa hiyo, nina uhakika Wakurugenzi wote wa taasisi ambazo ziko chini ya Wizara ya Kilimo kazi, wanaifanya na tunaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kipimo ni kipi? Kwenye bajeti kuna kutengewa bajeti, kuna fedha, lakini sisi kama Bunge, kazi yetu pia ni kusimamia zile fedha zinazoenda kuhakikisha zinafanyiwa kazi? Niwapongeze Wizara ya Kilimo, fedha ni ndogo lakini kazi ni kubwa. Leo hii unasema huna kipimo cha kuipima Wizara ya Kilimo, lakini Mtanzania maskini wa kawaida kule kwangu Kingale anapokea mbegu ya alizeti ya ruzuku, leo anapokea mbolea ya ruzuku kutoka kwa Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kipindi hiki cha miaka mitano ya utekelezaji wa bajeti na ongezeko hili pamoja na fedha zinazotoka, mazao ya chakula yamepanda kutoka shilingi 17,000,000 tani, ni mpaka milioni 23,000,000 ongezeko la zaidi ya 38%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mama yangu Mheshimiwa Kilango ametoka kuliongelea utoshelevu wa chakula, tulikuwa tuna utoshelevu 126% leo tuna utoshelevu wa 130%. Utasema huna? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumefika Tanzania Afrika Mashariki ndiyo nchi ya kwanza kumiliki ndege yetu ambayo inaenda kuua kwelea kwelea. Utasema huna cha kuwapima? Leo Mheshimiwa Rais watangulizi wake wawili waliacha eneo la umwagiliaji la ekari 600, yeye leo kwa bajeti hii ambayo bado tunamwombea Raymond apande fungu maalum hela ziendelee kwenda kwenye miradi ya umwagiliaji, amefikisha ekari 983,466 ndani ya miaka yake tu hii mitano ya utekelezaji wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti unafanyika. Leo tunaona *TARI* ilikuwa imekufa; leo tuna *center of excellence* kwenye utafiti ndani ya nchi yetu, utasema huna cha cha kuwapima Wizara ya Kilimo? Mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayaona, tutaendelea kuyaona. Rai yangu kwa Wizara ya Fedha, kweli ni sisi wanasiasa ndio tunatoa presha, tunataka vituo vya afya, hebu sasa hivi tupeleke kwenye sekta ya uzalishaji kilimo, itatuletea fedha za kujenga hospitali, na kujenga shule. Kwa hiyo, ninaiomba sana Wizara ya Fedha, kilimo kimeonyesha uaminifu na uadilifu, tuwapelekee fedha ili waweze kutuzalishia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la usimamizi, ninaunga mkono, na hii ilikuwa ni maoni kutoka kwa Kamati. Mheshimiwa Rais alitoa vifaa vya ugani, alitoa pikipiki na vipima udongo. Ufanisi wake ukawa mdogo kwa sababu vifaa vile vinasimamiwa chini ya Mkurugenzi. Mkurugenzi pikipiki ile anataka ipeleke mitihani, isiende kwa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono kwenye kwenda kuanzisha *National Agricultural Extension Services Agency* ili kule mashambani kwetu wakulima wafikiwe na wagani. Hili ni jambo muhimu katika usimamizi na ufanisi ili wakulima wetu waweze kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona leo watu wanasema *BBT* hamna chochote, vijana waliomaliza *SUA* leo wako, Mheshimiwa

Njalu shahidi, mimi nimeenda kwa watani zangu Wasukuma kule Simiyu wanasifia wanawaita ma-*BBT,* wasomi wale kweli wamekwenda kuweka mchango katika kuongeza tija kwenye zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninaomba nimshauri mambo mawili Mheshimiwa Waziri. Kwanza, ninamwomba, inawezekana wataalamu wake wa Wizarani wanafanya mambo mazuri, sisi tunahangaika hiyo sehemu ya *BBT* kuna vijana ambao wamesomea *marketing* na wengine wamesomea mambo ya kompyuta, watafutiwe ofisi wapewe vifaa, kazi yao ni kutafuta masoko nje ya nchi na walipwe kutokana na kamisheni kwa masoko watakayoyaleta. Mtakuja kunishukuru baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana watu wanapenda kupeleka besenga, nini, vijana wapo. Ninaomba niwasemee, wape vyumba wape kompyuta, wape vifaa na hutawalipa mshahara, utawalipa kwa *performance* kwa namna wanavyokuletea. Sasa hii ni bajeti. Bajeti ni mapato na matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya mwisho, ninaomba nishauri na ninajua wako watakaofurahia kimoyomoyo, wako watakaonibeza, lakini ni maoni. Liko zao ambalo mimi nataka nishauri kuliko kubanana banana, hebu tuangalie chanzo hiki kipya cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona na ninampongeza sana kaka yangu Aretas James Lyimo, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kupambana na madawa kulevya, lakini niliona kuna boti Bagamoyo imebeba jani linaitwa shajaratul fikra. Kuna wenzangu Mombasa kule wanaitwa *shajarat al-fikra*, wengine wanaita *khat* wengine wanaita miraa, wengine wanaita mirungi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaenda kufanya tafiti kama yale amekamata gizani, yaliyokamatwa ni mangapi? Ina maana tunamfaidisha jirani bila sisi kujua, ana soko kubwa, na anapata hela kupitia sisi. Nikaenda kujifunza zao hili la kati, na leo ninashukuru wageni wa Kisomali walikuwepo ndiyo soko kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Somalia inakusanya mapato zaidi ya milioni nane kwa mwaka kutokana na biashara ya mirungi. Kenya inaingiza dola milioni 300 tena kwa zile nchi ambazo ziko wazi; Tanzania hatuhesabiki kwa sababu sisi tunaletewa gizani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, dunia nzima mzunguko wa zaidi ya dola bilioni tatu kwenye zao hili la mirungi na huko nyuma nimeulizia ulizia Tanzania ilikuwa inaruhusiwa, sasa mimi sina ushahidi na kinga ya Bunge inilinde. Ninasikia kuna kiongozi fulani alikuwa na rafiki anatumia, sasa lile starehe nilivyofuatilia la wastaarabu hawapendi bughudha hawezi kusikia mtu amekula mirungi kapigana…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Malizia muda wako umeisha.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vya msingi vinaongea vya kushauri…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile biashara huwezi kusikia mtu kamrushia chupa anayekula mirungi kwa ustaarabu. Sasa yule rafiki yake akawa anamchelewesha muda wa kuonana naye, kwa hiyo, tunaomba *Hansard* zituonyeshe. Siyo dhambi, tujue lile Bunge lililotunga sheria, walitumia vigezo vipi? Leo ukiangalia madhara, inasema mirungi inasababisha kansa. Twendeni *Ocean Road*…

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa muhimu sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariamu muda wako umemalizika.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya sigara ambayo inatokana na zao la tumbaku, na mirungi wapi wagonjwa wengi wanaosababishiwa kansa? Twendeni tukajifunze. Wanasema mirungi inasababisha *social dependence*. Tuulize, zile pombe kali zinazozalishwa huko Babati Sungura na kadhalika, zipi ambazo zinaharibu vijana wetu? Ni mirungi ama hizo pombe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam umeeleweka, lakini hilo liko nje ya uwezo wa Mheshimiwa Waziri, inabidi irudi kwenye sheria. Kwa hiyo, umeeleweka.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie. Sheria zinaletwa kwa Miswada, nadhani Serikali, nami sio Mwanasheria, ndio maana tunashauri na yeye anao watafiti, ninadhani ana vyombo vingi ambavyo wanaweza kwenda kufuatilia. Kwa hiyo, twende tukajiridhishe kwamba kweli madhara ama hizo *element* za ulevi ndani ya mirungi na kwa vitu vingi leo wanasema mirungi inaleta madhara kiafya…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam muda umepita sana.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaulize, *energy drink* na mirungi ipi ambayo inaleta madhara zaidi kiafya. Muda umefika tutafakari, kwa sababu zao hili linaleta mapato mengi na pia nimefuatilia Kenya inapeleka Djibouti, Kenya inapeleka mirungi Somalia, mpaka Israeli Yerusalamu...

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam, hiyo ni kazi ya Serikali, umeeleweka.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** …mirungi inapelekwa kama zao la biashara katika nchi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninapenda kumalizia kwa kumpa sifa sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa, lakini *Comrade* Chongolo. Ama hakika Mheshimiwa Rais hajakosea kumleta Wizara ya Kilimo kwanza ni muumini wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka hata uanzishwaji wa Benki ya Ushirika, moja ya mafanikio makubwa ndani ya Wizara ya Kilimo yeye ndio mwanahisa wa kwanza kununua hisa kati ya benki hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam unawanyima fursa wengine.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** …alikuwa Katibu Mkuu ambapo anaenda kufanya ziara ya kichama, lakini anakagua miradi ya kilimo. Kwa hiyo, mzigo amepewa mtu sahihi. Kama Kamati…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam, unawanyima fursa wengine muda umepita sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau na Mheshimiwa Azza Hillal Hamad ajiandae.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nami nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, na Naibu wake; Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo pamoja na Wakurugenzi wake wote kwa namna ambavyo wameleta wasilisho zuri katika bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia kwa kazi nzuri ambayo inaonekana kwa miradi mbalimbali ambayo wanaendelea kuitekeleza katika Wizara ya Kilimo. Wizara ya Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Kwa kuzingatia hilo, tunaona fursa kubwa ambayo ipo kupitia kilimo katika nchi yetu hasa kutengeneza ajira nyingi zaidi wa vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kufikia uongezaji wa ajira kwa vijana wetu wa Tanzania nafikiri tunapaswa tufanye mambo mawili makubwa. Jambo la kwanza ni vizuri tukawekeza zaidi katika utafiti kama vile ambavyo wenzetu upande wa madini wanafanya utafiti ili kuondoa *uncertainties* zilizopo katika wachimbaji, vivyo hivyo tunatakiwa tufanye utafiti wa kutosha katika mbegu, katika ardhi na aina ya mazao ambayo yanaweza kuwa katika maeneo tofauti tofauti ili kuondoa *uncertainties* kwa vijana wanaotamani kwenda kuingia katika kilimo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo pia ni vizuri kuliwekeza kwa nguvu kubwa ni upande wa masoko wa mazao ambayo tunaenda kuzalisha tukiweka nguvu katika maeneo haya mawili, tutakuwa tumewashawishi wakulima na hasa vijana kuingia zaidi katika kilimo kwa kuwa watakuwa na uhakika mtaji wanaoupeleka katika eneo fulani la kilimo wana uhakika wa kuvuna na wana uhakika pia baada ya kuvuna wanalo eneo la kwenda kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa masoko, Waheshimiwa waliochangia jana, baadhi nimesikia wakiongelea vizuri kazi nzuri iliyofanywa na *COPRA*. Ninafikiri ni wakati mwafaka sasa Mheshimiwa Waziri ukaona namna gani unaenda kuwekeza zaidi katika taasisi hii ili iweze kutafuta masoko zaidi na kuwahakikishia wakulima masoko ya bidhaa ambazo wanakwenda kuzizalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tunatakiwa tuliwekee nguvu na ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameshaifanya na Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji ambao wamefanya kazi kubwa mpaka sasa, lakini bado tunayo kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha kwamba tunaendeleza miradi ya umwagiliaji katika maeneo mengi ya nchi, kwa kuwa hili nalo ni eneo ambalo litakwenda kuleta uhakika kwa wakulima badala ya kuendelea kutegemea mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo letu la Korogwe Mjini tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tuna miradi

miwili mikubwa ya umwagiliaji. Tunao mradi wa umwagiliaji katika Kata yetu ya Kwamdolwa, tunao pia mradi mkubwa wa umwagiliaji katika Kata yetu ya Kwamsisi. Miradi hii miwili kwa ujumla wake inagharimu takribani shilingi bilioni 29.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, katika bajeti yake na hasa atakapokuja kufanya *finalization,* angalau atupe tumaini kwa sababu miradi hii imekuwa ikisuasua kwa muda mrefu sana. Tunahitaji twende tukaone utekelezaji wa miradi hii inatekelezwa kwa kuwa inaenda kuleta chakula kwa wananchi, lakini pia inaenda kutengeneza ajira nyingi kwa watu wa Korogwe Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwa upande hasa wa jimbo langu, sisi ni miongoni mwa wazalishaji wa zao la mkonge na wananchi katika Jimbo la Korogwe Mjini wameonyesha utayari wao kwa kuwa wengi wamejikita katika kilimo cha mkonge, lakini tunayo changamoto ya upungufu wa mashine za kuchakata mkonge, mashine za *corona*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, alivyopita katika wakati wa kampeni katika Jimbo la Korogwe Mjini na Korogwe kwa ujumla aliahidi kutuletea mashine hizi za uchakataji wa mkonge katika Jimbo la Korogwe Mjini na Korogwe Vijijini pia. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri aone namna gani tunakwenda kupata sasa hizi mashine za *corona* katika eneo letu ili katani inayozalishwa isiende kuharibika kwa kukosa mashine za uchakataji wa mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninafikiri tuna fursa katika eneo hilo. Tunazalisha mkonge kwa wingi, lakini tunasafirisha mkonge nje. Hata hivyo, tunayo fursa ya kuanzisha viwanda vya kutengeneza *final products* za mkonge ambazo pia zitakwenda kutusaidia kukabiliana na *products* ambazo zinaharibu mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna wenzetu wanazalisha korosho, wanazalisha kahawa ambayo sisi tukiwekeza katika uzalishaji wa gunia tunaenda kuleta vifungashio ambavyo vitakuwa ni rafiki

kwa mazingira, lakini pia tunaongeza ajira kwa maeneo ambayo tunazalisha mkonge hasa Korogwe na eneo lote la Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Korogwe Mjini tuna vikundi vingi ambavyo vimejikita katika uzalishaji wa mboga mboga, lakini changamoto tunayokutana nayo ni kwamba wakati mwingine akina mama wale na vijana wanapopeleka mbogamboga sokoni, zinakosa wateja kwa wakati huo. Ombi lao kubwa la namna ya kuboresha biashara yao na kilimo chao cha mbogamboga ni kupata *cold room* ambayo angalau hata kama watakwenda sokoni na watakosa wateja, basi mboga zile zisirudi kuharibika na badala yake ziwe zimetunzwa na kuwe na uhakika wa kuuzwa wakati mwingine unaofuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamsihi sana Mheshimiwa Waziri aangalie katika bajeti yake namna gani tunaweza tukapata *cold room* kwa ajili ya *storage* ya mbogamboga na matunda yanayozalishwa katika Jimbo letu la Korogwe mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupatiwa kiwanda cha kuchakata haya mazao ambayo ni *perishable* kama namna ya mojawapo ya kwenda kufanya *storage* na hasa nyanya ambazo zinazalishwa na wakulima hawa wadogo wadogo katika eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie katika zao la machungwa. Sisi Tanga tunaamini hakuna eneo linalozalisha machungwa bora zaidi ya Mkoa wa Tanga. Sasa tunaomba kupatiwa kiwanda cha kutengeneza juisi za matunda. Korogwe ilikuwa na Kiwanda cha *Tang Gold* ambacho baadaye kilipewa mtu binafsi ambaye ameshindwa kukiendesha. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais alivyopita katika Jimbo la Korogwe Mjini wakati wa kampeni alisema kiwanda kile kitarudishwa kwa wananchi na kiendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tuone namna gani sasa tunaweza tukaanza ku-*process* matunda yetu ndani ya eneo la

Korogwe badala ya kusafirisha machungwa kwenda nchi jirani halafu baadaye tuletewe tununue kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Mahando Njama, ahsante sana. Mheshimiwa Mheshimiwa Edward Olelekaita Kisau atafuatiwa na Mheshimiwa Azza Hillal Hamad na Mheshimiwa Chiku Athman Issa ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Kilimo kwa kazi kubwa ambayo wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kuwapongeza wakulima wote nchi nzima. Wakulima wanafanya kazi kubwa, ukisikia Taifa lina chakula cha kutosheleza, kazi hii inafanywa na wakulima wa Tanzania nzima hii. Kwa hiyo, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni maisha, ni zaidi ya biashara, ni zaidi ya uti wa mgongo, ni zaidi ya mgongo wenyewe, ni maisha. Sifa ya kilimo, sifa nyingi sana zimeshatajwa kwamba Watanzania 65% mpaka 75% wanategemea kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninadhani hata hizi *data,* unajua kutokutegemea kilimo maana yake kuna mtu hali kabisa. Kwa hiyo, ni *more than 75%.* Kama hulimi, si unauza; kama huuzi, si unakula; sasa si unategemea kilimo. Kwa hiyo, kwa kweli tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wengine, bajeti ya kilimo kuongezeka mara tatu, mara nne kwa kipindi cha miaka mitano ni kazi kubwa sana. Kazi nyingine kubwa aliyofanya ni kumchagua Katibu Mkuu Mstaafu wa Chama cha Mapinduzi, rafiki yangu Mheshimiwa Chongolo. Yeye ni zaidi ya Waziri. Sio

Waziri tu, ni Waziri halafu ni Katibu Mkuu Mstaafu wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nini? Yeye anajua nchi hii yote, ameizunguka. Anajua kila mahali, kila kona ya nchi hii. Kwa sababu Chama cha Mapinduzi kinatunza misingi, sisi kazi yetu ni kuisimamia misingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kwa kweli wakulima kama unavyosikia kwa Wabunge hawa, kila Mbunge amependa kuchangia kilimo kwa sababu kinawagusa Watanzania wote na misingi ya kilimo ni kuzungumza na wananchi wenyewe na kusikiliiza Watanzania wanasema nini kuhusu kilimo. Huo ni msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi mwingine ni Serikali kuendelea kuwekeza na kuweka mazingira mazuri kwa wakulima nchi hii. Tuwe na sheria nzuri, tuwe na masoko mazuri, tuwe na mbegu bora, nzuri na mbolea na zifike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa ukurasa wa 148 ninanukuu sehemu ndogo tu: "Nawasihi wakulima wa nchi hii kuwa macho na kuhakikisha wananunua mbegu bora kutoka kwa mawakala waliosajiliwa na kukagua kwa makini nembo za udhibiti ubora na kwenye vifungashio na siyo vinginevyo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mkulima leo wa kule Emarti kule Kiteto ama Makame ama Longido huko, yuko kijijini kabisa kule atajuaje kwamba kuna nembo, kuna kifungashio? Unajua Wizara ya Kilimo lazima tuongee lugha ambayo Watanzania wa kawaida wanafahamu. Kuna Watanzania wengine wanakutana na hizi mbegu, imenunuliwa na mtu mwingine, kaileta kijijini. Kwanza atajuaje kwamba huyu kasajaliwa; na nani? Ataona wapi? Kwa hiyo, ninadhani Wizara ya Kilimo iongee lugha ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara ifanyeni hiyo kazi ya kupambana na wale wanaoleta mbegu. Tusilete jukumu hili kwa wakulima, ni kazi ya Serikali. Tutasaidiana ndiyo, lakini

isifanywe kwamba sisi ndio tukague, halafu tukishindwa tuseme sijui nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwaambia wakulima wangu, kesho ninachangia, yaani leo sasa; nikawaomba mawazo yao. Kwa kuwa Wizara ya Kilimo ni kuangalia misingi, wasikilize wakulima wa Kiteto wanasema nini, tunaomba magari yale ya Mama Samia Suluhu tukachimbe maji mashambani. Maeneo tunayo, tupate kilimo cha uhakika, ndicho wanachosema wakulima. Mwingine anamwambia mwenzake, anasema Waziri yuko sahihi sana, kilimo cha mara moja kwa mwaka cha kutegemea mvua ni mtihani. Ndicho wanachosema wakulima wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwingine anasema tupatiwe mbegu bora, lakini changamoto kubwa ni bei. Tunomba Serikali iendelee kupambana, iendelee kufikiria mbegu hizi ni ghali, ishuke ili wakulima wapate motisha ya kwenda mashambani. Vilevile, wanaomba na wanasema masoko yawepo na waunganishwe na masoko ya nje. Huyu ni mkulima mdogo sana wa Kiteto. Ndicho wanachosema. Kwa hiyo, tunataka Serikali iweke mazingira mazuri kwa ajili ya wakulima hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaangalia mazao ya chakula tunayaagiza kutoka nje ngano na maziwa. Nimekutana na maziwa sasa nikawa ninawaza, sasa hata maziwa yako kwako huku, sasa rafiki yako wa mifugo utakuwa umemwachia nini? Nyama tu. *Anyway*, lakini kama tunaagiza maziwa, ngano na mafuta ya alizeti, na tuna ardhi ya kutosha, kweli itatuchukua miaka mingi sana kwenda mwezini *which is fine*. Angalau huku chini basi na sisi tuwe *giants* kwenye maeneo haya, na tumepata *experience* wakati wa UVIKO. Mipaka ilipofungwa hakuna mafuta ya kula. Sasa kwa sababu hatuna namna ya ku-*control* majanga haya yanayotokea huko duniani, ni afadhali tuwekeze kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kama alivyosema Mheshimiwa Prof. Muhongo, *commitment* tuliyofanya ya Malabo ya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kutokana na wachangiaji kuwa wengi na kwa mujibu wa utaratibu wa uongozaji wa shughuli za Bunge kwa ubora wake, kila mtu ajipange kwa dakika tano. Yaani kengele ya pili ikipiga ninazima sauti ili watu wengi wapate kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa Chiku Athman Issa na Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba wajiandae.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na kunipa kibali cha kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu na kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi mikubwa ya umwagiliaji ambayo imewekezwa katika nchi hii. Nitumie fursa hii kufikisha salamu za wananchi wangu wa Jimbo la Itwangi hususan katika Kijiji cha Nyida ambako kuna mradi mkubwa wa shilingi bilioni 14.6 unaoendelea kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wao wote. Mipango ni mizuri, ninachoomba, Wizara ya Fedha watoe fedha na kuwapatia Wizara ya Kilimo ili waweze kukamilisha mipango mizuri waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajikita katika kilimo cha umwagiliaji. Mradi wa umwagiliaji uliopo katika Kijiji cha Nyida unatakiwa kukabidhiwa tarehe 24 mwezi wa Tano, lakini kuna vitu vingi bado havijakamilika, na kwa sababu ya muda, ninaomba nisivitaje. Kwa kuwa nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri

mambo mengi hayajakamilika katika Mradi wa Nyida, lakini kwenye hotuba yao wameandika mradi umekamilika kwa 100%. Ninaomba Waziri atakapokuja hapa anipe majibu, ni kwa nini wamesema mradi umekamilika wakati kuna vitu vingi ambavyo havijakamilika ndani ya Mradi wa Nyida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii pia kuiomba Wizara ya Kilimo miradi ya umwagiliaji. Katika Jimbo la Itwangi kuna mradi wa umwagiliaji wa Kijiji cha Isholo lo. Mradi huu umetekelezwa miaka saba nyuma, lakini haukukamilika, umebakiza kipande kidogo sana mradi huu kwenda kukamilika. Serikali imewekeza fedha nyingi pale, lakini kwa sababu mradi haukukamilika, maji yanaingia na kutoka na fedha ile iliyowekezwa pale na Serikali inakuwa haina maana yoyote kwa sababu maji hayakai. Hivyo, nitamwomba Waziri atakaposimama anipe majibu ya kwenda kukamilisha mradi huu wa Bwawa la Isholo lo uliopo katika Jimbo la Itwangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Itwangi nimesema ninajikita katika umwagiliaji kwa sababu kwa Mkoa wa Shinyanga ndiyo jimbo tunalolima mpunga. Ukisikia mchele wa Shinyanga 80% unatoka Jimbo la Itwangi. Wananchi wa Jimbo la Itwangi kilimo wanachotegemea ni cha maji ya mvua. Tunashukuru na kuipongeza Serikali kwa miradi hii mikubwa ya umwagiliaji. Katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 kuna miradi ambayo imetajwa itakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara katika Mradi wa Butini kwenye Ilani ya Uchaguzi, kunatakiwa kwenda kujengwa mifereji 25 ya kusambaza maji kwenye mashamba ya mpunga. Katika Kijiji cha Nsalala, kwenye ilani inasema mitaro ya maji ya kupeleka kwenye mashamba yetu inatakiwa ijengwe mifereji 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika Jimbo la Itwangi mradi wa umwagiliaji wa Kijiji cha Masengwa umekuwa ni historia. Kila siku yamekuwa ni maneno, unawekwa kwenye bajeti hautekelezwi, lakini katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mradi huu pia umewekwa kwa kutekelezwa kujengewa mifereji 35 iliyopo ndani ya mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini sana utendaji wa Mheshimiwa Waziri, kwa kazi anajulikana yeye na Naibu wake na watendaji wake. Ninawaomba na kuwasihi sana katika miradi hii ambayo imetajwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi twende tukaitekeleze ili wananchi wa Jimbo la Itwangi kwa sababu ndio zao kubwa wanalolitegemea kwa biashara na chakula, tuwatendee haki kuhakikisha kwamba miradi hii inakwenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii imekuwa ni ya muda mrefu, na imekuwa ikitengewa fedha lakini haikamilishwi. Ninaomba sana, ninaisihi sana Serikali iweze kutoa fedha zinazopitishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya kilimo ambayo imewekezwa ndani ya vijiji vyetu na ndani ya majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ya umwagiliaji ikienda kukamilika, hakika tunakwenda kunufaika kwa kiasi kikubwa. Tunaongelea mazao mengine, lakini sioni mtu anaongelea zao la mpunga kwa maana ya mchele. Tunaujua wali ukiwa kwenye Sahani, lakini shughuli yake iliyoko kule ni kubwa, na wananchi wanahangaika kwa kusubiri mvua. Mvua zinapokatika, uhakika wa kuvuna zao hili unakuwa ni wa mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaisihi sana Serikali katika miradi yote iliyowekwa ya umwagiliaji, tuhakikishe kwamba inakwenda kukamilika na kulipandisha thamani zao hili la mpunga ambalo kwa kiasi kikubwa ni zao la biashara na ni zao la chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Azza. Tunaendelea na Mheshimiwa Chiku Athman Issa, Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba, Mheshimiwa Moses Charles Bujaga jiandae.

**MHE. CHIKU A. ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa

Rehema kwa kuniwezesha pia kusimama leo kuweza kuchangia katika Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi kubwa na *political will* yake iliyokuwa kubwa ya kuiangalia Wizara ya Kilimo. Tumeona tangu ameingia madarakani bajeti imekua kutoka shilingi bilioni 294 na sasa tunaenda shilingi trilioni 1.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana Mawaziri: Waziri Daniel Chongolo pamoja na Msaidizi wake Ndugu Silinde na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa mnayoendelea kuifanya. Mimi kwa sababu ya muda nitaongelea mambo mawili, na kama muda utaniruhusu nitaongelea benki ya ushirika ambayo inamiliki 51%. Pia, muda ukiniruhusu nitaendelea kuongelea Tume ya Maendeleo ya Ushirika zaidi kwenye taarifa za ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Benki ya Ushirika nchini. Benki hii inaenda kuwa mkombozi wa wakulima katika nchi yetu. Katika muda wa mwaka mmoja Benki hii imefanya mambo makubwa sana, lakini zaidi ya hayo Serikali yenyewe imewekeza kiasi cha 10% katika Benki hii, baada ya Serikali kuwekeza, wananchi kuwekeza pamoja na wanaushirika wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa wanaushirika, wamepewa 51% kwa makusudi makubwa ili waweze kuimiliki Benki yao wao wenyewe. Unapomiliki kitu chako, una uwezo wa kuhakikisha kwamba unakiendesha kwa jinsi ambavyo kinaenda kukusaidia zaidi kama mkulima. Tuna benki nyingi nchini, tukiongeza na Benki hii ya Ushirika tunaenda kupata mikopo. Ni Benki pekee sasa hivi ambayo inaweza kutoa riba ya *single digit* ya asilimia tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki hii katika kipindi cha mwaka mmoja mizania yake imetoka shilingi bilioni 49 ikaenda shilingi

bilioni 176. Amana zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 15 kwenda shilingi bilioni 114. Mikopo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 14 kwenda shilingi bilioni 104. Tunaiomba Serikali iishike mkono Benki hii. Pia, ningependa kutoa ushauri katika 51% ambayo Benki hii imepewa, wakulima pamoja na wanaushirika, wana *deficit* ya kufikia hiyo 51% kwa kiasi cha shilingi bilioni saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kupitia Tume ya Ushirika, tuwahimize wanaushirika wakamilishe mtaji wao uweze kufikia shilingi bilioni saba. Pia, ninamshukuru Rais, baada ya Benki kuanza kazi ilikuwa na *deficit* ya shilingi bilioni tano. Menejimenti, bodi pamoja na Tume ya Ushirika ilimfuata Rais na kuomba iwaongezee wanaushirika shilingi bilioni tano, Rais amefanya hivyo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kuona umuhimu wa chombo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Benki ya Ushirika ambayo imebadilika, na sasa inaitwa *CRDB*. Makosa yale yaliyofanyika kipindi kile yasirudiwe. Tunaomba watendaji, usimamizi, ukaguzi na bodi iweze kuisimamia hii benki kwa weledi. Ninaishukuru Benki ya *CRDB* ambayo imewekeza pia 20% katika benki hii. Ukiona benki kubwa kama *CRDB* inawekeza katika benki ya namna hii, jua kuna jambo kubwa na wana maono makubwa na wanatoa *support* kubwa kuhakikisha benki yetu hii inaenda kusimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, katika ile 10% kulibakia fedha kidogo ambayo Serikali ilikuwa haijaimalizia ya shilingi milioni 800. Tunaiomba Serikali basi imalizie ili kuweza kui-*support* benki yetu iweze kusimama na kufanya kazi vizuri na kwa weledi zaidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Lutengano Mwalwiba, Mheshimiwa Moses Bujaga na Mheshimiwa Patrick Mwalunenge wajiandae.

**MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara yetu hii Wizara muhimu ya Kilimo. Pia, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Chongolo pamoja na Naibu Waziri na viongozi wote kwa maana ya watendaji katika Wizara hii ya kilimo kwa hotuba nzuri ambayo wametuletea hapa iliyojaa matumaini na dhamira njema ya Mheshimiwa Rais jinsi ya kuweza kutatua changamoto na kuwasaidia wakulima katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hilo, pia ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais jinsi ambavyo ameonesha dhamira ya dhati ya kuweza kuleta mabadiliko kwa nia anayoonesha. Bajeti hii ilikuwa shilingi bilioni mbili miaka minne iliyopita, lakini leo ameipeleka mpaka kufikia kiwango cha karibu shilingi trilioni 1.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie mambo machache, mambo mengi mazuri yanafanywa na Wizara hii kama nilivyoeleza utendaji wa Mheshimiwa Waziri haujawahi kutiliwa shaka kutoka akiwa Mtendaji Mkuu wa chama chetu, lakini pia Naibu Waziri tunamfahamu pamoja na watendaji wengine wote wakiongozwa na ndugu yangu Gerald Mweli ambaye rekodi yake haina mashaka yoyote. Tunaomba tutoe mchango mchache kwenye maeneo machache ambayo tunaomba yaboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wananchi wa Jimbo la Busokelo tunao mtanzuko katika eneo la chai. Chai imeongelewa na Wabunge wengi. Wawekezaji wa chai *TATEPA* kule wamegoma kununua chai ya wakulima na mpaka hivi ninavyoongea wakulima hawana sehemu ya kuweza kuiuza chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilifungwa kutoka mwaka 2024, Kiwanda cha Mwakaleli mwaka 2024 na mwaka 2025 Kiwanda cha Tukuyu. Hali hiyo imezorotesha sana maendeleo katika eneo la Busokelo. Sasa nimeongea na Mheshimiwa Waziri mara kadhaa na ameonesha dhamira jinsi anavyokwenda kushughulikia jambo hili akishirikiana na wataalamu wengine.

Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho hapa atueleze ni jinsi gani anakwenda kutusaidia, kwa sababu mgogoro uliopo, wananchi wanatakiwa kuuza chai kwa shilingi 256 ambapo mwekezaji anataka na bei elekezi ya Serikali ni 366.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wananchi wanataka kujua, ni nini msimamo wa Serikali kwa mwekezaji huyu ambaye kimsingi ana mambo mengi anayoyafanya, yanaonesha kabisa kwamba ameshindwa kusimamia yale ambayo yalimfanya awe mwekezaji katika eneo lile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mwekezaji huyu Mheshimiwa Waziri afanye maamuzi magumu kama alivyochangia jana Mheshimiwa Mwanyika kwamba ikiwezekana aondolewe kwa sababu pamoja na mambo mengine, wenzetu wamempa mkopo mwingine wa shilingi bilioni sita, bado hanunui chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mkopo, wananchi ambao wana 30% wataendelea kudaiwa katika deni hili. Jambo hilo hatutaweza kulikubali kwa sababu ni sehemu ya dhuluma. Tunayo imani kubwa na Wizara hii, tunayo imani kubwa na Mheshimiwa Rais ambaye ametoa maelekezo kwamba wawekezaji wa namna hiyo wasipewe nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nilikuwa ninataka niongee kwa uchache kwa upande wa maparachichi pia. Mheshimiwa Waziri ninaomba nimshukuru sana Mkurugenzi wa Bodi ya Chai, tumeshirikiana kwa kiwango kikubwa kupambana katika kutatua jambo hilo. Baadhi ya mambo ninajua alitamani yangefanyika, lakini Wizara inayo nafasi ya kuweza kusaidia kuona namna gani tunaweza tukavuka kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, nilikuwa ninaomba kwa upande wa parachichi. Ziko parachichi ambazo wanasema ni za daraja ya kwanza na daraja la pili. Wanapokwenda kununua unakuta wanaziangua hizi na wanamwambia mkulima kwamba parachichi zako ni za daraja la pili. Sasa hapo inakuwa ni

changamoto sana kwa wakulima wetu. Tunaomba wenzetu wa *COPRA* pamoja na kazi nzuri wanayofanya, waweze kuwatumia wagani waliopo maeneo yale waweze kuwasaidia wakulima wetu ili kuondoa dhuluma hiyo na kuweza kujua. Tusingependa kuwa na maparachichi ya daraja la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia katika eneo la mbolea. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuhakikisha kwamba anatoa mbolea ya ruzuku na wenzetu wa *TFRA* hapa wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Ndugu yangu Joel, amekuwa anafanya kazi nzuri ya udhibiti, pamoja na wenzake, wanasimamia vizuri na kuhakikisha kwamba, hatuna changamoto zile za mwanzo za mbolea tulizokuwa tunapata, ambazo zilikuwa hazikidhi ubora. Katika kufanya jambo hilo, tumeona mikakati mizuri ambayo wamesema katika kutuletea mbolea, lakini pamoja na hivyo, ninataka niishauri Serikali, isikubaliane na wazo la kuuza Kampuni yetu ya Mbolea Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima ijue kuna maeneo ambayo kampuni nyingine hizi tunataka pia nazo ziboreshewe mazingira, haziwezi kupeleka mbolea. Ndiyo maana Serikali ni lazima iwe na mashirika kama hayo, kama ilivyo kwenye mafuta na maeneo mengine, ili yale maeneo ambayo wafanyabiashara wataona hakuna faida, basi wenzetu wa *TFC* wanaweza wakaifanya kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa pia, ninampongeza Mkurugenzi, Ndugu Msote, na wenzake, wanafanya kazi nzuri. Tuwaongezee nguvu tuweze kuhakikisha kwamba, wenzetu hawa wanafanya kazi iliyokusudiwa. Ninawashawishi Wabunge, kama Mheshimiwa Rais amesema anakusudia kuacha tabasamu kwa Watanzania, moja kati ya sekta na eneo ambalo tunaweza tukapata matokeo ya kuwa na mguso wa moja kwa moja kwa wananchi ni katika Wizara ya Kilimo. Ninaomba Serikali tuhakikishe kwamba, tutakapoipitisha bajeti hii, fedha inakwenda kama jinsi ambavyo imepangwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Moses Bujaga, Mheshimiwa Patrick Mwalunenge na Mheshimiwa Simon Songe, ajiandae.

**MHE. MOSES C. BUJAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii, na mimi kipekee kabisa, ninapenda nianze kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa jana. Ninawapongeza watendaji wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Gerald Mweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri kwa sababu ameonesha wazi kwamba yuko tayari kuweka mwendelezo kwenye sekta hii ya kilimo. Sekta ya Kilimo inahitaji uwekezaji wa muda mrefu. Matokeo ya uwekezaji katika Sekta ya Kilimo hayatokei ndani ya muda mfupi. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu, katika hotuba yake ameonesha jinsi ambavyo ataendeleza programu za maendeleo ambazo zimeanza chini ya Kesho Iliyo Njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, ameonesha ni namna gani ambavyo bajeti yake imejikita katika Dira ya Maendeleo 2050. Jambo moja la msingi sana ambalo bajeti ya Mheshimiwa Waziri imesema ni kwamba, ameangalia mpango na bajeti, mpango kabambe wa mageuzi ya kilimo 2050. Tanzania *Agricultural Masterplan* haijawekwa wazi kwetu, kwa hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri asiweke mpango huu kwenye *shelf* za ofisini kwake. Mpango huu uwe ndiyo kipimo cha namna gani kilimo chetu kinafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa sababu, ameonesha umuhimu wa kuendeleza miradi ya umwagiliaji, miradi ambayo kwa namna fulani imesimama kwa muda mrefu, lakini Mheshimiwa Waziri ameonesha kwamba, itaendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, miradi ya umwagiliaji ambayo iko Wilaya ya Kwimba, hususan Jimbo la Sumve, ipewe kipaumbele kwa sababu, sasa hivi wananchi wa Jimbo la Sumve ni wazalishaji wakubwa wa zao la

mpunga. Katika Wilaya ya Kwimba peke yake tunazalisha zaidi ya tani 60,000 hiyo ni zaidi ya shilingi bilioni 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri ni kwamba, ametambua umuhimu wa kuongeza tija kwenye mazao ya kilimo. Tatizo la wakulima wetu limekuwa ni ongezeko ama uduni wa uzalishaji na ameonesha kwa uwazi kwamba, tija ndiyo mwelekeo, lakini jambo moja ambalo Mheshimiwa Waziri hakulisema sawasawa, ameongelea tu ukuaji wa uzalishaji wa mazao asilia, hajaongelea ni namna gani tija itaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema 2025 mazao ya biashara asilia tulizalisha tani 1,600 tunatarajia sasa 2026 tuzalishe tani 2,118, lakini Mheshimiwa Waziri hajatuambia ni kwa namna gani zao la pamba, kwa mfano, ambalo tija yake mpaka sasa hivi tuko 20%, tunapanda vipi kufikia kilo 1,000 kwa hekta. Kwenye zao la korosho tuko 18%, tunapanda vipi kutoka kilo nne na nusu kwa mti, kwenda kilo 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbaku tunafanya vizuri, tuko 77%, tunazalisha kilo 1,400 kati ya kilo 1,800. Sasa, kilimo ni takwimu, tunahitaji *numbers* kuona namna gani tunatoka kwenye uzalishaji duni, ili wananchi wetu ambao amesema ni wawekezaji (kilimo ni biashara na mkulima ni mwekezaji), ni namna gani wanatoka kwenye uzalishaji duni, ili wazalishe kwa tija na tuwaondoe katika umaskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ndugu yangu, Mheshimiwa Mbunge kutoka Kwimba amezungumzia jana. Mkoa wa Mwanza tunazalisha 20% mpaka 25% ya mazao jamii ya mikunde. Wakulima wa Mkoa wa Mwanza, Wilaya ya Magu, Wilaya ya Kwimba, Wilaya ya Sengerema na Wilaya ya Misungwi wanapanda kwa nguvu zao, wanalima kwa nguvu zao, wanatafuta mbegu kwa nguvu zao; wanapovuna wanakuja watoza ushuru. Anapovuna tunamwona *COPRA* na *TMX*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu wanachajiwa shilingi 230 kwa kilo moja ya choroko, kwa kilo moja ya dengu.

Sasa tunataka hawa watoza ushuru wajue kuwekeza kwa wakulima wetu ili unapokuja wakati wa mavuno washiriki nasi katika ulimaji, na upandaji, ili waweze kufaidika na kile tunachokivuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anasema zitanunuliwa mashine 100 za kusafisha, kuchambua na kupanga madaraja ya zao jamii ya mikunde na zitasambazwa kwa *AMCOS*, kwenye mikoa mingine, lakini Mwanza haimo. Tunataka Mheshimiwa Waziri anapokuja kufanya majumuisho jambo hili aliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la *agriculture financing structure*. Sasa hivi mifuko mingi ya mazao ipo kwa ridhaa ama kwa utaratibu wa Waziri peke yake. Ninapendekeza Mfuko kama wa Pamba *CDTF*, Mfuko wa Korosho *Export Levy,* Mfuko wa Maendeleo ya Sukari *Agriculture Development Fund,* itengenezewe *legal framework,* ili iwepo kisheria, isiwe tu kikanuni.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Patrick Mwalunenge, Mheshimiwa Simon Songe na Mheshimiwa Daniel Tlemai, ajiandae.

**MHE. PATRICK A. MWALUNENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja iliyoko Mezani, ya Wizara ya Kilimo. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa uthubutu wake, toka alipoingia madarakani ameonyesha dhamira ya dhati kwamba, anataka kupandisha kilimo chetu na kutengeneza ajira kwa vijana wetu ambao wamekosa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amefanya mambo mengi; la kwanza ni kuasisi mfumo wa mbolea, kwa maana ya ruzuku ya mbolea. Sisi sote ni mashahidi, alipoingia madarakani mbolea ilikuwa inauzwa zaidi ya shilingi 140,000 mpaka shilingi 160,000. Wakati mwingine ilikuwa haipatikani hata kwa pesa hizo, lakini Mheshimiwa Rais alihakikisha kwamba, mbolea inapatikana muda

wote kwa bei ya chini ya shilingi 70,000. Hiyo ni hatua kubwa ya maendeleo kwa wakulima wetu wa Tanzania, wanatakiwa wajue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha mbolea kuuzwa chini ya shilingi 70,000, maana yake ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inalipa gharama ya fedha hiyo na hii imeleta matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, pamoja na changamoto zote za bei ya mafuta na gharama nyingine zote, bado mfumuko wa bei ya chakula uko chini. Maana yake ni kwamba, Wizara ya Kilimo inabeba gharama nyingi, inatoa ruzuku ya mbolea, inatoa mbegu, miche, na kadhalika. Ndiyo maana unakuta sasa gharama za uzalishaji kwa mkulima zimekuwa siyo kubwa sana na mfumuko wa bei kutokuwa mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Waziri wa Kilimo, ndugu yangu, Mheshimiwa Chongolo na Naibu wake, sina mashaka naye. Tumeisikiliza bajeti, ni nzuri na inaonesha mwelekeo kwamba, vijana wetu wanapata matumaini. Waliomaliza vyuo vikuu sasa wanaweza wakaenda kuwekeza kwenye kilimo kwa sababu, mazingira ni mazuri. Umesema kwamba, ardhi itaenda kupimwa ili kujua inahitaji mbolea ya aina gani kwenye eneo husika, uwekezaji kwenye mabwawa, kwa maana ya skimu za umwagiliaji na ujengaji wa maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo yote ni *value chain* ambayo inaonesha kabisa kwamba, sasa kijana wetu wa Kitanzania ambaye ni msomi, akiamua kwenda kuwekeza au kufanya shughuli za kilimo, atafanya kwa tija, kwani ana uhakika wa kulima, ana uhakika wa kuvuna na ana uhakika wa kuhifadhi yale mazao ambayo yanaweza yakapotea wakati ule wa kuhifadhi baada ya mavuno. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaipongeza Wizara ni kwamba, wamesema wataendelea kuboresha huduma za ugani, maana katika jambo kubwa ambalo wakulima wetu wanahangaikia, ni shughuli za ugani.

Mmea umefika juu, unaanza kushambuliwa na wadudu, unakuta hana taarifa ni kitu gani kimemsibu. Mwisho wa siku inamsababishia hasara kubwa sana mkulima. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake, waendelee hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninawapongeza *COPRA*, wanafanya kazi kubwa kwa sababu, haya mazao mengi ambayo hayakuwa na bodi, baada ya kuundwa *COPRA*, tumeona mabadiliko makubwa kwenye mazao kama ya parachichi, ufuta na mengine yanayofanana na hayo, lakini bado *COPRA* waongezee nguvu, ili waweze kusajili wakulima wao wenyewe. Waweze kuyaangalia yale mazao yakiwa shambani kwa sababu, imekuwa ni changamoto, mazao mengi yanayokwenda kuuzwa nje ya nchi, yanakuwa na changamoto kwenye suala la ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *COPRA* wawekewe nguvu waweze ku-*control* mazao kuanzia shambani mpaka yanakokwenda kuuzwa, ili kuhakikisha kwamba, yanapata bei nzuri na soko la uhakika. Imekuwa ni mara nyingi mkulima amevuna mazao yake, anakwenda kuyapima, anaambiwa mazao haya hayana ubora, anarudishwanayo. Kwa hiyo, ni lazima *COPRA* iwe ni jicho la kuangalia yale mazao kuanzia kule shambani mpaka yanapokwenda kwa mlaji wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ni lazima Wizara ya Kilimo iwe na mahusiano na Wizara nyingine. Wizara ya Kilimo ndiyo Wizara mama, lakini ni lazima iwe na mahusiano ya karibu na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa maana ya TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Fedha na ikiwezekana kuwe na kamisheni moja, kiundwe chombo ambacho wanawasiliana kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo hii tukimwambia Waziri atupe takwimu ni viwanda vingapi ambavyo vinazalisha juisi ya matunda? Vimetumia matunda kiasi gani ya kwetu *versus* yale ma-*carbonates* yanayoagizwa toka nje, kemikali kwa ajili ya kuzalisha juisi ya matunda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaona vitu hivyo haviashabihiani. Tunataka watu wetu wanufaike kupitia biashara ya uzalishaji wa matunda. Sasa unakuta takwimu zinakuwa hazipo, mwisho wa siku matunda ya wakulima wetu yanaoza na wakati huo kuna viwanda vinazalisha matunda ya juisi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Simon Songe, Mheshimiwa Daniel Tlemai na Mheshimiwa Edwin Swalle, ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Nataka nizungumze eneo la zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumza mambo mengi katika zao letu la pamba ambalo takribani 51% mpaka 60% linazalishwa katika Mkoa wa Simiyu. Nimeona katika mpango uliokuwepo wa mwaka wa fedha 2025/2026 ilikuwa ni kuzalisha takribani tani 400,000 za pamba, lakini zilizozalishwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 mpaka kufikia Machi, ilikuwa ni tani 222,014 ambayo ni sawa na 55%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona bado tuna safari ndefu katika uzalishaji wa zao la pamba. Nina mambo mawili ambayo ninataka nichangie hapa. Mheshimiwa Waziri amesema, katika mpango wa uzalishaji wa zao la pamba watajikita katika uzalishaji wenye tija. Ninakubaliana naye, kwani uzalishaji wenye tija ndiyo uzalishaji unaotakiwa sasa hivi, lakini kuna mambo mawili ambayo tunatakiwa kuyaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni utafiti wa mbegu. Nina wasiwasi na mbegu tunayoitumia sasa hivi, inawezekana imepitwa na wakati ndiyo maana tunahitaji pembejeo na dawa nyingi katika kutibu magonjwa ambayo yanaathiri zao letu la pamba. Ukitumia pembejeo nyingi katika

kutibu zao la pamba maana yake ni kwamba tutatumia fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri, ametumia takribani shilingi bilioni 61 kuhudumia pembejeo katika zao la pamba, na hii ni kwa sababu ya mbegu kutokuhimili. Wadudu ni wengi. Wadudu wakiwa wengi, maana yake ni kwamba tunatumia dawa nyingi na uzalishaji wake unakuwa hafifu kwa sababu, pamba inakuwa ya njano. Sasa nini kifanyike hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tujikite katika utafiti wa mbegu zitakazozalishwa ili kuhakikisha kwamba, zao la pamba tunalilima na tunapata, ndipo tutakapoenda kwenye uzalishaji wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni *BBT* kwa vijana wetu. Ninakubaliana kabisa na Programu ya *BBT* kwa vijana, na ni jambo ambalo linaenda kuimarisha katika uzalishaji wenye tija. Ninakubaliana na hilo. Hapa nini kifanyike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, chukulia mfano, Mkoa wa Simiyu una kata 133, fanya *assumption* katika kata 133 kata ambazo zinazalisha pamba tufanye ni kata 120. Tumpe kijana mmoja kusimamia shughuli za ugani kwenye kata moja. Tunahitaji vijana ambao watashughulika na *BBT,* vijana 120. Tukienda na vijana 120, tukawalipa shilingi 600,000 kwa mwezi, tutatumia takribani shilingi bilioni 864 kwa mwaka kwa vijana wote 120. Nini tunataka kupata hapa? Nina imani tija inaenda kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa pamba kwa ekari sasa hivi unaenda kilo 200 mpaka kilo 300. Chukulia kilo 200 bei iwe kubwa, fanya shilingi 2,000. Mkulima atapata kwa ekari shilingi 400,000 lakini tukiwa na tija iliyo nzuri ya kuzalisha kilo 500 kwa ekari moja, mkulima atapata shilingi 1,000,000. Ndiyo maana ya kuwa na tija kwenye uzalishaji wa zao la pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali tukiwaajiri sisi wenyewe bila kuwabugudhi, hawa wawekezaji ambao sasa hivi

wameenda kwenye kilimo cha mkataba, ambapo mwisho wa muda watataka mkulima auze pamba yake kwa huyu mwekezaji, tukihama huko, Serikali iwaajiri hawa *BBT,* vijana waende kufanya kazi na wao wawe na *logbook* ya kuwatembelea wakulima. Mimi nitawaambia wakulima wa Jimbo la Busega, kila mkulima awe na *logbook*, akifika shambani huyu mtu wa *BBT* asaini pale kwamba amefika ili tumhudumie Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, hawa *BBT* na wenyewe wawe na mashamba ya mfano. Kama Waziri mwenyewe, Mheshimiwa *Comrade* Chongolo, pale kijijini kwake ana shamba, kwa nini *BBT* hana shamba la mfano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri huyu *BBT* naye awe na shamba la mfano kwa ajili ya wakulima walioko kwenye maeneo yetu. Baada ya kusema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mheshimiwa Edwin Swale, Mheshimiwa Mariam Nyoka, ajiandae.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, ninamshukuru Waziri, Naibu Waziri na watu wote kwenye Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unaanzia kwenye ukosefu wa mbolea kwa Takribani miezi minne sasa. Wizara wamejipangaje kwenye eneo hili la mbolea? Kwa sababu, katika jimbo langu takribani miezi minne sasa upatikanaji wa mbolea ni changamoto. Hii imechukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali inatoa mbolea ya ruzuku, lakini kwa sasa kila mwananchi anapewa mbolea mbili mbili au mbolea moja moja katika jimbo langu, na ninaamini na maeneo mengine katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa je, Wizara wamejipangaje katika upatikanaji wa mbolea? Kama changamoto ni vita inayoendelea katika nchi za wenzetu, mbona kwenye eneo la mafuta inapatikana? Kwa nini Wizara ya kilimo iko nyuma zaidi kuwatetea watu wao katika eneo hili la kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishauri Wizara. Hivi kulikuwa na ubaya gani kama mbolea inaletwa yenye ruzuku na ambayo haina ruzuku, ili inapoonekana mbolea ina upungufu kwa sababu, lalamiko la wafanyabiashara kwa sasa wanasema ni Serikali. Zile fedha za ruzuku hawaziweki kwa muda, ndiyo maana wafanyabiashara wanachelewa kuagiza mbolea kutokana na ucheleweshwaji wa fedha zile sasa za ruzuku inayowekwa kwa wafanyabiashara wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaonaje sasa kwamba, ilete mbolea ambayo haina ruzuku, ambayo mimi ambaye nitaona mbolea ya mifuko miwili hainitoshi, nitakwenda kununua ambayo haina ruzuku, ili mazao yangu yasiweze kuharibika katika maeneo yetu katika Jimbo letu la Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni katika Stakabadhi Ghalani. Mwaka 2025 Jimbo langu la Karatu limeingizwa katika mazao ya dengu na mbaazi na hakuna *AMCOS* hata moja katika jimbo zima. Vilevile utaratibu mzuri wa watu wetu wakivuna kipindi cha mwezi wa Nane mpaka mwezi wa Kumi, hupeleka mazao sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali kwa mwaka 2025, iliingia kwenye mageti kuzuia kwamba, sasa mazao yapelekwe ghalani, wakati huo katika jimbo langu zima hakuna ghala wala *AMCOS* ambayo Serikali inasema kwamba, tupeleke ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto kubwa katika Jimbo langu la Karatu, mwaka wa 2025 ilituletea shida kwa sababu hakuna mahali popote pa kupeleka mazao. Chaji zao za kupiga faini watu za kuanzia shilingi milioni moja mpaka milioni tano na wakati huo Serikali haijajipanga kuandaa maghala hayo na hizi *SACOSS* katika maeneo ya Jimbo langu la Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lingine la mipaka, Serikali yetu huwa kwa sasa wanasema tuna chakula kwa kiwango cha zaidi ya 100%, lakini inapofikia kipindi inapungua asilimia hiyo kutoka chini ya mia moja, wakati kuna upungufu wanasema mipaka yetu ifungwe kwa sababu ndani ya nchi yetu kuna shida ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Wizara hii ilikuwa inatafuta masoko, wakati huo soko limeonekana huko nje, Serikali inaanza kusema tuna njaa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, siyo kazi ya mkulima wa Tanzania kwenda kulisha wananchi wa Tanzania, kazi ya mkulima wa Tanzania ni kwenda kulima apate fedha na maendeleo mengine yaendelee ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi nyingine za nje zinapokuwa na njaa ndiyo fursa kwa mkulima wa Tanzania kwenda kupeleka mazao yake mahali popote, nchi zingine zote ambazo zina uhitaji wa chakula kipindi hicho. Huko nyuma imetokea na kutaifishiwa magari ya watu, imetokea katika mipaka yetu watu kutaifishiwa magari na mazao, lakini kwa miaka hii minne ya Dkt. Samia Suluhu Hassan tunatoa shukrani kwamba mipaka haijafungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ninaomba Wizara iendelee kuachia mipaka ili watu wetu wanapopata soko katika maeneo mengine ya nje waweze kupeleka mazao yao. Kama Serikali hii inaenda kutafuta masoko, Serikali hii hii tena inasema mipaka ifungwe itakuwa ni jambo ambalo halipendezi kwa wakulima wetu, tutie wakulima wetu moyo katika eneo hilo la mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Karatu tulipata bahati ya kupata hela katika eneo la umwagiliaji. Serikali ilitupatia fedha shilingi milioni thelathini na nane na milioni mia tano katika skimu ya Kata ya Baray na Kata ya Mang'ola. Vilevile, Serikali ilitupa fedha shilingi bilioni ishirini na moja kuzuia maji katika korongo la Mto Baray. Hata hivyo, mradi ule wa shilingi bilioni ishirini na moja una changamoto kubwa, sasa tuna miaka mitatu,

Serikali ilitoa fedha shilingi bilioni 3.5, kwa sasa mkandarasi yuko *site* anakaa tu mpaka miaka mitatu na Serikali imetoa fedha. Watu wa tume waliangalie hilo, katika eneo hilo la Mto Baray imetolewa shilingi bilioni 3.5 na mkandarasi yuko *site,* lakini hakuna kazi inayoendelea kwa sasa ni miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la umwagiliaji mradi wa shilingi 38,500,000,000 ambao uko katika Kata ya Baray na Kata ya Mang'ola unaendelea vizuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda kuweka jiwe la msingi mwaka huu katika eneo hilo la skimu katika Mto wa Qangdend katika Bonde la Eyasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Edwin Swalle na Mheshimiwa Maryam Nyoka na Mheshimiwa Haidary Sumry wajiandae.

**MH. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nianze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo ambayo ni hotuba muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niseme kwamba, nilikuwepo hapa ndani wakati Rais, Samia Suluhu Hassan, anakuja kuhutubia Bunge kwa mara ya kwanza. Nikiwa kama Mbunge wa awamu ya pili, ninaweza kusema kwa ushahidi, Dkt. Samia anawapenda sana wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Chama Cha Mapinduzi kinawapenda sana wakulima wa nchi hii. Kwa kiwango ambacho Rais ameongeza bajeti, kutoa ruzuku ya mbolea na kununua mahindi, ni dhahiri Dkt. Samia anawapenda wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninatumia nafasi hii pia kumshukuru sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo, kwa hotuba yake nzuri iliyoonesha dhamira ya kweli ya kuwasaidia wakulima wa Tanzania. Ninampongeza pia

Mheshimiwa Silinde na wataalam wote wa Wizara hii akiwemo Katibu Mkuu, Ndugu yetu Mweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea mambo matatu tu kwa asubuhi ya leo. Jambo la kwanza nianze na ushirika. Nimesoma kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 117-124, wameongea vizuri kuhusu ushirika, wana mpango wa kuhamasisha wananchi wafungue *SACCOS*, vikundi viunde *SACCOS* na kadhalika. Ushauri wangu kwa Serikali, ndugu yangu Dkt. Ndiege ninajua ananisikia vizuri sana. Tatizo kwenye ushirika ni vyama vya ushirika kuwaibia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Njombe kwa mfano, maeneo mengi vyama vya ushirika vimeibia wakulima fedha. Lupembe wananchi wangu wameibiwa fedha, Makambako ambako Mheshimiwa Waziri ametoka pale na nimsemee yuko hapa. Pale Makambako chama cha ushirika kimekula fedha za wakulima, ukienda Igumila, ukienda Njombe. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwenye hotuba hawajasema wana mpango gani wa kuwasaidia wakulima walioibiwa fedha zao kwenye ushirika ziweze kurejeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu sana, waje na huo mpango mahsusi watuambie wakulima hawa kabla ya kuhamasisha kufungua *SACCOS* zingine, watuambie wananchi ambao hela zao zimeibiwa wanawasaidiaje fedha iweze kurudi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu zao la parachichi. Sisi Mkoani Njombe kama wakulima wa zao la parachichi, wananchi wengi wanalima haya matunda. Changamoto kubwa ni juu ya uhifadhi wa mazao ya parachichi. Wananchi wa Lupembe wamenituma, niiombe sana Serikali kwenye mpango wake ambao inakwenda nao watusaidie kujenga *cold rooms* kwa ajili ya kuhifadhi matunda ya parachichi ili kusudi yaweze kuwa na bei nzuri na yasiuzwe kwa kutupwa kama sehemu ya *reject*. Hii ni hoja muhimu, jimbo la Lupembe wanaomba kujengewa *cold room* na hata wananchi wa Makambako kwa Mheshimiwa Waziri wanahitaji *cold room* pia kwa ajili ya matunda ya parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni zao la chai. Ninaipongeza sana Wizara hii, nimesoma kwenye hotuba, kwa mara ya kwanza zao la chai limeandikwa angalau kwa *page* nne. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, ameandika *page* nne kujadili zao la chai na hapa ninampongeza sana pia Mkurugenzi wa Bodi ya Chai, dada yangu Beatrice Banzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wameandika mipango humu kwenye hotuba hii kwamba wana mpango wa kulikwamua zao la chai. Ombi langu Mheshimiwa Waziri, wananchi wa Lupembe wamelia kwa muda mrefu kutaka kiwanda chao kirejeshwe. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, wamesema kwenye taarifa hii, wakirudi ofisini baada ya bajeti hii wakarejeshe kiwanda cha wakulima wa Lupembe tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, wamesema zao la chai duniani bei imepanda kutoka shilingi 2,450 mpaka shilingi 4,000. Ninataka niiombe sana Serikali, badala ya kujadili kupunguza bei ya chai, tufikirie kuongeza bei ya wakulima wa chai hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine pia kwenye chai, sisi watu wa Mkoa wa Njombe wanaweza wasituelewe, tunaposema kuhusu viwanda vya *DL*, hatusemi *personal*. Viwanda hivi vilichukuliwa vikiwa vinafanya kazi, lakini baada ya viwanda vyote vile kuwa vimechukuliwa sasa havifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kwenye taarifa kwamba wanakwenda kufanya tathmini. Mheshimiwa Waziri, waende wakafanye tathmini viwanda vya chai, kama wawekezaji hawa wamekiuka masharti, wachukue hatua wapewe watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa asubuhi hii pia niseme kuhusu pembejeo za wakulima. Wananchi wetu ni kweli wanapata mbolea na mbegu, lakini masoko ya uhakika kwenye mazao wanayovuna, bei ambayo wanalima na bei ambayo wanauza haviendani! Tunaiomba Serikali iwasaidie wakulima wapate bei nzuri ya kuuza mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja hizo tatu, ninaunga mkono hoja hii ipite kwa kishindo ili Waziri akafanye kazi yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka. Mheshimiwa Haidary Sumry na Mheshimiwa Exaud Kigahe wajiandae.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza, ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na ninaipongeza Wizara kwa hotuba yao nzuri ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwenye zao la mahindi Mkoani Ruvuma. Mkoa wa Ruvuma tunapata mbolea za ruzuku na pia tunapata mbegu. Hata hivyo, ninaiomba Serikali kupitia Wizara yake iandae utaratibu kwa wataalam wetu kupita mashambani ili wapate takwimu sahihi za wakulima ili mahitaji ya wakulima yaendane na mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kwenye zao letu hili. Serikali inanunua mahindi kupitia Wakala wake wa *NFRA*, lakini hawanunui mahindi yote kulingana na uwezo au labda sijui utaratibu wao ambao wamejiwekea. Mahindi yale yakibaki yananunuliwa na walanguzi, hivyo kusababisha walanguzi wale kupanga bei ambayo iko chini kwa mkulima na ambayo haimnufaishi mkulima wetu. Ninaiomba Serikali, kutokana na *NFRA* kuwa na uwezo usiokidhi kununua mazao yote, basi kuwe na soko huria ili mkulima aweze kuuza mazao yake popote pale ili awaze kupata manufaa kwenye mazao yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ni Serikali kuchelewesha malipo ya mazao kwa wakulima wetu. Ninaiomba Serikali iwalipe wakulima kwa wakati kwani kuchelewesha kuwalipa wakulima hawa kunasababisha kushindwa kulima kwa wakati na kukosa pembejeo. Hali ambayo inasababisha msimu mwingine wa mazao kuchelewa kulima kwa ajili ya ukosefu wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara kupitia wataalam wake, ni vyema wakazalisha mbegu za kutosha ndani ya nchi. Tena ziwe mbegu zenye ubora na zipatikane kwa bei nafuu. Kutegemea nje inakuwa siyo sawa, hata hivyo, tunaona madhara ambayo tunayapata hata sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaiomba Wizara iandae utaratibu wa kufanya ukaguzi wa maduka ya pembejeo mara kwa mara ili kuweza kubaini mbegu na viuatilifu visivyo na ubora na vilivyopitwa na wakati wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mariam kwa kutumia vizuri dakika tano. Tunaendelea na Mheshimiwa Haidary Sumry, Mheshimiwa Exaud Kigahe na Mheshimiwa Thomas Maganga wajiandae.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu na kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, niendelee kumshukuru na kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, jemedari ambaye anaongoza mapambano kuhakikisha kwamba nchi hii inaenda kwenye mabadiliko makubwa kwenye Wizara hii ya Kilimo. Ninawapongeza na kuwashukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu wake na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Mpanda Mjini tuna maeneo ambayo yanapaswa kulimwa kwa kilimo cha umwagiliaji, maeneo mawili. Eneo la kwanza ni eneo la Mwamkulu. Ninaishukuru sana Serikali kuna mradi pale wa umwagiliaji unaendelea na tayari umeshafikia 70%. Tunaishukuru sana Serikali, lakini rai yangu katika eneo hili, tunaiomba Serikali ikamilishe huu mradi na kubwa zaidi iweze kujenga mabwawa, kwa sababu tunatamani kupata matokeo. Mradi huu ukikamilika

kufika 100% ya ujenzi wa ile miundombinu ya umwagiliaji, kama hatuna bwawa tafsiri yake wakulima watabaki kwenye hatua ile ile ya kulima mara moja kwa mwaka ambayo siyo malengo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba sana Wizara ije na mpango wa kujenga mabwawa na wakulima na wananchi wa eneo lile wako tayari na wameupokea vizuri mradi. Tunaamini watazalisha karibu mara mbili au mara tatu ya kile wanachozalisha sasa. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, tupia jicho kwenye eneo hilo ili tuweze kupata matokeo ambayo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, anatarajia kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la hii Skimu ya Umwagiliaji ya Kakese kumekuwa na ahadi za Serikali na juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya ziara kwenye jimbo langu. Maombi yangu na ya wananchi wa Jimbo la Mpanda Mjini ilikuwa ni kuomba hii skimu sasa ianze kujengwa. Majibu ya Naibu Waziri wa Kilimo ambaye tulikuwa naye kwenye ziara hiyo alisema kwamba Serikali wakati wowote itatangaza zabuni ya huu mradi ili sasa kazi ya ujenzi wa hii skimu ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia kwenye hotuba yote ya Wizara ya Kilimo nimeona kwamba tuko kwenye upembuzi yakinifu kwa 25%, mambo hayo yalishafanyika tayari na kwa 100% mambo yote yameshakamilika, sasa kwa nini wanaturudisha kwenye upembuzi yakinifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kupitia Wizara, wautangaze mradi huu wa Kakese ili nao uweze kuanza kujengwa. Ukianza kujengwa utaleta ukombozi na utaongeza mapato kwa Serikali, lakini pia utaongeza mapato kwa Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda ambayo bajeti yake kwa 50% wanategemea haya mabonde mawili ili kuweza kupata mapato ya ndani ya Halmashauri. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri azingatie huu mradi atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi wa Kakese ambao bwawa lake litajengwa kwenye eneo la Dilif utahudumia

mabonde mawili, utahudumia Jimbo langu la Mpanda Mjini na Jimbo la pili la Mheshimiwa Lupembe kwenye eneo la Nsimbo. Kwa hiyo, unaona ni muhimu kiasi gani bwawa na mradi huu uanze kujengwa ili kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea eneo la umwagiliaji, niende kwenye soko. Ahadi ya Ilani ya CCM ya mwaka 2025 - 2030 ni kujenga Soko kubwa la Kimataifa la Mazao kwenye Jimbo langu la Mpanda Mjini. Ninaiomba Serikali, hiyo pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni, mambo mahsusi aliyoongelea ni pamoja na hili soko la mazao kwenye Jimbo langu la Mpanda Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, tunafahamu ndiyo umeingia kwenye Wizara, inawezekana mambo hayajakaa sawasawa. Ninakuomba katika bajeti ijayo, sijaliona kwenye bajeti hii, ninakuomba katika bajeti ijayo, basi watutengee ili na sisi tuweze kupata soko. Tuna soko dogo pale…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna soko dogo pale ambalo linafanya vizuri, lakini watu wanapigwa na jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Ninaunga mkono hoja na Mungu awabariki sana Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Exaud Kigahe na Mheshimiwa Thomas Maganga na Mheshimiwa Neema Mwandabila wajiandae.

**MHE. EXAUD S. KIGAHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo. Kwanza, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyetujaalia kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu siku hii ya leo. Pili, ninachukua nafasi

hii kutoa pongezi za kutosha na nyingi kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya sekta tunayoiongelea leo, sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi za kutosha pia kwa Wizara ya Kilimo chini ya *Comrade* Chongolo, mkulima mwenzangu ambaye kwa kweli amekuja na mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo na huu ni mwanzo mzuri. Ahsante sana na pongezi zote kwa Wizara nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninashukuru sana, Waziri, mkulima mwenzangu na mimi hii ni Wizara yangu, ni mkulima katika sekta ya chai, ninakushukuru sana. Changamoto ya sekta chai kwangu mimi, Jimbo la Mufindi Kaskazini, kilimo ni maisha kama walivyosema wengine lakini sisi chai kwetu ni maisha. Yeye anajua mimi nimelelewa kwenye chai na chai ndiyo kila kitu kwetu. Leo hii changamoto ya chai chini ya mwekezaji ambaye wengi wamemsema *DL Group* kwa kweli ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii, wananchi wenzangu, wakulima wenzangu na wafanyakazi wengine, moja; mwekezaji huyu anadaiwa zaidi ya shilingi 5,000,000,000 kwa michango ya wafanyakazi katika kile Kiwanda cha Itona. Pili, wakulima wadogo wanaopeleka chai katika kiwanda kile hawajalipwa kwa zaidi ya miaka karibu miwili sasa. Tatu, wazabuni waliokuwa wanapeleka tenda pale nao wanadai. Kwa hiyo, ni changamoto kubwa katika maeneo mengi ikiwemo pale kwangu Mufindi Kaskazini katika Jimbo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wengi sasa ambao tuliwahamasisha kulima chai katika Kata za Ihanu, Mdabulo, Ihalimba, Ifwagi na maeneo jirani wana changamoto kubwa. Mwekezaji huyu pamoja na mambo mengine, analima chai, lakini amekuwa na changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tuna makampuni mawili, *DL Group* na *Brown*. *Brown* anafanya vizuri, changamoto aliyonayo yeye hatuielewi, kama walivyosema wenzangu tunadhani labda mwekezaji huyu ana nia ovu au hana nia njema. Tukasema mhujumu kwa namna moja au nyingine. Wizara ya Kilimo tunaomba wachukue hatua tuone namna gani tunawakwamua Watanzania ambao wanategemea kilimo na hasa Jimbo la Mufindi Kaskazini na maeneo mengine ambayo tunalima chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iringa inashika nafasi ya pili sasa kwa *GDP per capita*, baada ya Dar es Salaam ilikuwa Mbeya sasa tunakuja juu. Mengi haya katika Mkoa wa Iringa *GDP per capita* inatoka Wilaya ya Mufindi na moja ya maeneo ambayo yanatoa fedha nyingi ni kwenye sekta ya kilimo ikiwemo chai. Hatuko tayari kuona tunashuka kwenye *GDP per capita* kuwa namba mbili kwa sababu ya wawekezaji ambao hawafanyi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya chai ninashukuru, lakini niseme kidogo kwenye maeneo mengine, kwenye umwagiliaji kama walivyosema Wabunge wenzangu, tunadhani maendeleo sasa kwenye sekta ya kilimo tukuze umwagiliaji. Kwenye Jimbo la Mufindi Kaskazini tunayo skimu ya umwagiliaji ya Ikweha ambayo imekwama kwa zaidi ya miaka 10. Zaidi ya shilingi 800,000,000 ziliwekwa pale, mradi ule umekuwa sasa wenzetu wazungu wanasema *white elephant*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 800,000,000 zimelala pale na sisi kule tulikuwa tunatumia mabonde haya kwa kilimo *a.k.a* vinyungu, wanajua ni bustani zile za mabondeni. Baada ya kuboreshwa imekuwa sasa haifanyi kazi, badala ya kuboresha sasa imekuwa ni uharibifu, wananchi sasa wanashindwa kuzalisha kwenye eneo lile la bonde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, Tume ya Umwagiliaji iliahidi mwaka jana ikaja kukagua, wakasema wanaleta fedha mpaka leo kimya. Tunaomba mradi huo wa umwagiliaji wa

Ikweha ukamilike mapema kama ambavyo Rais amekuwa akitaka kilimo kiendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu mbolea. Nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kuzalisha mbolea hapa nchini. Tuna *INTRACOM* lakini pia tuna kile cha Minjingu, wananchi sasa wameanza kuamini mbolea zinazozalishwa ndani. Niiombe Serikali yangu na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ana nia njema, tuone namna gani; moja, kuhakikisha kwamba tunawawezesha wawekezaji wa ndani ili wazalishe kwa tija ili tuendelee kufaidika na uwekezaji wa ndani na kuhakikisha kuwa wakulima sasa wanaanza kuzoea na kuona mbolea ya ndani inaweza ikafanya vizuri zaidi kuliko ya kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia muda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Exaud. Nilimtaja Mheshimiwa Thomas Maganga na Mheshimiwa Neema Mwandabila ajiandae.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante na nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa rehema na kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja ya Wizara ya Kilimo. Nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Daniel Chongolo, kwa kazi nzuri anayoifanya. Nami nimtakie kila la kheri, Mwenyezi Mungu amsaidie atimize majukumu yake; na sisi wakulima tuna matarajio makubwa sana na yeye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri sana. Mheshimiwa Waziri akitaka kumsaidia mkulima wa Tanzania ni lazima achukue hatua za makusudi kuwezesha kuwekeza nguvu kubwa kwenye kilimo cha umwagiliaji. Nimpongeze sana kwa hatua anazozichukua na nimpongeze sana, kwenye Jimbo langu la Katavi pale nina mabwawa matatu. Nina Bwawa la Ipati, Bwawa la Irunde na Bwawa la Ipwaga Masigo; yote haya wamekwishakuja

wataalam, wameyafanyia stadi na wamejiridhisha kuwa yanaweza kutoa matokeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, kwamba hakuna namna anayoweza kuisaidia nchi hii kwenye sekta ya kilimo kwenye *angle* ya kilimo bila kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji. Mabadiliko ya tabia ya nchi yanabadilika kila kukicha. Tutoke kwenye hatua ya kusubiri kilimo cha mvua za masika na vuli twende kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, mwaka wa 60 nchi nyingi ambazo tulikuwa tunalingana nazo uchumi ikiwemo China na Vietnam wamepiga hatua kubwa kwenye *angle* ya kilimo kwa sababu waliwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Jimbo la Katavi tunalima sana tumbaku. Kwenye zao la tumbaku tumeingia kwenye kilimo cha mkataba *(contract farms),* linafanya vizuri sana. Na kwenye kilimo cha mkataba Mheshimiwa Waziri limeitoa zao la tumbaku kule likokuwa mpaka sasa Jimbo la Katavi ni wazalishaji wakubwa wa zao la tumbaku kwa sababu ya kilimo cha mkataba, lakini ukiangalia *(contract farm),* kilimo cha mkataba hakina sheria. Imefika wakati sasa Wizara kuja na mkakati mahsusi wa kuleta mabadiliko ya Sheria ya Kilimo cha Mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, kuliko sasa tulivyo, wakulima wanalima na wanaingia mikataba ya hiari; mikataba ya hiari ni *very risk* kwenye maisha ya mkulima; nimwombe sana kaka yangu Mheshimiwa Chongolo, kilimo cha mkataba lazima uingie kwa makusudi kuwekeza kwenye upande wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kwa sababu muda ni mfupi, nimwombe Mheshimiwa Waziri, tunayo taasisi yetu ya *COPRA* inafanya kazi vizuri sana; lakini changamoto waliyonayo *COPRA* watumishi wachache na taasisi ni changa. Hii taasisi iongezewe bajeti. Ushauri wangu kwa dada yangu Irene; anafanya kazi vizuri

sana, lazima na yeye sasa utoke nje ya boksi aingie kwenye kuwahamasisha wakulima kwenye kilimo cha mkataba. Yaani lazima atoke kuhamasisha kilimo, asiwe sasa amekaa anasubiri wakulima wanalima kazi yake ni kukusanya ushuru. Atoke, atoke akahakikishe anawahamasisha wakulima waingie kwenye kilimo cha mkataba. Hii ni kwa sababu ni kilimo cha mkataba pekee yake ndicho kinachoweza kumkomboa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la pamba lilikufa sababu ya kilimo cha buyaga buyaga. Sasa kilimo cha mkataba katika nchi hii ndicho kitakachokwenda kumkomboa mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa nne ni kuhusu kilimo cha bangi. Umefika wakati Taasisi yetu ya *TARI* itoke nje ya boksi ikafanye utafiti wa kilimo cha bangi kwa ajili ya huduma za kitabibu. Si haya wanayowatazama na wanayofikiri kwenye watu wengine. Nchi nyingine kama Uholanzi, Venezuela, Mauritius, wanatumia kilimo cha bangi kwa ajili ya shughuli za kitabibu. Sasa hapo ukiongea kilimo cha bangi watu wote wanawaza *negative* hawaendi *positive*, hatuwezi kutoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARI* wasijifungie ndani, watoke nje watwambie; kama kweli tafiti zinaonesha hiki kilimo kinaweza kutusaidia kwa ajili ya huduma za kitabibu kuna shida gani kuleta sheria hapa?...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Thomas Maganga.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Neema Mwandabila na Mheshimiwa Patali Shida Patali ajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika wizara hii yetu pendwa, Wizara ya Kilimo. Niseme tu, mimi ni mmoja ambao

wanaamini katika suala la kilimo. Kwa kweli ninaamini kwamba kama kilimo kitapewa kipaumbele, ni kitu ambacho kinaweza kikawasaidia Watanzania wengi katika kuinua maisha yao. Ukweli ni kwamba bado hali ya Watanzania si nzuri kiuchumi, hasa wale wanaohusika na masuala ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mdogo sana ningependa kujielekeza moja kwa moja kwenye mchango. Niendelee kuipongeza Wizara na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo wanaendelea kupambana kuona kilimo kinaendelea kuwa ni kitu cha msaada kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitataka niongelee kwenye jambo la mbolea, Mfuko wa Pembejeo kwa ujumla na masuala ya *AMCOS*, Vyama vya Ushirika hivi, *SACCOSS*, *AMCOS*. Ninataka nianze na Mfuko wa Pembejeo ili dakika zitakapokwisha niwe nimeshaongea kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia Taarifa ya Mheshimiwa Waziri hapa, wanaonesha kwamba wataupatia Mfuko wa Pembejeo shilingi 5,000,000,000 ili uweze kuwafikia wananchi wa chini waweze kupata mikopo yenye riba nafuu. Nikaenda mbele tena nikaona wanasema kupitia huo Mfuko wa Pembejeo kuna dola milioni 35, ambapo nilipofanya *calculation* nikapata shilingi 91,000,000,000 ambayo itaenda kwenye taasisi za kifedha ili waweze kukopeshwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikashuka chini zaidi nikakuta kipengele kingine, wanasema wataweza kuwapatia wananchi bilioni 21.47 kwa ajili ya mikopo ya riba nafuu kupitia *Mkulima Nafuu Loan* na *Mkulima Loan* na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu yangu, kwa sababu huu Mfuko tumeanza kuusikia siku nyingi, tumekuwa tukienda kuwahamasisha wananchi wetu, kwamba Wizarani kuna Mfuko wa Pembejeo ambao unatoa mikopo kwa wananchi; hawajaweza kupata fedha katika maeneo yetu. Wanatuhakikishia vipi kwamba fedha hizi zitaenda kwa wananchi? Kwa sababu fedha iliyokuwa imetengwa kwa mwaka

wa fedha uliopita tulisikia hapa, wametuambia imeenda kwenye Benki ya Ushirika, bilioni tano *out of* bilioni tano point mbili, kama nina kumbukumbu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninataka kusema nini? Ni kwamba huu Mfuko mimi kama Mheshimiwa Mbunge wa Wanawake, Mkoa wa Songwe sina imani nao. Ninasema haya nikiwa na ujasiri kwa sababu nimeenda kule Wizarani, nimefuatilia, nimehamasisha wananchi wangu na hakuna hata mmoja mpaka saa hizi aliyepata fedha. Hata tulipokuja hapa ilionesha kuwa ni watu 49 tu katika nchi hii ndiyo walioweza kupata hiyo fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo huu Mfuko tunaomba kama kweli upo na unafanya kazi tuuone kwenye maeneo yetu kwamba unawasaidia wananchi wetu. Pia na hiyo Benki ya Ushirika watafute fedha za kuipa hiyo Benki ya Ushirika, siyo hizi fedha wanazotutengea sisi wananchi ndiyo waende kuzipa hizo Benki za Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ninachotaka kuongelea ni suala la mbolea. Ukweli ni kwamba mbolea ilikuja, lakini pia kumekuwa na uhuni mwingi kwenye mbolea. Ninayasema haya kwa sababu tumeona tukienda kwenye vikao kule chini wananchi wanatuambia mbolea imefika, lakini unakuta bei inayotajwa ya ruzuku huku ni tofauti na wanayouziwa wananchi. Kwa hiyo tuombe Wizara iongeze usimamizi wa hizi mbolea za ruzuku wanazozipeleka kule chini ili wananchi wapate kwa bei ambayo imelengwa. Hilo nisiongee sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka pia niongelee suala la *AMCOS* na *SACCOSS*. Hasa zaidi *AMCOS* ambao alikuwa anaongea kaka yangu hapa, Mheshimiwa Enosy Swalle. Amesema vyama vya ushirika vina wizi mkubwa. Hata wakisikia Mheshimiwa Mbunge anaongea wanamkasirikia, hawataki kusikia kwamba wao wanafanya uwizi wa kuwaibia wananchi wetu fedha. Alikuwepo hapa kaka yangu Mheshimiwa Mwenisongole, ilikuwa ni ajenda yake ya msingi humu ndani. Walikuwa wanamkamia, wanampania kwamba hatarudi Bungeni kisa tu

ameongelea kwa habari ya mambo wanayoyafanya kwenye *AMCOS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunamwomba Mheshimiwa Waziri, kaka yetu Chongolo, Mheshimiwa Naibu Waziri, kaka yangu Silinde na Katibu Mkuu na timu yake kipengele hiki cha *AMCOS* wakisimamie vizuri wizi upungue huko chini. Wanaoumizwa ni Watanzania wenzetu ambao hiyo ingekuwa ni fursa ya kwao kutengeneza maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zimeingizwa na *AMCOS* kweli ni nyingi, hii shilingi trilioni ngapi iliyotajwa hapa ni fedha nyingi sana. Nimesoma hapa, mwaka huu imechangia trilioni 3.74. Ninavyofahamu mimi, utitiri wa vyama vya ushirika hivi ambavyo viko hapa, si kweli kwamba vyote vinafanya kazi kwa ukubwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapoenda kuvihamasisha viweze kukua watusaidie, waje na mkakati ambao vyama vyote vikue kusiwe na vile vyama wanavyovithamini tu vile vikubwa ambavyo tayari vimeshavijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Patali Shida Patali na Mheshimiwa Florent Kyombo atamalizia.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishukuru kwa nafasi hii uliyonipa. Mchango wangu kimsingi ninaomba ujikite kwenye maeneo, hasa eneo kubwa la mbolea. Ninaomba nifikishe salamu za Wanambeya Vijijini kwa kuwasemea maeneo mawili kwa haraka. Kwanza ni kuhusu pareto. Mbeya Vijijini ni moja ya wilaya ambayo inaongoza kwa kilimo cha pareto nchini, kwa mujibu wa taarifa za Bodi ya Pareto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kuna jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kwa ajili ya kuboresha biashara ya zao hili. Hivi karibuni na kwa kupitia Taarifa

iliyowasilishwa, kuna mpango wa ujenzi wa haya makaushio 150 na sisi Mbeya vijijini tunayo 40. Tuiombe Serikali ituharakishie ujenzi huu wa haya makaushio kwa ajili ya kuboresha hili zao la pareto Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie bei; moja ya changamoto kubwa kwenye zao hili la pareto ni kuwa na vishoka wengi ambao wanadidimiza jitihada za makusudi za wakulima. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Chongolo wawaangazie macho hawa vishoka ambao wanaingilia kati kwenye hizi bei za hili zao la pareto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie mazao. Jimbo la Mbeya Vijijini tunazalisha zaidi ya tani laki sita za mazao ya chakula lakini mahitaji yetu ni takribani tani laki moja na tisini hadi laki mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia katika Bunge hili, tusipoliangalia vyema hili suala la masoko nchini, tunaenda kuzalisha mazao mengi na tukakosa masoko kwa kwenda kuyauza. Cha kwanza, ninaomba nisisitize kuboresha masoko ya ndani, ikiwa ni pamoja na kujenga masoko kwenye kila wilaya ambazo zinaongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukawaza hizi tani 400,000 sisi Mbeya Vijijini ambazo tunazalisha ziada ya chakula dhidi ya mahitaji yetu tutazipeleka wapi endapo hatutaboresha au kuchukua hatua za makusudi kujenga masoko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ninatamani kujikita ni suala la mbolea; na hapa ninaomba nichangie haraka haraka kwa sababu ya muda mfupi. Nchi yetu hii inakadiriwa ifikapo mwaka 2030 tutakuwa na takribani ya wastani ya watu wasiopungua milioni 77.55. Watu hawa wote wanahitaji ardhi kwa ajili ya kilimo ili kuelekea ule uchumi wa dola trilioni moja ifikapo mwaka 2050 kama Dira yetu ya Taifa inavyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kilimo chetu kiwe na tija ni lazima tuangalie uwezekano na kuchukua jitihada za makusudi katika kuimarisha upatikanaji wa mbolea nchini. Hali ilivyo sasa, tunapata mbolea ya ruzuku na hapa ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais; lakini bado kuna changamoto ya kuchelewesha mbolea na pia kuingiliwa na walanguzi wanaoficha mbolea. Wakati mwingine zinaadimika sokoni na kuwalazimisha wakulima wazitafute kwa njia nyingine. Ni kwa sababu mkulima anakosa *option,* kwa hiyo inabidi awatafute walanguzi. Niiombe Wizara ya Kilimo kupitia *TFRA*, ninatambua wanafanya kazi nzuri sana, lakini waboreshe eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ili kutatua hii adha ni kuhakikisha viwanda vyetu vya ndani tunavipa nguvu katika maana ya uwekezaji. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema tuna takribani viwanda 48 vya uzalishaji wa mbolea, lakini viwanda viwili tu; *INTRACOM* na Minjingu ndivyo *at least* vinazalisha, vinabeba viwanda vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kwa kumalizia, tutafute uwezekano wa kuwekeza kwenye viwanda hivi ili kuongeza tija ya upatikanaji wa mbolea na kuwarahisishia wakulima ili kupata mbolea na kilimo ambacho wanalima kiwe na tija na cha uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Patali. Tunamalizia na Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kwa nafasi kabisa, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mageuzi makubwa ndani ya sekta hii. Tunaona *BBT* zimeanza na afua nyingine ambazo zinaendelea ndani ya Wizara ya Kilimo. Kwa nafasi ya pekee ninampongeza sana Mheshimiwa Daniel Chongolo na msaidizi wake ambaye ni Mheshimiwa David Silinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema haya maneno machache, kwamba Mheshimiwa Chongolo hayuko pale kwa bahati mbaya. Ukiangalia katika maneno Matakatifu Daniel alikuwa ni nani? Alikuwa ni mtu anayetafsiri maono ya Mfalme Nebukadreza na yeye Mheshimiwa Rais amemweka hapa akatafsiri maono yake ndani ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakumwacha peke yake, akamwongezea Mheshimiwa David, ambaye ni Daudi. Daudi alikuwa kijana mdogo, kwa kombeo na jiwe aliweza kumuua Goriati na maisha yakaendelea. Kwa hiyo, tunamwomba atafsiri ndoto za Mheshimiwa Rais katika kilimo. Mtume Daudi, huyo David aende kule chini kuhakikisha kwamba maono ya Mheshimiwa Rais yanaweza kufika. Hiyo *collabo (Collaborate)* ya watu wawili Daudi na Daniel ukiunganisha na Mtendaji Mkuu wa Wizara ndugu yangu makini sana Gerard Mweli, ninaamini wataenda mbele na Makatibu Wakuu wawili pamoja na viongozi wengine ndani ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika maeneo manne. Eneo la kwanza ni kuhusiana na masoko ya mazao, lakini eneo la pili katika eneo la kimkakati la kilimo cha umwagiliaji la Bonde la Mto Ngono na eneo la tatu ni maboresho ya vibali ndani ya *COPRA* na mwisho nitashauri katika maendeleo ya Tume ya Ushirika. Katika masoko ninaendelea kupongeza juhudi za Mheshimiwa Rais, ameendelea kujenga masoko katika maeneo mbalimbali ndani ya nchi. Hapa sasa tunaona masoko matano yanaendelea kujengwa katika Halmashauri za Ngara, za Tarime, Kyerwa pamoja na Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni shahidi, wanaendelea kubainisha kujenga masoko ya mazao katika maeneo ya Rusumo, Namanga pamoja na Kasumulu na Holili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Chongolo amekuwa Mtendaji wa Chama, hivyo anaijua nchi hii vizuri. Eneo la Mutukula ndani ya Wilaya ya Misenyi ni eneo linalofanya kazi kubwa ya biashara ya mazao nje ya nchi. Ukiangalia katika takwimu Mwaka wa Fedha 2023/2024, zaidi ya tani 300 zimeuzwa

pale, mwaka uliopita tani 50,000. Nimwombe Mheshimiwa kwa ajili ya Wanamisenyi, aweke mazingira mazuri ya ushindani ndani ya Wilaya ya Misenye eneo la Mtukura. Nimwombe akija kuhitimisha atuambie ni lini anaenda kujenga soko la mazao ndani ya eneo la Mutukula ili tuweze kufanya biashara shindani na wenzetu wa Nchi ya Uganda na maono ya Mheshimiwa Rais yaweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu eneo la kimkakati la Bonde la Mto Ngono. Tunajua Bonde la Mto Ngono, Mheshimiwa Waziri wamekwishaliainisha, lina hekta 16,000, linajumuisha wilaya tatu ndani ya Mkoa wa Kagera, *is a game changer* ya uchumi wa Mkoa wa Kagera; na Wilaya ya Misenyi tunaona katika eneo la Nkenge, Buchurago, Buturage, pamoja na Burembo ni maeneo yote. Ukienda Wilaya ya Muleba yapo maeneo saba, ukienda eneo la Bukoba Vijijini yako maeneo saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amesimamia upembuzi umekamilika, usanifu umekamilika, wakandarasi wamepatikana, leo majadiliano ya kusaini mkataba yamechukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Daniel mtafsiri ndoto na maono ya Mheshimiwa Rais, ninamwomba aje kuhitimisha kutuambia je, ni lini mikataba hiyo inaenda kusainiwa ili Bonde la Mto Ngono tuweze kupata mazao na iwe *game changer* ya uchumi ndani ya mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, *COPRA* inafanya kazi vizuri, inatoa vibali. Ombi langu, kwa ajili ya Wanamisenyi na wananchi wengine ambao wanapata vibali vya mazao; tunatoa kibali cha tani 100 tu ilhali pembeni mtu anao mzigo wa tani 1,000, anazo tani 500. Niombe kiwango hicho kiongezwe. Vijana wanakuwa wamekwishapata mazao, yako pembeni wanasubiri kibali kimoja. Kwa hiyo akitoa kibali cha tani 1,000 au tani 2,000 inampa nafasi mfanyabiashara kufanya vizuri na kuondoa gharama zingine ambazo anaweza akazipata kwa sababu ya usafirishaji. Kwa hiyo niombe idadi ya vibali tani ziongezeke; lakini na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba mfumo upo unafanya vizuri na taasisi yetu inafanya kazi vizuri, niombe Mheshimiwa Waziri, asimamie vizuri kazi inayoendelea ndani ya *COPRA* muda wa kuidhinisha vibali angalau masaa machache kama mtu ame-*comply* vigezo vyote apewe kibali aendelee na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwisho ni katika Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania. Mheshimiwa Rais amefanya kazi katika Tume hii, imekuwa na maendeleo makubwa. Tunaona leo Benki ya Taifa ya Ushirika imeanzishwa, tunaona viwanda vilivyokuwa vimekufa sasa vimefufuliwa, tunaona kumeanza kuwa na mfumo ndani ya Tume ya Ushirika ambao umeunganishwa na mifumo mingine. Kazi nzuri inafanyika. Tunaomba Wizara iunge mkono, kuisaidia kwa sababu mambo yanayotekelezwa ndani ya tume hiyo mengine katika vyama vya ushirika hawaungani nayo kwa sababu ya maslahi. Tuwape nguvu waweze kusimama na kutekeleza maono ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo bima ambayo imeanzishwa kwa ajili ya wakulima. Mkulima akilima iwe ni mafuriko, iwe ni mvua ya mawe, iwe ni upepo, mkulima anakuwa-*compensated* kwa ajili ya mazao yake. Vilevile tunaona wameleta mizani mizuri ya kupima mazao ya mkulima ya *electronic*, mkulima hapunjwi mazao yake; lakini hayo mambo yana vipingamizi kule kwenye vyama vya ushirika. Tume wapewe nguvu ili iweze kusimama vizuri na kuhakikisha kwamba maono ya Mheshimiwa Rais yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua nimevumiliwa, ninashukuru. Kwa maono ya Mheshimiwa Rais ya Daniel na Daudi ninaomba wakafanye kazi ili tuhakikishe kwamba Wizara yetu inaendelea kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Florent Kyombo. Huyo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo. Niwapongeze sana kwa kuwajibika ipasavyo pande zote mbili. Waheshimiwa Mawaziri wako makini wanasikiliza. Niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote waliotumia dakika tano kutoa hoja zao kwa Mheshimiwa Waziri.

Hii inaonesha kwamba Waheshimiwa Wabunge wana uwezo wa kutoa mawazo yao kwa muda mfupi na yakaeleweka na yakawafikia wananchi wetu. Kwa hiyo ninaamini hii itaendelea ili Waheshimiwa Wabunge wengi waweze kupata fursa ya kuchangia; kwa sababu leo tulikuwa na wachangiaji wengi; na ninaamini kwamba ingefika jioni tungeweza kuhitimisha hoja bila kuwamaliza Waheshimiwa Wabunge. Kwa mwendo huu wa leo Waheshimiwa Wabunge wote watapata fursa ya kuongea.

Kuna jambo moja ambalo kama sitalisema ninaweza kuumwa na kichwa. Waheshimiwa Wabunge Taifa letu ni miongoni mwa mataifa machache ambayo yanathamini na kujali afya za wananchi wetu; na ndiyo maana kukawa na sheria ambazo zinadhibiti baadhi ya mazao ambayo yanazalishwa hapa nchini. Kwa mfano bangi na mirungi. Hata hivyo, endapo Serikali itakuwa na utaalam wa kutosha na kujiridhisha kwamba matumizi ya mimea hiyo kwa kiwango kinaweza kuwa ni tiba kwa namna ambayo itaona inafaa, sina pingamizi na hilo, lakini kwa minajili ya matumizi na kuwanufaisha baadhi ya wafanyabiashara ambao ndiyo wanufaika, hilo kwa kweli Taifa letu letu halitoweza kufanya; na ndiyo maana tukawa na sheria hizo. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge katika michango yetu mizuri sana tuangalie na tuwe makini katika kuona kwamba mazao ambayo yanaweza kuleta madhara kwa wananchi wetu tusiwe tunashauri sana. Ninaomba sana hilo tulizingatie kwa mujibu wa Sheria za Nchi yetu.

Mwisho kabisa kwa sababu jioni tutakuwa na wachangiaji ninaomba niwataje wachangiaji wachache. Kutakuwa na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew, Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, Mheshimiwa Nassir Ali, Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara.

Kabla sijamaliza tuna wageni ambao tumekuwa nao mpaka kipindi hiki, ninaomba nao tuwatambue.

Kuna wageni waliopo Bungeni ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete ambaye ni Mbunge, ni viongozi wa Jumuiya ya Wazazi kutoka Mkoa wa Mara na Morogoro. Karibuni sana viongozi wetu wa Jumuiya ya Wazazi kutoka Mara na Morogoro. *(Makofi)*

Tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wageni 19 ambao ni familia ya Ndugu Christopher Maganga kutoka Miyuji, Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafamilia wetu wa ndugu Christopher. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 39 na walimu wawili kutoka Chuo cha *SAUT* Kampasi ya Arusha. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Arusha. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, pia tuna tangazo moja kutoka kwa Katibu wa Wabunge wote wa CCM, anaomba tuwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CCM kuwa kesho saa 7.00 Mchana mara baada ya kusitishwa Shughuli za Bunge kutakuwa na *Party Caucus* katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete. Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama Cha Mapinduzi, mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Baada ya kusema hayo, ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 Jioni.

*(Saa 7.03 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano, tunaanza na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew atafuatiwa na Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo na Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali ajiandae.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuongea Bungeni hapa naomba nianze kumshukuru Mungu kwa nafasi aliyonipa, baraka na kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru Chama changu Cha Mapinduzi kikiongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniteua kuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tabora ninayetokana na wanawake wa UWT. Ninawashukuru sana akina mama wa Mkoa wa Tabora kwa kunichagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja niende kwenye Hotuba ya Wizara ya Kilimo, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha vizuri. Pia, nimpongeze Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri wanazofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Tabora kwa 80% tunategemea kilimo, kilimo ndiyo uti wa mgongo na uchumi wetu unatokana na kilimo kwa asilimia kubwa sana. Hivyo, uchumi wetu upo ndani ya Wizara ya Kilimo, hivyo niombe Wizara na nimwombe Waziri aweze kutuangalia wanamkoa wa Tabora kwa jicho la tatu kwa kuweza kutusaidia kupandisha uchumi wetu kuwa wa kiwango kikubwa kutokana na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna zao la korosho ambalo Serikali ilileta ambalo lilikuwa ni zao jipya kwa wananchi wa Mkoa wa Tabora na wakulima wakalipokea na wakaanza kufanyia kazi lakini bado tuna changamoto katika zao hilo. Changamoto ya kwanza ni masoko, masoko yamekuwa ni changamoto sana. Lakini vilevile viuatilifu vinavyotolewa na Bodi ya Korosho kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, wakulima wa zao la korosho Mkoani Tabora walilima eka 14,632 lakini viuatilifu vilivyotolewa ni vya eka 1,438, sawasawa na 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaona kabisa bado mkulima huyu wa korosho hajasaidiwa ikiwa ni zao ambalo la kibiashara na wakulima wameona waliangalie kama mbadala wa tumbaku. Niombe sana Wizara na nimwombe sana Mheshimiwa Waziri awasaidie sana wananchi hawa wa Mkoa wa Tabora waliowekeza kwenye zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nihamie pia kwenye zao la tumbaku. Wananchi wa Tabora tunategemea sana tumbaku kwa asilimia kubwa na tumbaku kwa mwaka huu, msimu huu, bei imekuwa imeshuka sana. Msimu uliopo sasa wa Serengeti mkulima analipwa dola 1.45, lakini gharama za uzalishaji kwa kilo ni dola 1.85 unaona kabisa mkulima huyu amefanya kilimo hiki kwa hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo kilimo hiki ni kigumu sana na wananchi wa Tabora tunagemea uchumi ina maana wakulima wanapopata ndipo wafanyabiashara wengine hawa wanaweza kupata mzunguko wa mahitaji yao. Kama kilimo kikidondoka moja kwa moja mkoa huu unakuwa umedondoka kiuchumi. Niombe sana Mheshimiwa Waziri atuangalie, sisi wananchi wa Tabora kwa ajili ya kupandisha uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe vilevile Wizara kusimamia ahadi zilizowekwa na viongozi wetu wakubwa wa kitaifa. Kwa mfano, Mheshimiwa Rais alipokuwa akinadi Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi aliahidi viwanda. Tunaomba viwanda hivyo vitano

ambavyo vimeahidiwa na Mheshimiwa Rais wakati wa kuomba kura, basi viwanda hivyo vitekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kiwanda cha kuchakata tumbaku kiweze kupatikana kwa sababu maeneo yameshatengwa, wananchi wameshayaandaa Ilolangulu ambapo ni Uyui na Ifucha ambapo ni Tabora. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri tupate kwa uharaka kiwanda cha mbolea. Tunaomba Kiwanda cha Pamba Igunga, tunaomba kiwanda cha nyuzi ambazo pesa zake tayari zimeshatengwa, ni suala la uamuzi tu wa Serikali kuanzisha kazi hiyo kwa uharaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala zima la kilimo chenye tija kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Tunapongeza sana Serikali na Wizara kwa kutusaidia, Urambo tumepata Bwawa Kalemela A limeshakamilika, lakini bado Mkoa wa Tabora tuna maeneo 47 ambayo yametengwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana…

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia sentensi…

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilimtaja Mheshimiwa Bazilio Kapunda, lakini ninaona wamebadilishana, atazungumza Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, atafuatiwa na Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali na Mheshimiwa Morris Joseph Makoi ajiandae.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hii Wizara ya Kilimo. Kwanza nianze na kumshukuru Mungu Mwenyezi kwa kunipa kibali

cha kuweza kusimama siku ya leo. Niwashukuru na niendelee kuwashukuru sana wananchi wa Kigoma Kaskazini kwa kuniamini na kunipa heshima ya kuwa mwanamke wa kwanza kuongoza Jimbo la Kigoma Kaskazini na sitawaangusha niko hapa kuwapigania maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma Bajeti ya Waziri wa Kilimo. Nichukue fursa hii kuwapongeza kwa namna ambavyo mnafanyakazi lakini wote tunasema kilimo ni uti wa mgongo. Asilimia 65 ya Watanzania wanategemea kilimo na wote tuko hapa Bungeni tumekuzwa na wazazi ambao ni wakulima na pato la Taifa 29.1% linatokana na kilimo, lakini kilimo Tanzania bado kina changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri pamoja na kazi ambayo unaifanya na Naibu wako na ninafurahi katika mpango wenu wa 10/30 ambao wamejipanga kuhakikisha kwamba tunatoka tulipo kilimo kinatusaidia kuboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana, yapo mazingira ambayo kilimo bado ni changamoto. Jambo la kwanza suala zima la zana. 65% ya Watanzania kama nilivyosema ni wakulima, lakini wengi bado wanatumia *primitive way*, hawana vifaa vya kulimia. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe wanawasaidia wakulima. Wakulima wengi wanatumia majembe, wakulima wengi hawana uwezo, wakulima ambao wana uwezo wa kununua trekta au *caterpillar* ni wachache sana labda ni 10% kati ya 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi ukija kama kule Jimboni kwangu Kigoma Kaskazini wengi wanatumia majembe. Wizara iweke miundombinu ya kuwasaidia kama ni mikopo Benki ya Kilimo wawape wakulima mikopo wanunue vifaa vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo wakulima wa Tanzania ni changamoto kwao ni suala zima la masoko. Leo Watanzania wanalima mazao, lakini wengi wao hawajui mazao

wanakwenda kuyauza wapi baada ya kuvuna? Ukiangalia kwa mfano, ndani ya Jimbo la Kigoma Kaskazini kule kwetu Manyovu Kusini watu wanalima sana kahawa na ni moja ya sehemu ambayo kahawa bora inatoka ndani ya Jimbo la Kigoma Kaskazini - Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wakulima ambao wanatumia pesa, wanatumia gharama, maisha ni magumu, lakini wakishavuna hawajui wapi wanakwenda kuuza kahawa yao. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, siku zote ninaamini katika *competition* hata ndani yawezekana ukiwa na mke mmoja yuko peke yake akavimba sana kwa sababu yuko peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanaokuja kununua mazao ya hawa wakulima wa kahawa Kigoma yuko mtu mmoja Chama cha Ushirika cha Kanyovu ndiye anayenunua mazao, hii kahawa ya wakulima wa Kigoma Kaskazini. Maana yake ni kwamba hana *competition* anapokuja kwenye soko atanunua kahawa kwa bei anayoitaka yeye kwa sababu hakuna mtu mwingine anayekuja kununua ile kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atuletee watu wa kuja kununua kahawa yetu. Watuletee watu wa kuja kununua mazao yetu, tusitegemee mtu mmoja. Tutafute watu kutoka nchi mbalimbali, tuna kahawa nzuri sana, lakini mazao mengine kama pamba na parachichi Tanzania tunazalisha *product* ambazo ni *very quality* na *pure*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika nchi za wenzetu unaweza ukashangaa na ninatamani sana tuchukue kilimo kwamba ni *very serious* kwa sababu ndiyo asilimia kubwa ya Watanzania tunategemea. Nimshauri Mheshimiwa Waziri tuwekeze sana katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda Morocco unaambiwa Morocco wana uwezo wa kukaa miaka sita hawajaona mvua, lakini wamepiga hatua katika kilimo kwa sababu wana mabwawa ya umwagiliaji. Kwa nini sisi Tanzania tuna mvua, tuna ardhi yenye rutuba, lakini ukija hapa miaka yote tunazungumza

skimu za umwagiliaji? Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri tuwekeze katika skimu za umwagiliaji, tuna ardhi yenye rutuba, kule Kigoma tuna mabonde, tuwekeze tuweze kulisaidia Taifa na litoke katika umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nizungumzie suala la mbolea…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiza, muda umekwisha, unga mkono hoja tuendelee.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa malizia sentesi ya mwisho…

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Jambo la mwisho, Mheshimiwa Waziri ni suala zima la mbolea hapa watu wanasema mbolea inafika, tusemeni ukweli na Mheshimiwa Waziri afanye *research*, ashuke chini, akutane na wakulima, asitegemee hao watu waliokaa maofisini wampe majibu sahihi, wananchi huko wanalalamika hawapati mbolea kwa wakati…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana.
**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilimtaja Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali, atafuatiwa na Mheshimiwa Morris Joseph Makoi na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara ajiandae.

*(Hapa Mhe. Nassriya Nassir Ali alichangia kupitia mtaalamu wa lugha ya alama)*

**MHE. NASSRIYA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii ya kuchangia kwa mara nyingine tena.

Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia hadi nikapata nafasi ya kusimama hapa na kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake kubwa ambayo ameifanya kwenye nchi yetu na ninaweza kusema ni mwanamke jasiri na mama mwenye maono kwa wananchi wake. Ninaweza kusema ni shuhuda namba moja wa Mheshimiwa Rais na kazi zake ni mwanamke ambaye ni *very strong,* hakuna mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru vilevile Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za kutekeleza masuala mengi yanayohusu watu wenye ulemavu katika hali ya ujumuishaji. Tunapoongelea kilimo tunaongelea pia Dira ya Mwaka 2050. Nilikuwa ninafuatilia vizuri Hotuba na hoja ambayo iko Mezani juu ya Bajeti ya Kilimo na nimefuatilia kwa ukaribu na nimejaribu kuangalia kama kuna mahali nitaona kuhusiana na wanawake na vijana katika ujumuishwaji wa masuala mazima ya kilimo na uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatamani kujua watu wenye ulemavu wamejumuishwa vipi kwenye programu mbalimbali za kilimo ambazo zinaendelea hapa nchini? Kuna huu Mradi unaitwa *BBT,* (Jenga Kesho Bora). Ninatamani sana kuona watu wenye ulemavu wamejumuishwa kikamilifu kuhusiana na huu mradi. Kwa sababu na wenyewe pia ni wakulima na wenyewe ni Watanzania na wenyewe wana nguvu kazi, wana uwezo wa kufanya hayo yote kama watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sioni sababu ya wao kuachwa kwenye programu kama hizi wakati zinaweza kuwainua kiuchumi. Hata hivyo, nina imani sana na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Daniel Chongolo kwa uwezo wake mkubwa na ninaamini kazi yake ni njema katika hii Wizara atakwenda kutujumuisha watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Tanzania kuna watu wenye ulemavu wa kila aina na wapo kila Mkoa na vijana wenye ulemavu wapo wa kila aina na wana uwezo mkubwa, lakini kwa

sababu hawashirikishwi, wanashindwa kuonekana, lakini kama wakihitaji kuwashirikisha kwenye programu kama hizi wanaweza kutumia Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu kwenye Mikoa mbalimbali na Wilayani tuko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, washirikiane nao ili waweze kupata data kamili ya kuwajumuisha ili kupunguza utegemezi wa kuombaomba, wataomba mpaka lini na wakati wana uwezo wa kujikomboa kimaisha. Mfano mzuri tu Mbeya, kuna wakulima wazuri wenye ulemavu wanalima maharage, wanalima mpunga, lakini kwa sababu hawako kwenye programu hizi jumuishi hawawezi kujua ni namna gani wanaweza kufanya kilimo bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa unyenyevu mkubwa kwenye masuala haya ya kilimo na kilimo ni *agenda* ambayo iko duniani siyo tu Tanzania, kilimo ni kila kitu, kilimo ni maisha; kwa hiyo watu wenye ulemavu pia ni Taifa la kesho kama ambavyo vijana wengine ni Taifa la kesho na wenyewe ni Taifa la kesho na kilimo tunaambiwa kuwa ndiyo uti wa mgongo wa Taifa. Sasa kama kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa tunaachaje kuwajumuisha watu wenye ulemavu na wenyewe wakawa sehemu ya kuchangia pato la Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba sisi kama Tanzania tulikuwa moja ya watu walioridhia Mkataba wa Kimataifa wa Watu wenye Ulemavu na unasema wazi namna gani ya kujumuisha watu wenye ulemavu kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo, ninaomba Mungu mwezi Juni niweze kupata nafasi ya kwenda kushiriki kwa mara ya kwanza Serikali yetu itakwenda kutoa ripoti ya utekelezaji wa masuala mbalimbali ya watu wenye ulemavu Geneva kama sikosei. Kwa hiyo, nitakwenda kule kwa kifua mbele kwamba Serikali yangu imefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninatamani kuona miundombinu inarahisishwa kwa watu wenye ulemavu ili waweze kufanya shughuli zao. Kama hapa miundombinu imerahisishwa ndiyo maana ninaweza kuchangia. Kwa hiyo na wao wakiwezeshwa wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa nafasi na sina maneno mengi na ninadhani nimetumia vizuri muda wangu. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Iibariki Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema haya, niwapongeze Wizara nzima na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nassriya Nassir Ali, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Morris Joseph Makoi atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara na Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba ajiandae.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba nikushukuru wewe binafsi, lakini kwa vile ninaongea hapa kwa mara ya kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini, ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nimshukuru pia Makamu wa Rais, lakini na Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha nchi yetu inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na timu yao yote, bila kumsahau Mkurugenzi Mkuu wa *COPRA* na Mkurugenzi wa Wizara ya Kilimo wa Mazao Mchanganyiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu ninalotoka la Moshi Vijijini na Vunjo, kilimo kikubwa ambacho kimesaidia wananchi miaka mingi ni kilimo cha kahawa, lakini katika miaka ya hivi karibuni kilimo kile ni kama kimepewa kisogo na ninaona hata Wizara ya Kilimo na wenyewe kama wamekaa pembeni kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea ninaomba kabisa kwa ruhusa yako nimwombe Waziri wa Kilimo na timu yake ya Wizara watusaidie Wilaya ya Moshi, Jimbo la Moshi Vijijini na Vunjo, waweze kurejea tena kwenye kilimo cha kahawa kwa

sababu ndiyo njia pekee ya kujipatia riziki na kipato kwa wananchi wa Majimbo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa pamoja na kwamba Wizara imetusaidia hivi karibuni kupata miche ya kahawa, ninawaomba waendelee kuongeza nguvu kwa sababu wananchi wale sasa wamekubali kurudi shambani ili wazalishe upya kahawa baada ya kugundua kwamba bei imekuwa kubwa na wamegundua kwamba Mheshimiwa Rais Samia ana nia ya dhati kabisa kuwezesha wakulima wote ambao wana nia ya kuzalisha mazao ya biashara hususan zao la kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojua kule kwetu Kilimanjaro, Chama Kikuu cha *KNCU* ndicho ambacho kilichochea vyama vingi vya msingi na wakulima kujiondoa kwenye kulima kahawa kutokana na madeni mengi ambayo chama kile kimeshindwa kuwalipa vyama vya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba nimepata hakikisho la fedha zinazodaiwa kulipwa, lakini ninataka niweke kumbukumbu sawa kwenye Bunge hili kwamba, Chama Kikuu cha Ushirika *KNCU* wanadaiwa na vyama 40 kutoka Jimbo la Moshi Vijijini na Jimbo la Vunjo jumla ya shilingi milioni 800 na kidogo. Uhakiki uliofanyika karibuni unaonesha kwamba hizo fedha ni za msimu wa 2010/2011- 2012/2013 mpaka karibu 2016 zilikuwa hazijalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza kuona jinsi gani hali hiyo imechochea umaskini, kukata tamaa kwa wakulima na hali nyingine ambayo kwa kweli kumshawishi mtu arudi shambani alime kahawa imekuwa ni ngumu, lakini wananchi wale sasa wapo tayari baada ya kupata hakikisho kwamba fedha zile zitalipwa kupitia Mkurugenzi wa *TCB*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongelee ushirika: ushirika nayo imekuwa ni changamoto kubwa sana katika Wilaya ya Moshi; majimbo mawili Vunjo na Moshi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika wameshindwa kabisa kurekebisha sheria ambayo itawezesha wale ambao wachache wanaotumia fedha za wananchi vibaya waweze kukumbwa na mkono wa sheria. Kwa hiyo, kule Moshi *SACCOS* nyingi ambazo zilikuwa zimeanzishwa na wakulima ama zimefilisika, ama zimefilisiwa na wale viongozi na hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kufanya majumuisho, aniambie na awaambie wananchi wa Moshi Vijijini kupitia Bunge hili ni hatua gani watachukuliwa wale ambao wamekula fedha zao kutoka kwenye baadhi ya Vyama vya Msingi na *SACCOS* ambazo zilikuwepo na ambazo zilikuwa zimeenda vizuri na zilikuwa zinatoa tija kubwa sana kwa wale wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niombe nizungumzie habari ya upatikanaji wa mbolea. Ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mkurugenzi wa… eeh...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makoi.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Tunazungumza Wizara ambayo 80% ya Watanzania wanaitegemea, ni bahati mbaya kwamba muda ni mchache sana, lakini nitaomba nipite kwa harakaharaka baadhi ya maeneo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa Kilimo waliopo kwenye maeneo mbalimbali hasa kwenye kata na wilaya:

wenyewe ni wataalam wa kilimo, lakini wachache ambao hata wana mashamba darasa. Shughuli ambazo wanafanya haziendani na kazi ambazo wanafanya, watu wetu wanashindwa kujifunza. Ukimwita Afisa Kilimo aende kwenye shamba unakuta mkulima ni mtaalam kuliko Afisa Kilimo. Inabidi jambo hili Mheshimiwa Waziri alione, watu wafanane na kazi ambayo wanafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule mbalimbali za msingi na sekondari, kuna maeneo ya mashamba ya shule. Mashamba haya, ama yanakodishwa na walimu au walimu wanalima vyakula vyao vya biashara, lakini wazazi wanatakiwa wapeleke vyakula shuleni, kwa nini watoto wasilime mashamba yao ya kitaalam halafu wapate chakula hicho badala ya kupelekewa chakula shuleni kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wa vyuo hapa hata *SUA*, wataalam wetu maprofesa wanafundisha kilimo, lakini jioni wao wanaenda kufungua *bar* badala ya kufungua mashamba darasa. Hili nalo pia ni kitu ambacho kina-*discourage* wanafunzi, unamfundisha namna ya kulima vizuri, lakini kazi ambayo walimu wao wanafanya sio hiyo ambayo wanawafundisha darasani.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto, Tarime inalima kahawa, hakuna mnada wa pamoja, mnada upo Bukoba, Mbinga, Mbozi na maeneo mengine. Unamtaka mkulima wa kahawa kutoka Tarime asafirishe kahawa apeleke maeneo niliyoyataja, ni changamoto.  Ninaomba jambo hili liangaliwe. Bei ni ya chini sana, hakuna hata viwanda vidogo vidogo kukoboa kahawai li waweze kuboresha thamani ya zao hilo katika eneo lile, inasababisha watu kung'oa kahawa na kuanza kulima mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahindi yenyewe yanalimwa Tarime soko ni Kenya, hata jimbo langu hakuna gulio, hakuna ghala, hakuna wakala wa pembejeo ni changamoto kubwa. Hili ninaomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie namna ya kulitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Tarime wanalima ndizi, wanalima mihogo, wanalima viazi vitamu, mazao yote yapo

Kenya, sasa hii Mheshimiwa Waziri anisaidie bei ya mazao haya yote ni nzuri Kenya kuliko Tanzania. Maana yake Kenya ukipeleka ni watu binafsi wanaweza wakaamua wakanunua, wakasema watakulipa kesho kutwa na wasikulipe na watu wanadhulumiwa wanapata hasara. Hili pia ninategemea pia nipate msaada kwa kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa sababu ya muda. Hivi ni lini tutaacha kuagiza ngano kutoka nje ni lini? Ni lini tutaacha kuagiza sukari kutoka nje? Ni lini viwanda vya ndani vitatengeneza *juice* kwa matunda yaliyopo Tanzania hapa ili watu wetu waweze kupata soko? Haya ni mambo ya muhimu Mheshimiwa Waziri, akiyafanyia kazi atatusaidia kwa maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni lazima Serikali ifanye utafiti, ipo imani ambayo tumejengewa sana, mwenzangu amesema hapa asubuhi kwamba pale kwangu, mimi ni Mbunge wa Tarime Vijijini lakini ukienda maduka ya Kenya ukiona jani la mgomba maana yake unauza mirungi, hapa Tanzania hairuhusiwi lakini wale wanapata fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kusiwe na udhibiti wa mazao yakalimwa kimkakati na kuwekwe sheria kali ikafanya kazi. Kule kwangu hakuna pembejeo kwa maana ya mbegu, mbolea lakini zao la bangi lenyewe halihitaji mbolea, halihitaji mbegu bora, halihitaji mvua, halihitaji kupalilia. Kilo moja ya mahindi pale ni shilingi 650, kipisi ambacho kinalingana na mkono wangu hapa ni shilingi 2,000 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni nini? Kuna matumizi ya bangi ya kitaalam; ganzi wakati wa operesheni, watu wenye shida ya usingizi, mambo ya saratani na vitu vingine. Unaweza kuelekeza wakalima kwa usimamizi, wazazi wanatuambia wamevuta bangi wengine miaka 90 mpaka 100 hawana madhara. Sasa zao hili kwa sababu ni watu wanapata fedha na maeneo mengine linakubalika ni vizuri Serikali ikafanya utafiti, madhara yakadhibitiwa, lakini tukapata fedha katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ambayo yapo, tumeshaaminishwa, lakini tukifanya mchakato wa kitaalam na kisayansi, tukauze nje. *Cocaine* ni madawa ya kulevya, lakini kiwango kidogo kipo kwenye soda ya kuoga na watu wanakunywa. *Cocaine* ni madawa ukipatikana ni ajabu kubwa duniani kote, lakini kuna watu wanapata fedha kwa njia hii. Kwa hiyo na sisi hizi ni fursa ambazo tunaweza kuzitumia na kutafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri, akitaka Watanzania wakulima wanufaike, ni kutafuta masoko ya mazao ambayo watu wanalima. Kama watu watalima kwa nguvu kubwa kwa jasho halafu mazao hayana soko, tutakuwa hatujawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja ya *Comrade* mpigaji, Mheshimiwa Chongolo na ndugu yangu Mheshimiwa David Silinde. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwita Waitara. Nilimwita Mheshimiwa Juma Mustafa Kawamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Asha Juma Feruz ajiandae.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nichangie bajeti ya Wizara ya Kilimo 2026/2027. Kwanza kabisa ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amejaalia mimi na Wabunge wote jioni hii tumekutana hapa Bungeni. Pili, shukrani zangu za kipekee ninazipeleka kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anazoendelea kufanya kupitia Wizara hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango, kwenye Wizara hii ya Kilimo. Kama jinsi tunavyoona Wizara hii ya Kilimo imeajiri zaidi ya watu 65% Watanzania wa nchi hii. Hata hivyo, inachangia kwenye pato la Taifa zaidi ya 27%, inachangia kwenye Mfuko Mkuu wa pato la Taifa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na faida hizi bado kuna changamoto mbalimbali ambazo zinatakiwa zichukuliwe hatua za haraka kwenye Wizara hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata tukiangalia kwenye Ripoti ya Wizara ya Mwaka 2026 inaonesha ongezeko la mazao yanakuwa kwa asilimia 4.5, hii inatuambia nini? Mazao yanaongezeka lakini bado ongezeko la watu haliendani na mahitaji ya chakula nchini. Hapa tunaona kwamba, bado Wizara haijawekeza kwa wakulima wadogo wadogo kwa sababu ndio uti wa mgongo wa sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaishauri Wizara ijielekeze kwenda kuwekeza tija zaidi kwa wakulima wadogo wadogo hapa nchini, hasa hasa kuweza kuangalia kwenye masuala ya pembejeo, mbegu zenye ruzuku na kuwatafutia masoko wakulima wadogo wadogo, ndiyo watakuwa wameweka tija kubwa kwenye sekta ya kilimo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio haya ya Wizara, lakini ndani ya Jimbo langu la Igalula bado kuna changamoto mbalimbali ambazo zinawakabili wakulima wangu. Ucheleweshaji wa pembejeo kufika kwa wakati kwa wakulima hasa vijijini bado inaonekana ni changamoto kubwa sana, licha ya wakulima kulima kwa bidi, lakini bado pembejeo zinachelewa kufika. Zinafika katikati ya msimu wa kilimo na wakati mwingine zinafika zinakuta wakulima kabisa wamemaliza kulima kilimo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri nini hapa? Serikali ihakikishe tunapata pembejeo kwa wakati ili wakulima waweze kulima vizuri na tuweze kupata tija kwenye sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, tunaona ni jinsi gani sisi kwenye Mkoa wetu wa Tabora ilani imetuelekeza vizuri. Katika miaka hii mitano, ilani imetuelekeza kwamba inatakiwa tukaongeze uzalishaji wa mbegu kutoka tani 80,000 mpaka tani 19,000; inatakiwa

tukaongeze uzalishaji wa mazao ya biashara kutoka tani 200,000 mpaka tani 300,000 lakini na mazao ya chakula kutoka tani 200,000 mpaka tani 500,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote hatuwezi kuyapata bila kuirejea ilani ambayo imetuahidi kwamba Mkoa wa Tabora inatakiwa tupate kiwanda cha mbolea ndani ya miaka hii mitano ili tuweze kuyashuhudia haya. Watu walioandaa ilani wameyaona malengo haya ya miaka mitano kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba sana Wizara iharakishe mchakato wa kupata Kiwanda cha Mbolea katika Mkoa wa Tabora. Kama watakuwa wanakutana na changamoto zozote za kuhusu maeneo, sisi Wabunge tupo, tutakaa na Viongozi wetu wa Mkoa, kuweza kutafuta maeneo ambayo tutaweza kujenga Kiwanda chetu cha Mbolea Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miundombinu ya skimu ya umwagiliziaji. Takwimu zinaonesha kwamba ni chini ya 10% tu, ardhi ambayo inafaa kuwekezwa kwenye umwagiliziaji ndiyo ambayo imetumika nchini. Ninaiomba sana Wizara iendelee kutafuta fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, tuhakikishe skimu za umwagiliziaji tunakwenda kuzikwamua nchi nzima na hii ndiyo italeta maendeleo ya kweli kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spia, kwa sababu Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, sisi Mkoa wa Tabora inatuelekeza kwamba ndani ya miaka hii mitano inatakiwa tukazalishe kutoka ekari 37 za sasa mpaka ekari 150,000. Bila ya kwenda kuzirejea hizi skimu za umwagiliziaji sisi hatutaweza kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara ya Kilimo ihakikishe kwamba Skimu ya Umwagiliziaji ya Bwawa la Goweko inakwenda kujengwa ndani ya miaka hii mitano, lakini Skimu ya Umwagiliaji ya Kata ya Miswaki inakwenda kujengwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** …Skimu ya Umwagiliaji pia ya Kata ya Loya na yenyewe inakwenda kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mazao...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda umekwisha, malizia sentensi ya mwisho.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ninapenda kuishauri Wizara kama tunataka maendeleo ya kweli na mageuzi ya kweli kwenye sekta ya kilimo, sera zetu ziende zikawalenge wakulima wadogo wadogo kwa ajili ya kwenda kuleta mapinduzi makubwa na halisi ya kiuchumi nchini.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Juma Feruz na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii ya wakulima, ambao ndiyo 80% wamenituma hapa Bungeni. Kwa hiyo ninashukuru sana na nimpongeze sana Mheshimiwa Daniel Chongolo, kwa hotuba yake nzuri sana ambayo imezingatia maeneo mengi ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Ludewa wanaiomba sana Serikali iangalie eneo la mbolea, hasa maeneo ya upatikanaji na vilevile gharama. Nitatoa mifano michache hapa wamenipa kazi hiyo, kwa mfano, mbolea aina ya *DAP* ambayo wanaitumia sana kwenye kilimo cha viazi, maarufu sana kwa *kipalila*, ilikuwa inauzwa shilingi 74,000, lakini sasa ni shilingi 85,000. Kuna mbolea aina ya *SA,* wanaitumia sana pia ilikuwa

shilingi 52,000, sasa ni shilingi 70,000.  Ipo pia *CAN* ilikuwa shilingi 62,000 sasa ni shilingi 72,000; na kuna *urea* ilikuwa shilingi 70,000 sasa ni shilingi 78,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi wa Ludewa wanaiomba Serikali ijitahidi kuangalia hii gharama.  Wanatambua kwamba kuna changamoto kubwa kule mashariki ya kati ambapo Serikali inaagiza zaidi ya 90% ya mbolea hapa nchini. Kwa hiyo, wanaomba sana iangalie eneo hili hasa upatikanaji wa mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimu wa mvua nyingi kuna baadhi ya mazao yanaathirika sana na tabia za nchi, kwa mfano kama ukungu. Kwa hiyo, sasa hivi kiangazi wanalima sana kilimo cha umwagiliaji hasa eneo la vitunguu na Serikali iliwaahidi wale wananchi wa Lutemaluchi pale Lubonde, itaenda kuwapelekea Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji, kwa hiyo wanakumbusha. Pale Madilu wananchi wanalima sana *vipalila*, wanahangaika sana wao wenyewe kutafuta vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wanamwomba sana Mheshimiwa Chongolo, wana imani naye sana kwa sababu yeye mwenyewe pia wanamfahamu ni mkulima. Kwa hiyo, wanaomba awatembelee na kuna ahadi ya Serikali pale Mangalanyene kwenye kilimo cha chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze Wabunge wote waliozungumzia zao la chai, kungekuwa na muda wa kutosha ningerudia. Kuna ahadi pale ya Serikali ya mradi wa maji pale kwa ajili ya kumwagilia zao la chai. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iutekeleza mradi huu pamoja na ule Mradi wa Bonde la Masimavalafu. Serikali imeshawekeza pale zaidi ya shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo fedha hii ili isipotee ni budi sasa kwa Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Mradi huu wa Umwagiliaji, Bonde la Masimavalafu. Ni mradi ambao zaidi ya watu elfu sita watanufaika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kuna ardhi kubwa sana pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumzia eneo la mbolea, ninapenda sana kuishauri Serikali kuagiza mbolea 90% katika nchi ni changamoto kubwa sana. Wakati tuna fursa nyingi za kuwa na viwanda hapa hapa nchini. Nitatoa mfano, makaa ya mawe yale yanayopatikana Ludewa kule Mchuchuma, yamefanyiwa utafiti, yameonekana yana ile *Methanol* kwa wingi, yana *Nitrogen* nyingi ambayo wenzetu kule mashariki ya kati wanatumia katika kujenga viwanda vya mbolea. Kwa hiyo na sisi tuna *potential* hiyo ya kujenga viwanda vya mbolea hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuvishirikishe vilevile Vyuo Vikuu vya Kilimo kama Sokoine na vyuo vingine na taasisi mbalimbali za kilimo kufanya tafiti, kwa nini wakulima wetu kuna aina fulani ya mbolea hawapendi sana kuzitumia ili tuone hizo mbolea zinakosa nini ili tuweze kuongeza. Kwa sababu mpaka wafanyabiashara sasa wanalazimika kufumua ile mifuko ya mbolea hizi zetu ambazo wakulima hawajazizoea sana, wanajaza mbolea, yaani wanaweka mbolea kwenye mifuko ya nje, lakini mbolea inayopatikana hapa hapa, wakulima wakinunua wanaenda kuona matokeo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali ilianza kuchukua hatua kwa wale ambao walikuwa wanauza mbolea *fake*, niipongeze sana Serikali katika eneo hilo na niwasihi sana waendelee kuchukua hatua kwa sababu mwananchi akinunua mbegu *fake* au mbolea *fake* anapata hasara kubwa na anakata tamaa kuendelea na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, eneo hili liweze kuangaliwa, tujenge viwanda vyetu vya mbolea na zile ambazo zinazalishwa tayari, tupongeze ili kulinda ajira za ndani na viwanda vya ndani. Tuangalie zile zinapungua kitu gani ili tuweze kushirikiana na wenye viwanda kuboresha ili wakulima waweze kuziamini na kuweza kuzitumia kwenye shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulisemea ni eneo la barabara za maeneo ya kilimo na uzalishaji mkubwa. Kwa hiyo, Wizara hii ya Kilimo pamoja na kushughulika

na mambo ya sera za kilimo na sheria na vitu vingine washirikiane pia na *TARURA* kuboresha barabara za vijijini ambako ni maeneo ya uzalishaji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, muda umenitupa mkono, ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana kwa kupewa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kamonga. Nilimwita Mheshimiwa Asha Juma Feruz, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji ajiandae.

**MHE. ASHA J. FERUZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo. Awali ya yote ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakika mama huyu amefanya mapinduzi makubwa sana katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia fursa hii kuwapongeza Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri wa Kilimo, Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha kuwa tunapata pembejeo, tunapata mbegu na tafiti zinafanyika, utafutaji wa masoko unafanyika, viuatilifu vinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nijielekeze katika mchango wangu leo. Mchango wangu wa kwanza nitauelekeza katika eneo la mikopo ya wanawake na vijana. Ninaomba Wizara hii sasa ichukue hatua za makusudi katika mikopo ya vijana na wanawake kupitia ule Mfuko wa *AGITF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Wizara hii iangalie kwa jicho la kipekee vijana wetu wanaohitimu katika vyuo vikuu ambao wamesomea kozi za kilimo. Kama tunaweza kumpatia kijana huyu mkopo wa elimu ya juu kabla hana hata haya maarifa ya kilimo, basi kijana huyu niombe aangaliwe kwa jicho la tatu pale anapohitimu masomo yake katika *course* za kilimo anapokwenda kuomba mkopo katika Benki ya Kilimo ama taasisi

zinazotoa mikopo hiyo, akopeshwe kupitia cheti chake. Kwa sababu tunaamini kijana huyu amepata maarifa na anaweza kwenda kuya-*implement* na akaleta tija. Kwanza itachochea ajira kwa vijana na pili tutapata uhakika wa wataalam ambao wana-*practice* kile ambacho wamejifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili niuelekeze katika mazao ya *horticulture*. Mazao haya tumekuwa tukipoteza 30% mpaka 40% katika *post-harvest losses*. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara hii iangalie umuhimu mkubwa wa kuandaa *cold rooms* katika maeneo ya *airport* na bandarini. Mkulima au mwekezaji anatumia takriban dola 2,500 katika *shipment* anapokwenda kusafirisha mazao haya. Umuhimu wa *cold room* ni mkubwa, mazao ya mbogamboga na matunda tunapoteza pesa nyingi katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niishauri Serikali yangu tuangalie katika Bandari ya Mtwara, Tanga, Dar es Salaam, tuzifanye bandari hizi kuwa ni sehemu kubwa ya kujenga hizi *cold room* au zile *warehouse* za mazao ili ziweze kufanya usafirishaji mkubwa. Pia, niombe katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, *KIA*, maeneo ya Tabora na Mwanza, tunaweza tukawekeza hizi *cold rooms* na zikatusaidia kuokoa pesa nyingi ambazo tunazipoteza kwa kupitia Bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa tatu katika Wizara hii, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, tunauza mazao mengi yakiwa ghafi. Tuwekeze katika viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ili tuuze *end user products*. Tukifanya hivyo tutakuwa tumeweka wigo mkubwa wa upatikanaji wa ajira kwa vijana, kwa jamii zetu. Hata yule mkulima na yeye ataona tija ya kile anachokilima kwa maana ya kwamba zao limelimwa hapa, limekuwa *processed* hapa, pesa za kigeni tutazipata, tutainua pato la Taifa na uchumi wa wananchi wetu utakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba nitumie fursa hii kuunga mkono bajeti hii iliyoko mezani na niwatakie kila la heri watekelezaji. Hakika haya yote ambayo wametuletea yakitekelezeka vizuri wananchi wetu watafurahia na

kuona kuwa kilimo kwao ni *option* ya kwanza, siyo ya mwisho baada ya kukosa *option* zote. Haya yote ambayo nimeyaongea yaende sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya barabara. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Juma Feruz. Ninamtaja Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Arif Suleiman Premji na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa ninaomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai muda huu tuko mahali hapa. Ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa ajili ya sekta ya kilimo, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, watendaji wote wa sekta ya kilimo, ninaomba niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa jimbo langu ni wakulima wa tumbaku. Zao la tumbaku limeporomoka kwa kiwango kikubwa sana na mwaka huu wananchi walihamasika walilima sana kutokana na miaka miwili ya nyuma kwa sababu walipata fursa kubwa ya mapato makubwa. Mwaka huu wananchi wakakopa, wakalima, matokeo yake pembejeo imekuwa juu, zao limeshuka kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili Waziri ni msikivu, tunaomba watuangalie kwa jicho la tofauti kupitia wananchi kwa sababu wananchi wamekopa, pesa hawana, matokeo yake yatakuwa ni magumu sana katika zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuleta kampuni mbalimbali ambayo ziliongeza mapato makubwa kwenye zao la tumbaku. Sasa zao la tumbaku limeporomoka kupitia hali ya uhalisia wetu wa dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tuishauri Serikali, sasa hivi ni kipindi cha kujenga kiwanda katika maeneo yetu. Kama

kiwanda kikijengwa Tabora, kiwanda cha mbolea haya yote yatapunguza ile kero ambayo iliyotokea mwaka huu. Tunaomba sana kuishauri Serikali tujenge Kiwanda cha Mbolea katika Mkoa wa Tabora. Maana yake Tabora itatulisha Katavi, Kigoma na Shinyanga, wote tutachukulia mbolea Tabora. Tunaiomba sana Serikali ituangalie kwa jicho la tofauti ili wananchi wetu waweze kupata unafuu kidogo kwa ajili ya pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu nina skimu za umwagiliaji. Skimu kama nne zote hazijafanya kazi, wakandarasi hawapo *site* ina maana kuwa hawajalipwa. Ninaomba Skimu ya Usense, Skimu ya Itenka, Ugala pamoja na Uwila. Skimu zote hazina mkandarasi kwa ajili ya uendelezo wa miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwa sababu kilimo cha umwagiliaji ndiyo uti wa mgongo wa Mtanzania. Tukiendeleza kilimo cha umwagiliaji tutapata manufaa makubwa kwa Watanzania. Ninaomba mwaka huu wa fedha wakandarasi warudi *site* ili kilimo hiki cha umwagiliaji kiweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Waziri kwa kusimamia, sasa hivi tunaona uboreshaji wa *AMCOS* zetu pamoja na Benki ya Kilimo inafanya kazi vizuri, inakopesha, wakulima wanafurahi. Hata sisi Benki ya Kilimo ilikuwa haitufikii, lakini sasa hivi Benki ya Kilimo inatufikia. Mheshimiwa Waziri tunaomba tukupongeze sana, lakini uongeze juhudi kwa sababu kilimo ndiyo uti wa mgongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazao yanayolimwa katika Jimbo langu la Nsimbo, pamba ninalima. Ninaona safari hii kidogo zao la pamba lina unafuu kwa bei. Ninaomba nikupongeze Mheshimiwa Waziri wananchi wangu wanaolima pamba watanufaika, lakini bado kuna zao la ufuta bado halijakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao yote hayo ni mazao ya kibiashara wananchi wanalima, tunaomba basi ili waweze kufanikiwa tuwekewe mazingira bora na mazuri kwa ajili ya *AMCOS* zetu ili waweze kufanya kazi vizuri na mafanikio yawe makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishukuru sana ninaomba kwenye zao la tumbaku tuwaangalie wananchi kwa jicho la tofauti kwa sababu wameporomoka. Sasa hivi wamekuwa na wasiwasi kwa sababu hawajui hatima ya mwakani wataingiaje katika kilimo cha tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lupembe. Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano ajiandae.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wizara ya Kilimo hususan Mheshimiwa Rais. Ni siku mbili tu zimepita jimbo la Mtwara vijijini tayari tumeshaanza kupokea *sulphur* na viuatilifu vinaanza kugawiwa kwenye jimbo letu kwa wakulima pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongelea kilimo na kwenye kilimo ardhi inahitajika, maji yanahitajika, mbolea inahitajika, hali ya hewa iwe nzuri, lakini bei ya sokoni pia iwe njema ndiyo inaweza ikaleta tija kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, *factor* mbili, hali ya hewa na bei, vitu hivi havipo kwenye udhibiti mzuri wa Serikali. Ninasema hivyo kwa nini? Hakuna mtu ambaye anaweza aka-*predict* bei ya sokoni, inategemeana na *demand* na *supply* na soko la dunia pia. Pia, hali ya hewa hakuna mtu ambaye anaweza akajua kesho kuna ukame au kuna mafuriko na vitu hivi viwili ndiyo vinapelekea wakati mwingine mkulima anapata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe ushauri na ushauri wangu wa kwanza ni *Crop Revenue Insurance*. Ni bima ya mapato yanayotokana na mavuno ya mazao. Ni lazima tujikite hapo, hiyo ndiyo bima ya kwanza ili kudhibiti kwamba panapotokea na mfumuko au bei haijawa sawa basi mkulima anaweza akalindwa na hiyo bima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna bima nyingine inaitwa *Weather Index Insurance*, ni bima ya mazao kulingana na hali ya hewa. Dunia ya sasa hivi imebadilika na wakulima wengi vitu hivi hawavitambui. Kwa hiyo, nishauri Serikali yetu ijikite sana kwenye kutoa elimu hiyo, lakini pia tuangalie jinsi ya kuweka mifumo imara ya kuwasaidia wakulima hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliyoko madarakani ni ya Chama Cha Mapinduzi na ukiangalia nembo ya Chama Cha Mapinduzi utaona kuna jembe na nyundo. Jembe lile ni wakulima na waasisi wa chama hiki cha kwetu ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ujumbe ambao wakulima wa Mtwara Vijijini wamenituma na ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa nimpatie Mheshimiwa Waziri. Moja, wanasema tozo zilizopo kwenye zao la korosho shilingi 469 zipitiwe tena, ziboreshwe au zirekebishwe kwa kuwa wakati mwingine wanahisi zinapelekea kufanya bei isiwe *stable* au kushuka. Hilo la kwanza. La pili, kwenye uwiano wa pembejeo, wanapewa robo kilo (gramu 250) kwa kila mti mmoja wa korosho na hilo pia wanaomba waboreshewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, kuna sheria ya manunuzi ya 2023 na *PPRA* mara nyingi wanasema kwamba 30% iende kwenye makundi maalum. Vijana wa Mtwara, walemavu wa Mtwara, akina dada zangu wa Mtwara wameniagiza hili na mama zangu na shangazi zangu pia, kwamba inapotokea zile *tender* za ku-*supply sulphur*, magunia na viuatilifu, basi na wenyewe wapewe kipaumbele kwa kuwa sasa hivi tunachoki-*advocate* ni kwamba vijana wajikite, tuwapatie fursa na hiyo ni fursa mojawapo. Kwa hiyo, ninaomba sana hilo tulizingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia wengi wameongea, mimi ninatia msisitizo tu. Sukari, ngano, mafuta ya kupikia; tukichukua hivi vitu vyote ni kuanzia trilioni 2.5 mpaka 3.2 ndio tunaagiza. Kwa hiyo tuliangalie na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya faida ya muda, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii ya kupata dakika tano hizi ambazo nitachangia Wizara yetu ya Kilimo. Kama ambavyo Wabunge wenzangu wamesema mara kadhaa kuhusu umuhimu wa kilimo katika nchi yetu na kadhalika Mkoa wa Morogoro tunasema mara zote ni Ghala la Taifa. Tunaongoza katika nchi yetu katika kilimo cha miwa pamoja na mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kusimama hapa kwa kusema ninaanza na mambo ya kushukuru, lakini nimesimama kwa upole kidogo kutokana na yale mambo ambayo yanaendelea kwa wakulima wetu wa miwa ya sukari, nikipata muda huko nitaelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyosema wenzangu Wabunge, tuna imani kubwa na wewe Mheshimiwa Waziri wetu, Mheshimiwa Godfrey Chongolo kwa sababu wewe ndiyo mtunzi wa ilani na umepewa kazi sasa ya kuisimamia ilani. Kama ningelisema kwa Kindamba, Kipogoro ama Kisukuma basi ningesema: *"A square peg in a square hole is in safe hands."* Kwa hiyo, sisi tupo salama mikononi mwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri anasoma hotuba nimekusikia kwamba Mkoa wa Morogoro tunapata kituo kikubwa cha kibaolojia, tunashukuru sana sana. Tunashukuru sana nimeona kwamba tunapata miradi mikubwa ya umwagiliaji ambao upembuzi yakinifu umekamilika kwa 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mradi wa Umwagiliaji tuliopata wa Ifakara - Idete hekta 53,000 unaofanywa *na SABA Engineering* ambao umekamilika kwa 100% upembuzi yakinifu utakaokuwa unajengwa bwawa la maji na pamoja na skimu. Kuna Bonde la Kilombero hekta 19,000 wanafanya wao *SABA Engineering* umefika 95%, tutakuwa na bwawa pamoja na skimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Mradi wa *Mang'ula Youth Group,* tuna Maki - Magombera, tuna Kisawasawa, Kiberege, Mkangawalo na Signal. Hiyo yote ikikamilika itatusaidia kwa kiasi kikubwa sana kuendelea kuufanya Mkoa wa Morogoro kuendelea kuwa Ghala la Taifa na kupunguza athari kubwa za mafuriko ambazo tunazipata Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru wanafanya pia kilimo cha umwagiliaji katika maeneo ambayo wanakwenda kuchimba visima. Sisi Kilombero maji tunayo yanazidi mpaka yanamwagika kwa wananchi. Hapa ninavyozungumza kuna wananchi zaidi ya 200 wako pale Shule ya Msingi Lipangalala kutokana na mafuriko kuwa katika majumba yao. Sasa endapo tutapata miradi hiyo ya umwagiliaji ambayo inajenga mabwawa kukinga Mto Lumemo itatusaidia sana kupunguza mafuriko kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nilikwenda kukaa hapo kwake na wapiga picha wakapiga picha, nilikuwa na jambo langu nilimpelekea. Kwa heshima kubwa na unyenyekevu mkubwa ninataka kushukuru jambo lile Mheshimiwa Waziri limekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu Mkuu amenipigia simu ameniita hapa; Katibu Mkuu wa Wizara yake na Mkurugenzi wa *TARI* ananiambia ule mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Kata ya Lumemo na *TARI* walikuwa wanatengeneza kituo cha mbegu. Tuna hekta 98 zilikuwa na mgogoro pale zinazuia *TARI* kuendeleza kile kitalu cha mbegu umekamilika. Kwamba watasaidia yale ambayo wananchi walikuwa wanayataka angalau wapate malipo kidogo yasaidie kutafuta ardhi nyingine ili wananchi waachie ardhi ile ya *TARI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya ziara pale wananchi waliongea kwa hasira kubwa sana kwamba viongozi mnakuja hapa mnapiga picha mnatuma kwenye mitandao hamtatulii kero yetu. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa, Katibu Mkuu wake ameshanisaidia suala hili na ameniambia limekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninataka kuzungumzia miwa. Bunge lililopita nilisimama hapa kidete kuomba kiwanda kipya cha sukari kwa sababu miwa ya wananchi ilikuwa inabaki. Sasa kiwanda kipya tumepata, tuna changamoto zinazotokana na hicho kiwanda kipya kuwekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kiwanda hicho kime-*test* miwa ya wakulima lakini wakulima wale hawajalipwa vizuri katika *testing* ya miwa hiyo. Wanasema walipeleka miwa ya majaribio kiwanda kimesimama na ni miwa walipata hasara wanaiomba Serikali iwakumbuke. Wakulima wa miwa wanasema sasa hivi wanang'oa miwa wanapanda mpunga kwa sababu mpunga unalipa zaidi kuliko miwa. Endapo hilo litaachwa kwa vyovyote vile uwekezaji wa shilingi bilioni 700 za kiwanda kipya hautakuwa na mafanikio yoyote ambayo tulikuwa tumeyaomba huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chonde chonde ninaiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ambao wako hapa; ninamwomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara, aende akakutane na wakulima wa miwa wa Kilombero. Sisi tutamwandalia mkutano mzuri azungumze na vyama vile na wakulima wale wasikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo wanazungumza kabla ya sukari kuingizwa nchini ambayo mwekezaji amekuwa ni kisingizio chake, lakini kuna matatizo mengine yametokana na sukari kuingizwa nchini. Wakulima wakati wote wanalalamikia kupunjwa mzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba mamlaka ya mizani iende pale iweke kiti ili wakulima wale wanapouza miwa yao ile *sucrose* (utamu) wasilalamike kwamba wanapunjwa. Wakulima wanasema wameingia mkataba na kiwanda, muwa unaoungua, moto bahati mbaya unavunwa wanakata 10%, lakini Serikali imetoa katazo kwamba miwa inaoungua kwa bahati mbaya inatupwa. Watu wamepata hasara mpaka za shilingi milioni 500 ndiyo huku tunaposema kuna umuhimu wa kuwa na bima ya kilimo na bima ya mazao ili kuwasaidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu dakika ni tano, anisaidie katika Bunge hili kama atapata nafasi aandae ziara nzuri pale, azungumze na wakulima awasikie wenyewe uso kwa uso ili tuweze kuwasaidia wakulima wetu hawa kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Abubakari Asenga. Nilimtaja Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo na Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala ajiandae.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa fursa hii na kwa dhati ya moyo wangu nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema. Nipate fursa pia ya kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi mama Samia Suluhu Hassan. Pia, niipongeze Wizara husika, Wizara ya Kilimo kwa kuwa na hotuba nzuri ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wanabumbuli nianze kuiunga mkono hoja. Baada ya hapo niende moja kwa moja kwenye zao la chai kule Bumbuli. Hili ni zao la kihistoria, zao la kimkakati na zao la kibiashara. Kata 14 kati ya 18 zinategemea zao hili. Hata hivyo, kuna changamoto ambazo ninaziwasilisha moja kwa moja kwa Wizara ya Kilimo kwa sababu wanazijua nyingi, nitataja hizi chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni uwezo mdogo wa kiwanda, kinatumia laini moja mpaka sasahivi, kiasi cha kukatisha tamaa wakulima wa zao la chai. Basi ninaomba iongezeke laini ya pili na ya tatu, ili kuongeza tija katika zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai na madeni; wakati kiwanda hiki kiliposimama, kabla Serikali haijakitwaa yapo madeni; madai ya watumishi zaidi ya shilingi 800,000,000, lakini na wakulima pia, walikuwa na madai yao, shilingi 12,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine kubwa kwa kiwanda hiki ni pembejeo, hasa mbolea. Kwa bahati mbaya kule Bumbuli, wakala ni mmoja tu, ambaye anashindwa kuweza kuwafikia wakulima wa chai, lakini wakulima wanalalamika bei ndogo, shilingi 366 kwa kilo, ni kiwango kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo changamoto pia ya barabara kwa sababu, kata 14 kuziunga katika jimbo ambalo lina milima na mabonde ni changamoto kubwa. Kingine ni ukosefu wa mitaji na uwekezaji wa kutosha. Pia, lipo zao la mkonge katika Kata za Tambarare, Kata za Kwemkomole Milingano, Mahezanguu pamoja na Usambara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa changamoto kubwa ni mbolea na mbegu bora. Wakulima wengi hutumia mbegu ambazo zinachipua pembezoni mwa mashina ambazo siyo bora na hata umri wake ni mdogo. Sasa kwa sababu, kuna ile mbinu ya kisayansi ya *tissue culture* na tunayo *TARI* ya Mlingano, basi ipate maelekezo ili iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaenda kwenye eneo nyeti kidogo, nalo ni kilimo cha umwagiliaji, lakini ninajikita zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji wa skimu ndogo ndogo za mbogamboga. Hii ni lazima kulingana na sayari yetu kukumbwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi. Mvua haitabiriki, lazima tuwe na benki ya maji na haiwezi kupatikana, isipokuwa kwenye mabwawa. Tija gani itapatikana kwenye maji haya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwashauri wenzetu wa kilimo, tufike mahali kuwe kuna *user efficient irrigation* kwa maana kwamba, tutumie mbinu za maji kidogo, ambayo tunaita *drip irrigation.* Hii itapunguza gharama ya umwagiliaji, itapunguza hata changamoto ya magonjwa yanayotokana na unyevu wa maji, lakini pia, itapunguza changamoto zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwashauri kwamba, kilimo kiwe kilimo hifadhi; yaani kilimo ambacho kinatumia *mulching,* kule uswahilini tunaita matandazio, lakini ina-*cover crop* au mimea funiko. Kuwe na uchaguzi wa mazao ambayo

yanaweza yakahimili mabadiliko ya tabianchi kwa sababu, Wizara ya Kilimo ni Wizara ya *research*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima kuwe na usimamizi madhubuti wa zile *water users groups,* zisiposimamiwa vizuri mwisho ni migogoro. Ninakumbuka kesi moja kule Moshi, wakulima na kiwanda cha miwa, ilikuwa ni changamoto kubwa kwa hiyo, lazima wasimamiwe vizuri, lakini ni nini faida ya kilimo hiki cha mbogamboga?

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaboresha lishe. Ikiwa mbogamboga zinapatikana kwa mwaka mzima, maana yake ni tunaenda kuboresha afya ya jamii. Tutapunguza utegemezi wa kutumia mvua. Tukiongeza mavuno na kipato, maana yake tutakuwa na mbogamboga kwa wingi zaidi, lakini pia, tukiwa tunategemea…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. RAMANDANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Wizara ya Kilimo, lakini ninaunga tena mkono hoja. *(Makofi)*

**AIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Edibily Kinyoma na Mheshimiwa Onesmo Mnkondya ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Kilimo kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nafasi hiyo. Ninampongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo, bajeti hii ya kilimo amekuwa akiiongezea fedha kila mwaka hata tumefika katika kiwango hiki kikubwa cha karibu shilingi 1,000,000,000,000. Haya ni mapinduzi makubwa na ukiangalia katika fedha hizo za maendeleo, fedha nyingi zimeenda kwenye suala zima la umwagiliaji kwa hiyo, haya ni mapinduzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ninaomba Wizara ya Fedha iweze kuongeza nguvu ya kutafuta fedha na ku-*finance* miradi hii ambayo Wizara ya Kilimo inaitekeleza ili kuweza kufikia malengo. Vilevile, ninachukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali, katika Wilaya yangu ya Bahi nimepata mradi wa shilingi 5,600,000,000 pale katika Skimu ya Kongogo. Jambo hili ni zuri na mradi ule ni mkubwa. Hoja yangu tu ni kwamba, wenzetu wa umwagiliaji waweke umadhubuti zaidi mradi ule ambao kwa sasa upo karibu 46% uweze kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Chongolo, alipokuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, alifanya ziara pale Bahi, mwaka 2023 na akaelekeza kwamba, Skimu ya Umwagiliaji ya Bahi ikarabatiwe. Ninavyozungumza leo ukarabati wa *scheme* ile umefanyika. Tumepata karibu shilingi 3,600,000,000 na bajeti yake ni shilingi 5,000,000,000, kwa hiyo, ukarabati ule unaendelea. Kwenye hilo ndugu yangu Mheshimiwa Chongolo, ninamshukuru sana, ziara yake ilizaa matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ambacho ninataka kusisitiza ni kwamba, ukarabati huu ambao tumeufanya bado hatujaumalizia, skimu zingine zinaendelea itabidi tukarabati. Bado kuna shida ya miundombinu ya barabara kwenye mashamba na zile skimu, tunaomba Serikali iweze kumalizia kile kiwango kilichobaki, ili tuweze kukamilisha ukarabati huo. Ninaishukuru Serikali imefanya usanifu katika Mabonde ya Mkakatika, Mtitaa na pale Lukali, ninaomba kazi ikamilike ili tuanze sasa kazi ya ujenzi wa skimu, kwenye skimu tatu nilizozitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali, mwezi Machi nilipata janga la kweleakwelea, wale ndege, katika Vijiji vya Mwitikila, pale Lukali, Ibiwa na maeneo ya Tarafa ya Mndemu. Ninaishukuru Serikali imeleta ndege ile ya kupulizia wale ndege, kweleakwelea, imekuja mara mbili. Ilikuja mara ya kwanza kidogo hawakufa, imekuja mara ya pili, kidogo tumepata ahueni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka tu kusema, ninamshukuru Profesa Ndunguru kwamba, tumepata ndege

ambayo Serikali imeinunua kwa hiyo, *accuracy* kubwa iweze kuangaliwa katika dawa zinazopuliziwa, ili wakienda kupulizia tuweze kuhakikisha tunawaangamiza wale ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine niongee habari ya kilimo cha ngano, wenzangu wengi wamesema. Kwa kweli, katika jambo hili Ndugu yangu Mheshimiwa Chongolo, kwenye kilimo kuna mambo mengi, lakini aondoke na suala la ngano. Kila mwaka tunatumia fedha karibu dola za Kimarekani 377,000,000 ambazo ni karibu shilingi 900,000,000,000 au *all most* 1,000,000,000,000, tunaagiza ngano kutoka nje ya nchi. Mashamba tunayo katika maeneo mbalimbali, ninachoomba ni Serikali iweke *incentives* kwa mashine zile kubwa zinazokuja kwenye kilimo cha ngano, ili tuweze kulima ngano yetu hapa nchini na ikiwezekana tuweze kuuza katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili tumefanya kwenye sukari, kwa sasa nchi yetu inajitosheleza kwa kuzalisha sukari ndani ya nchi. Kwa hiyo, jambo hilo tulifanye. Mheshimiwa Waziri, Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuja kwenye kampeni Bahi, tarehe 9/9, aliahidi kwamba, kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, na jambo hilo lipo, kwamba, maji ya Ziwa Victoria yatakuja mpaka Kanda ya Kati, maji ambayo yanakuja kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba ahadi ya jambo hili la kihistoria waweze kulitekeleza, ili tuweze kupata maji, kwa ajili ya umwagiliaji. Mambo haya yataleta mapinduzi makubwa katika Mikoa yetu ya Kanda ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Yusuph Majala, atafuatiwa na Mheshimiwa Edibily Kinyoma na Mheshimiwa Onesmo Mnkondya, ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara yetu ya Kilimo na bila ya kupoteza muda, ninaomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja. Kwanza ninawapongeza Wizara ya Kilimo, kwa maana ya Mheshimiwa Waziri na timu yako yote, lakini hoja yangu ya kwanza ni suala zima la mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Taifa letu tumekuwa hatuna mbegu bora, lakini zinapatikana kwa bei ghali, hususan mbegu ya mahindi, alizeti na zingine. Sisi Mkoa wa Dodoma, alizeti, mahindi, mbaazi na ufuta hizo ndiyo mbegu ambazo tunazitumia kwa wingi. Mbegu hizi zimekuwa ni ghali, lakini nyingi hazimpi tija mkulima. Tumwombe Mheshimiwa Waziri, kupitia taasisi yake ya mbegu, waende wakawasaidie wakulima waweze kupata mbegu iliyo bora na inayopatikana kwa bei rahisi, watakayoweza kuimudu kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuzungumzia zao la alizeti. Mheshimiwa Waziri, nchi yetu imekuwa ikitumia gharama kubwa sana kuagiza mafuta nje. Hili jambo tumekuwa tukilisema na nimekuwa ninasema kila mwaka wa bajeti, sasa ni takribani mwaka wa 11. Tunazungumzia suala la kujiimarisha kwa mbegu za mafuta ndani ya nchi yetu, ili tuweze kuondokana na uagizaji wa mafuta nje ya nchi. Mheshimiwa Waziri tunaomba watusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupate mbegu nzuri itakayoweza kuleta tija kwa wakulima wa alizeti, lakini itakayoweza kuleta tija kwa Taifa kwa kupata mafuta ya kujitosheleza ndani ya Taifa letu. Fedha tutakazozibakisha kwenye kuagiza mafuta nje, zitumike kwenye mambo mengine ndani ya Taifa letu. Ardhi tunayo, watu wapo, nini kinachoshindikana kwenye suala zima la kutupatia mbegu iliyo bora yenye tija kwa wakulima, ili tuweze kuondokana na adha kubwa tunayoipata ya mafuta ndani ya Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu lingine ambalo ninatamani kulisema ni suala zima la Mfuko wa Pembejeo. Mfuko wa Pembejeo upo, kwa ajili ya kuwasaidia wakulima, kwa ajili ya

kuwapatia pembejeo za kilimo pamoja na mikopo, kwa ajili ya kilimo, lakini kuna changamoto moja kwenye Mfuko huu, wameamua kufanya kazi pamoja na Benki yetu ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima anahitaji *power tiler* lenye thamani ya shilingi 15,000,000 anaambiwa apeleke hati ya nyumba ama hati ya shamba. Hati za kimila *coop bank* nao hawazitaki, sasa ninataka watusaidie, uwepo wa Benki ya Ushirika *vs* Mfuko wetu wa Pembejeo…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tujadili kwa sauti ya chini, Mbunge anachangia. Ninaomba tujadili mambo mengine muhimu kwa sauti ya chini.
Mheshimiwa endelea.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Hizo dakika zangu mbili utanijazia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema uwepo wa Benki yetu ya Ushirika *vs* Mfuko wetu wa Pembejeo ambao wameamua kufanya kazi kwa pamoja. Ni kwa nini Benki ya Ushirika inakataa hati za kimila kwenye benki zao, kwa ajili ya wananchi wetu kupata mikopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kwenye suala zima la Mfuko wa Pembejeo. Wamesema wanatoa mikopo ya aina mbalimbali ikiwemo uwezeshwaji wa mbegu, suala la palizi, suala la kilimo na ufyekaji wa mashamba; hivi vitu havifanyiki. Tunaomba, Mheshimiwa Waziri, kama kweli nia na dhamira ya Wizara yake kupitia Mfuko huu wa Pembejeo wa Taifa ni kuwasaidia wakulima wadogo wa kule chini, maneno wanayosema yaendane na vitendo, ili wananchi wetu waweze kuiamini Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu lingine ni suala la Vyama vya Ushirika na Benki yao tena ya Ushirika. Mheshimiwa Waziri, kuna Sheria inayosema kwamba, Chama cha Ushirika kikiundwa kinatakiwa kikae miaka mitatu, ndiyo kikopeshwe. Sasa

ninajaribu kujiuliza, hivi kwenye suala zima la hii Benki ya Ushirika, madhumuni na malengo yake ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *CRDB* na *NMB* wana hayo masharti, leo tena Benki ya Ushirika, ambayo tunategemea hawa wananchi wetu ambao tunawaaambia wajiunge kwenye vyama waweze kupata fursa ya kuwezeshwa kwa urahisi, kunakuwa na hivyo vikwazo! Mheshimiwa Waziri tunaomba, suala la Vyama vyetu vya Ushirika, kama nia na uwepo wa Benki ya Ushirika ni kuwasaidia wanaushirika, tunaomba wasaidiwe bila vikwazo, ili kuwaondolea adha wanayoipata kwenye huduma zingine za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile dakika zangu mbili ulizonituliza, ninaomba nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Malizia Mheshimiwa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Jambo langu lingine ni, suala la stakabadhi ghalani. Ni jambo jema, hatuna shida nalo, lakini ninaomba niseme changamoto kadhaa ambazo wanatakiwa ku-*share* wenzetu wa Kilimo, Wizara ya Viwanda na Wizara ya Fedha, ili waweze kuzitatua na hatimaye mfumo wetu uweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kwenye changamoto ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni uwepo wa maghala machache. Tunahitaji maghala mengi, ili yaweze kuwasaidia wakulima wetu; moja, kupunguza gharama ya usafirishaji wa mazao, lakini pili, kumsaidia mkulima huyu kutopoteza mazao anaposafirisha kwa umbali mrefu. Kwenye hilo tunaomba pia, wakati wanajipanga, watusaidie kuwa na maghala yanayotembea, kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni ulipwaji kwa wakati ili kuweza kuwaondoa wananchi wetu kwenye hizo changamoto. Ninakushukuru kwa muda wako. Ahsante sana na Mungu akubariki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA** Mheshimiwa Edibily Kinyoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Onesmo Mnkondya na Mheshimiwa Amosy William Maganga, ajiandae.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara ya Kilimo. Kwanza ninawapongeza Wizara, nimeona mikakati waliyonayo kwenye kilimo, mikakati hiyo kama wakiitekeleza inaweza ikatutoa hatua moja na hatimaye ku-*boost* uchumi wetu, kwa maana ya *GDP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wetu kwa 60% umeajiri watu kwenye sekta ya kilimo. Sekta hii ya kilimo inachangia zaidi ya 23.3%, kwa mujibu wa *World Bank,* kwenye pato la Taifa letu na pia, zaidi ya 20% kwenye *export*, kwenye mauzo ya nje. Maana yake ni kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache ya kuchangia. Ukiangalia uchumi wetu kwa asilimia 42.9 umejengwa na shughuli za msingi *(Primary activities),* kwa asilimia 19.7 shughuli za upili *(Secondary activities)* na *tertiary activities* kwa asilimia 37. Hii inaashiria nini? Ni kwamba, kilimo ndiyo chenye mchango mkubwa kwenye uchumi wetu. Sasa hii nayo ina athari zake, maana kikitokea chochote kwenye kilimo, uchumi wetu una hatari ya kwenda kuanguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya 1970 uchumi wetu ulianguka kutokana na ukame uliojitokeza kwenye Taifa letu. Kama tunataka kukipeleka kilimo chetu mbali, kujenga uchumi wetu na kuhakikisha kwamba, tunafikia Dira yetu ya 2050 ya kuhakikisha tunafikia pato la shilingi 1,000,000,000,000 lakini pia, dola 7,000 kwa *capital income,* ninashauri tuwekeze kwenye

viwanda vya kuongeza thamani mazao yetu ya kilimo. Tutoke kwenye *stage* ya uchumi wetu kuchangiwa na shughuli za msingi, kuuza mazao ghafi, tuuze mazao ambayo yameongezwa thamani; maana yake ni tujenge viwanda. Viwanda hivi vitatusaidia masoko na vitatuongezea ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu 2002, kwa mujibu wa Wizara ya Viwanda, kulikuwa na viwanda zaidi ya 50 vilivyoanzishwa, lakini vilivyoweza ku-*survive* ni viwanda 23 tu. Tuna viwanda vingi ambavyo vilikufa, viwanda vya *textile*, viwanda vingi vya kutengeneza nguo. Kwa mujibu wa bodi pia, 80% kwenye zao la pamba wanauza nje, maana yake sisi tunazalisha kitu ambacho hatukitumii, ninaishauri Wizara tuwekeze kwenye viwanda ili viende vika-*boost* mazao yetu tunayolima, wananchi wetu wanaolima tuweze kuhakikisha soko lipo la uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona pia kwenye zao la muhogo, Mheshimiwa Waziri anisaidie kiwanda cha kuchakata zao la muhogo pale Kasulu Vijijini, tuna shida ya kiwanda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Onesmo Mkondya, atafuatiwa na Mheshimiwa Amos William Maganga na Mheshimiwa Josephine Kapoma, ajiandae.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi ambayo umenipa ili niweze kuzungumza na Wizara yetu ya Kilimo, ambayo ina Waziri bora kabisa na Naibu Waziri. Ninawapongeza kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwenye Wizara yetu ya Kilimo, ninaweza nikasema ndiyo Wizara pekee ambayo imeajiri watu wengi kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumza kwa niaba ya Wanambozi ambao wamenituma na leo nifikishe ujumbe huu kwenye Wizara yangu muhimu kabisa hii, kwa Jimbo langu la Mbozi peke yake, waliojiajiri kwenye kilimo ni 80%. Maana yake nini, ni kwamba kilimo ndiyo ajira kwa Jimbo langu la Mbozi, tunategemea kilimo kwa asilimia hizo zote ambazo nimezisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, wao walichoniagiza kwenu Mawaziri wangu, mwaka jana walipata shida ya changamoto ya mbolea, wamepata changamoto ya mbegu, wamepata changamoto ya madawa, lakini asilimia kubwa wamepata changamoto ya mbolea aina ya *DAP*. Sasa Mheshimiwa Waziri, tunapomaliza msimu huu wa kilimo, tunaanza msimu mpya mwingine. Tunaelekea kumaliza msimu lakini tunaunganisha msimu kwa jimbo langu, msimu wote tunalima sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mwaka jana changamoto ile kidogo imeleta tafaruku kwa jimbo langu. Wananchi wamelalamika kama nilivyowahi kuuliza swali hapa, wameingia hasara na hakuna mtu wa kuwafidia, ni nani wa kwenda kuwafidia na kwenda kuwaomba kwa msimu huu unaoanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji mbolea iwahi kwa wakati, tunahitaji mbolea ya kupandia iwahi kwa wakati, tunahitaji tena mbolea ambayo ni bora, hakuna mbolea feki. Tunahitaji madawa bora, tunahitaji mbegu bora ili tumlinde mkulima. Ili tumlinde nani, mkulima. Bila kufanya hivyo tunahatarisha uchumi wa Wanambozi, uchumi wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo mbolea zinapokuja tumeruhusu watu kuuza mbolea feki, hatumlindi mkulima, unajiuliza *TFRA* wako wapi, unajiuliza wako wapi walinzi hawa, wasimamizi wa bei, lakini wasimamizi wa ubora wa mbolea wako wapi? Hawapo! Wabunge tunaanza kuhangaika madukani siyo sawa, watu wa *TOSCI* wako wapi kwenye mbegu, watu wa *TIFA* wako wapi kwenye madawa hawasimamii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyozungumza mbolea Jimbo la Mbozi inauzwa shilingi 100,000 hadi shilingi 90,000, hivi ndivyo bei

ya mbolea ya ruzuku ambayo Rais Samia ametupatia ndiyo bei hiyo. Kwa nini wasitoke tamko marufuku kuuza mbolea kwa bei ya juu, twende tuuze mbolea kwa bei elekezi na bei elekezi ipo wazi. Niombe tumlinde mkulima, tuwalinde wakulima wetu, tuwalinde baba zetu, tuwalinde vijana wetu ambao wanakimbilia kujiajiri wanapokuta mbolea shilingi 100,000 watajiajirije? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda ninaomba nishauri lifuatalo: Mwaka jana kwenye huu msimu kampuni ya *TFC* imekuwa mkombozi mkubwa sana, kampuni hii ndiyo kampuni pekee imetuagizia mbolea ya *DAP* tani 50,000 pekee yake, kampuni zote zilinyamaza. Ninaomba wakakae na kampuni hizi nyingine pia, wakazungumze kilimo, wakazungumze biashara wakazungumze maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huohuo hii kampuni, ninaomba nishauri kwa Mheshimiwa Waziri, waendelee kuisimamia na kama kuna ruzuku waliyosambaza mbolea hawajalipwa, walipwe waagize mbolea mapema kwa ajili ya wakulima wa Mbozi na Watanzania, lakini niombe ikiwezekana wawa-*support*, wawape mtaji wawawezeshe, kwa sababu wana uwezo wa kufanya kazi ya kutuletea mbolea bora kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, *TFC* wanapoagiza mbolea tunahitaji mbolea iwahi, wawahi kuagiza na wakulima wawahi kuipata mbolea. Kuna mlolongo mkubwa kwenye uagizaji wa mbolea, taratibu za manunuzi na mlolongo wa manunuzi kwenye Taifa letu yanaeleweka, watu hawa wanaponunua mbolea wananunua kwenye Mataifa mengine....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananunua kwa wafanyabiashara wakubwa, ninaomba nimalizie sekunde.

**NAIBU SPIKA:** Malizia sentensi yako ya mwisho.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanaagiza kwa wafanyabiashara wakubwa, wale wafanyabiashara wakubwa hawazijui taratibu zetu, ninachokiomba wawape fedha wawaondolee mlolongo mrefu wa kuagiza mbolea, habari za *NeST* aachane nazo kwenye suala la mbolea tu ikiwezekana wakaagize mbolea kwa faida ya Watanzania kwa faida ya Wanambozi ili tupate mbolea kwa wakati. Wakati wanasubirisubiri mbolea huwa inapanda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja lakini dakika ni chache. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Amosy William Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Kapoma na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandae.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuwa mmoja wa wachangiaji katika Wizara hii muhimu sana Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mashaka na wala hakuna wasiwasi wowote kwamba ni kweli tunapokwenda ni kuzuri na tukizingatia kwamba kweli Wizara yetu ya Kilimo imepata watu shupavu ambao tunaona kwa kweli wanatupeleka kule ambako Watanzania tunakutaka.

Mheshimiwa Naibu Waziri, hivyo nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, lakini nimpongeze sana Naibu Waziri wa Kilimo, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanazozifanya. Kazi wanayoifanya inaonekana Watanzania tunaiona, wanafanya kazi mbalimbali hasa tunaona wanavyohangaika katika utafutaji wa masoko, tunawapongeza sana. Sisi wakulima wa tumbaku soko letu liliyumba, lakini chini ya uongozi wa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan tunaona masoko ya tumbaku yanapatikana, hivyo tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kazi nzuri za tafiti wanazofanya, wanafanya tafiti kwenye mbegu, viuatilifu pia kwenye afya ya udongo. Niseme kwamba waongeze kasi katika afya ya udongo. Tuna matatizo makubwa sana katika maeneo mbalimbali ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu Sikonge Waziri ni vigumu sana sasa hivi kupata angalau magunia 10 ya mahindi kwa ekari moja ni kazi kubwa kwelikweli. Pamoja na kwamba utatumia *input* zote, utatumia mbolea zote, mbolea ya kupandia, mbolea ya kukuzia pamoja na kuzalishia na taratibu zote za kilimo umezifuata, lakini imekuwa changamoto kwelikweli kupata hata gunia 10. Tunaomba hili kwa kweli lifanyiwe kazi kubwa ili kusudi suluhu ya afya ya udongo iweze kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi zote hizi kwa Wizara ya Kilimo, lakini nilete sauti ya wakulima wa tumbaku hapa Tanzania hususani wakulima wa zao la tumbaku Wilayani Sikonge. Kwa kweli kitendo cha bei ya tumbaku kushuka na wakati uleule bei ya mbolea kupanda kimeleta mkanganyiko mkubwa sana kwa wakulima wa zao la tumbaku hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimu uliopita bei ya tumbaku kwa wastani ilikuwa ni dola 2.559. Hii siyo kwamba wastani huu ulipatikana Sikonge, hapana ni kwa nchi, hii ni kwa taarifa ya Wizara. Ukienda kwenye randama ukurasa wa 44, tani zilizouzwa zilikuwa tani 185,772 na fedha zilizopatikana zilikuwa milioni 475 *plus*. Ukichukua hiyo ukagawa unapata wastani wa dola 2.559, wakati huo mfuko wa mbolea ya *NPK* tunayoitumia ilikuwa ni dola 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msimu huu mfuko wa mbolea umekwenda mpaka dola 63.89 wakati bei ya tumbaku kwa wastani ni dola 1.95, hili ni anguko kubwa sana kwa wakulima wa tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimependa sana dhima ya Wizara katika mambo mengi ambayo yamewekwa kwenye hiyo dhima, lakini kuna sentensi moja inasema kuboresha maisha ya Watanzania. Kweli tuendee kuyaboresha maisha ya Watanzania, lakini huu msukosuko wa bei kupanda na kushuka ninadhani ni vizuri tuangalie kama tunataka kuona kwamba kweli tunaboresha maisha ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kuangalia kwa nini bei ya mbolea imepanda namna hii. Nimejaribu kupitia maandiko mbalimbali, nikaja kuona kwamba bei ya kuzalisha kilo moja ya *NPK* ya mbolea pale Zambia ni wastani wa Kwacha 17,500 kwa tani. Kwacha moja ni sawa na dola 0.053, ukizidisha 0.053 kwa hiyo 17,500 unapata wastani wa kuzalisha tani moja ya mbolea ya *NPK* kule Zambia ni takribani dola 972 na *point*. Sasa ukizigawanya zile kwa mifuko 20 ambayo ndiyo tani moja unapata wastani wa dola 46.375.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga, ahsante sana, malizia sentensi ya mwisho.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana kwamba, Serikali iangalie namna ya kupunguza hizo tozo ambazo ni nyingi sana, kwa sababu toka 46 mpaka 63 ni hela nyingi sana. Tunaomba wapunguze ili kusudi wananchi waweze kupata tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimemtaja Mheshimiwa Josephine Kapoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamza Saidi Johari - Mwanasheria Mkuu wa Serikal na Mheshimiwa Ernest Silinde - Naibu Waziri wa Kilimo ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii niliyoipata ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninapenda kumpongeza kaka yangu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Daniel Chongolo pamoja na timu yake Naibu Waziri, Katibu Mkuu kwa hotuba kubwa na nzuri ambayo imelenga na kuwapa matumaini makubwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya maslahi ya muda, ninaomba nijielekeze moja kwa moja. Mosi, nitaelekea kwenye zao la tumbaku. Kwa nini zao la tumbaku, zao la tumbaku mimi nikiwa kama mwakilishi wa watu wa Morogoro hili zao ni katika mazao ya kimkakati ambayo watu wa Morogoro linatuingizia kipato kikubwa kwa sababu viwanda vya kuchakata tumbaku viko Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la tumbaku kwa takwimu tu, mwaka wa fedha 2020/2021 tulipata jumla ya mapato ya *USD* milioni 392, lakini kufika mwaka wa fedha 2024/2025 tumepata mapato ya zaidi ya *USD* bilioni 1.2, ni zaidi ya 187% ya ongezeko la pato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi watu wa Morogoro, Kiwanda cha Mkwawa *Tobacco* mwezi Aprili, 2024 kufika Disemba, 2025 tumefanikiwa kupata zaidi ya ushuru wa Halmashauri *levy* bilioni 2.7, lakini viwanda hivi tu kwa Morogoro toka Rais alivyokuja na mapinduzi ya tumbaku, Morogoro viwanda hivi vimeweza kuajiri ajira za muda mrefu zaidi ya wafanyakazi 1,000 na ajira za msimu zaidi ya 5,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi huwezi kuziongelea bila kumtaja Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku Ndugu Stanley. Kazi kubwa aliyoifanya katika mapinduzi ya tumbaku watu wote tunaelewa. Pia, sisi kama watu wa tumbaku pongezi kubwa tunazipeleka na wachangiaji wengi wamelalamika kwamba mbolea zinachelewa, lakini wakulima wa tumbaku na wadau wa tumbaku kwa kweli kwenye suala la mbolea hilo hatuna

malalamilko kwa sababu mbolea tumepata kwa wakati. Kwa hiyo pongezi nyingi sana ziende kwa kaka yangu Mshote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajielekeza sasa kuishauri Serikali. Wachangiaji wengi waliopita wamelalamika kuhusu suala zima la bei. Kweli mwaka jana wastani tuliuza kwa dola 2.3, lakini mwaka huu tunaenda kuuza kwa dola 1.9. Sasa ninaishauri Serikali, soko la tumbaku linakuwa-*controlled*, ni soko la kidunia hatuna *control* na bei ya tumbaku. Sasa tufanye nini, nilikuwa ninaishauri Serikali kwa sababu soko la tumbaku liko-*controlled,* ni wakati sasa sisi kama Tanzania tukaangalia masoko mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano Tanzania hatufanyi biashara na China, lakini tunao Mabalozi kama Balozi ambayo iko China. Huu ni wakati sahihi wa kuona ni vipi tunaweza tukatanua wigo wa soko na kwa kifupi China kufanya biashara na sisi, kitu ambacho tunatakiwa kukifanya ni mikataba ya nchi kwa nchi ambayo ni *bilateral agreement*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitanua wigo wa soko na kuongeza watu wengine *Wallah* nakuapia, hili suala la bei ya tumbaku halitakuwa kero kwa sababu tutakuwa na wigo mpana sana wa soko. Kwa sababu sasa hivi tuna wanunuzi wachache ambao wanaweza wakapanga bei wanayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuishauri Wizara kwamba shida ya bei ya tumbaku kidunia pia inasababishwa na *cost of production*. Hata hivyo, Tanzania tuna uwezo wa kutengeneza viwanda vyetu, ambapo tutatengeneza vifungashio kama magunia na kamba, tunayo katani na hizi malighafi ambazo hivi vitu tunaweza tukavitengeneza katika nchi yetu. Kwa sababu bei ya tumbaku inaathirika kikubwa sana na *cost of production*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukipata nafasi ya kuweka mikakati katika kujenga viwanda vya mbolea, viwanda vya magunia na nyuzi zikapatikana hapa, tunaenda kupunguza *cost of production,* hivyo hata soko la dunia likiyumba kwenye bei ya tumbaku, sisi bado tutakuwa tumeuza tumbaku yetu kwa faida na

soko likipanda maana yake tutauza kwa *supper abnormal profit*. Kwa hiyo ninatoa ushauri huu katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, soko la tumbaku sasa hivi tumekuwa na shida kubwa hasa katika mikutano ya kidunia, tumekuwa tunapigwa vita sana katika uzalishaji wa tumbaku.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja ninamalizia.

**NAIBU SPIKA:** Unga mkono hoja, muda wako umekwisha.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri na mtoa hoja ajiandae.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Nitachangia katika hoja kuhusu kuhalalisha matumizi ya mirungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mariam Mzuzuri ametoa ushauri kuhusu kuhalalisha mmea wa mirungi kutokana na mapato makubwa ambayo nchi zilizohalalisha mmea huo zimekuwa zikipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmea wa mirungi, umekatazwa chini ya Sheria ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya, Sura ya 55. Ni mmea ambao umeorodheshwa katika mimea ambayo imekatazwa *(prohibited plants)*. Sababu kubwa ya kukataza mmea huu ni athari kubwa za kiafya na kiakili za muda mfupi na

za muda mrefu kama ambavyo Mheshimiwa Mzuzuri mwenyewe amezitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu pia kwamba katazo hili limekuwepo pia katika ile Sheria ya awali ya Madawa ya Kulevya, Sheria Na.9, isipokuwa tu inawezekana kwamba hakuona kwa kuwa sheria hii tuliifanyia marekebisho kupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2002. Kule kwenye jedwali la kwanza tukaweka mirungi *(khat plant)* kwamba ni miongoni mwa mimea ambayo ni hatarishi na hairuhusiwi kwa matumizi ya mwanadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tafiti mbalimbali zimefanyika duniani, kwa sababu ni jambo ambalo na jumuiya za kimataifa pia vilevile zililiona; na katika tafiti hizo wakati tunajadiliana au tuna-*negotiate*, *United Nations Convention Against Illicit Narcotic Drugs and Psychotropic Substances* ya mwaka 1988, tafiti zile zilileta matokeo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mmea huu unaojulikana kama mirungu au *khat* au wakati ule wa hiyo *convention* waliujumuisha katika zile *cathinone* au *catha edulis*, kwamba kwanza unashambulia *cardiovascular system* au afya ya moyo; pili, *mental health system*; na tatu, kwa kadri yule anavyotafuna mwisho kabisa inaenda kuishia kwenye ini, kwa hiyo inaenda kuleta *liver toxicity* ambayo inasababisha athari kwenye afya ya ini. Kwa hiyo hatuwezi tukaja na hoja kwamba mapato iwe faida zaidi kuliko afya ya mwanadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Usafirishaji Haramu wa Dawa za *Narcotic* na *Psychotic Substance,* Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni *signatory,* kwa maana tulisaini na tuliridhia tarehe 20 Disemba, 1996 na ndiyo ilikuwa sababu hasa kuja kufanya marekebisho ya sheria hii ya mwaka 2002. Kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwamba, afya za wananchi zisiwe *at the expense* ya mapato au *revenue*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nilitaka nilichangie, ilikuwa ni hoja ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Thomas Maganga. Yeye ameishauri Serikali itunge sheria ya kusimamia kilimo cha mkataba *(contract farming)*. Serikali inatambua kuwa mfumo madhubuti wa kisheria kusimamia kilimo cha mkataba ni muhimu sana ili kulinda haki na maslahi ya wakulima na wadau wote wa katika mnyororo wa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu taarifa, kwamba zipo sheria katika sheria ambazo tunazo ambazo kwa kiasi fulani zinazungumzia masuala ya kilimo cha mkataba. Kwa mfano, Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura 249; kuna Sheria za Kisekta, kama Sheria ya Tasnia ya Pamba, Sura 201; Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura 251; Sheria ya Tasnia ya Korosho, Sura 203; na Sheria ya Tasnia ya Tumbaku, Sura 202.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, lazima tukubali kwamba inawezekana sheria hizi zisijitosheleze na huko tunakokwenda ili kutekeleza malengo ya Dira ya 2050 ambapo tunasema kwamba, kilimo liwe eneo ambalo watu wote watataka kukimbilia, ikiwemo vijana, basi tunaona kwamba ni muhimu tuangalie vizuri kuona kama je, tunakuja na sheria mahususi ya *contract farming* au tunakuja na kanuni za *contract farming*. Tulisema na tunaendelea kusema kwamba, hayo yote lazima iwe ni zao la utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna orodha ya sheria ambazo tumeanza kuzifanyia mapitio kwa lengo la kuzifanyia marekebisho. Mifumo ya sheria za kilimo, itafanyiwa mapitio na marekebisho mwaka wa fedha 2026/2027. Kwa hiyo, pale tutakuwa tumekuja na majibu kwamba sasa tumekuja na sheria mpya au mahususi ya *contract farming* au tutakuwa tunafanya vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ni nzuri na tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuileta na tutaifanyia kazi kuona kama tunakuja na sheria mpya mahususi ya *contact farming*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Hamza Saidi Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mchango wako. Mheshimiwa Naibu Waziri, atafuatiwa na Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na shukurani. Kwanza ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kukaa hapa siku mbili na leo tunakwenda kuhitimisha baada ya kujadili bajeti yetu ya Wizara ya Kilimo. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kwangu kwa kuniteua na kuwa Naibu wa Waziri wa Kilimo. Ninaahidi kulipa imani kwa imani, nikitambua wajibu wangu kwa nchi yangu, Rais wangu, pamoja na chama changu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipeleke shukrani zangu za kipekee kwa Waziri wangu Mheshimiwa *Comrade* Daniel Chongolo. Waziri bora kabisa na mtu makini. Amekuwa akitupa uongozi mahiri kabisa katika Wizara na miongozo yake imekuwa mizuri kwelikweli. Ni mtu anayesikiliza, ni mtu anayetaka tubadilishe Wizara iende ikamhudumie mkulima wa chini kabisa, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri. Nina hakika Mheshimiwa Waziri ana upendo mkubwa sana na sisi kama wasaidizi wake tunajifunza sana kutoka kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru sana Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote wa taasisi zote za Wizara, wamekuwa wakitupa ushirikiano mkubwa hata leo tunapojadili mafanikio ya Wizara ya Kilimo ni matokeo ya michango yao na ushauri wao, ambao sisi kama wasimamizi wa sera tumekuwa tukizisimamia ili zilete matokeo yenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika ufafanuzi wa hoja, na niseme tu kiukweli, Wizara ya Kilimo tangu Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingia madarakani, imekuwa ni Wizara yenye tija na matokeo makubwa sana. Ndiyo maana hata leo katika Bunge lako Tukufu utaona katika siku mbili Waheshimiwa Wabunge wengi wameomba kuchangia, kwa sababu wanaona kuna fursa kubwa, kuna matokeo makubwa na hatua kubwa imepigwa tangu Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeingia madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wanafahamu, wakati wa mapinduzi ya viwanda duniani huko katika miaka ya 1760, kule Uingereza, mapinduzi ya viwanda yalikuja baada ya matokeo ya mapinduzi makubwa ya kilimo; na wenzetu wale waliwekeza katika maeneo makubwa manne. Moja katika eneo la umwagiliaji, eneo la pili waliwekeza katika matumizi ya zana bora za kilimo, eneo la tatu waliwekeza katika matumizi sahihi ya mbolea na eneo la nne waliwekeza katika matumizi ya mbegu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa upi ni mwelekeo wa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? Ninataka niwaeleze, haya waliyoyafanya wenzetu, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wabunge wote watakuwa mashahidi wa hiki ninachokwenda kukisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, Mheshimiwa Rais wakati anaingia madarakani, bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilikuwa bilioni 51.5. Leo tunapozungumza bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeongezeka na kufika bilioni 382. Huo ni uthubutu mkubwa wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, ukiangalia hivyo na hata ukienda kuangalia bajeti mama ya Wizara, wakati anaingia madarakani Mheshimiwa Rais, ya bilioni 294, leo tunazungumza bajeti ya Wizara ya Kilimo trilioni 1.105, ambayo tunakwenda kuipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alituelekeza sisi Wizara ya Kilimo, alisema ninataka sasa tutoke kwenye kilimo cha kutegemea mvua kilimo cha msimu, ninataka kwenda kwenye

kilimo cha umwagiliaji. Haya ambayo yalileta mapinduzi ya viwanda, leo tunakwenda kuyatekeleza. Cha kwanza tunapozungumza leo, tunatekeleza miradi ya umwagiliaji 146 yenye thamani ya Shilingi za Kitanzania trilioni 2.4, ipo inaendelea na utekelezaji wake na wakandarasi wako kazini. Hii ni nia ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha tunatoka kwenye kilimo cha msimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameelekeza, tuwe na Gridi ya Taifa ya umwagiliaji, kutoa maji Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika kupeleka katika mikoa yenye ukame. Wewe fikiri unatoa maji zaidi ya kilometa 1,645 kupeleka katika maeneo yenye upungufu, mradi huu peke yake utagharimu zaidi ya fedha za Kitanzania trilioni 2.5. Eneo la umwagiliaji peke yake litakuwa zaidi ya hekta milioni tatu. Mikoa ambayo itanufaika katika maeneo hayo ni mikoa 12, wilaya 24, na vijiji 441; na kutakuwa na mabwawa makubwa zaidi ya 52. Huu ni uthubutu na nia njema ya Mheshimiwa Rais kwa Watanzania kwenye eneo la umwagiliaji peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi Mheshimiwa Rais alituelekeza tufanye usanifu wa kina kwenye mabonde yote makubwa hapa nchini; na hiyo kazi inaendelea sasa hivi. Tunavyozungumza tumeshafanya usanifu wa kina na mabonde 10 yanakwenda kutekelezwa; ambapo gharama tu peke yake ya mradi huu ni takribani fedha za Kitanzania trilioni 3.9. Mabonde kama Bonde la Mto Rufiji, Bonde la Mto Kilombero, Bonde la Mto Malagarasi, Bonde la Kamsamba, Bonde la Mto Ngono, Bonde la Mara Valley, Bonde la Lukuledi, Bonde la Ziwa Rukwa, Bonde la Suguti na Bugwema na Bonde la Kasinde. Haya ni malekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye eneo la umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametuelekeza vilevile, tuhakikishe kwenye miradi ya umwagiliaji ya asili, kwa sababu kuna vijiji vingi vina vile vimiradi vidogovidogo vyenye wastani wa thamani ya shilingi 500,000,000 mpaka shilingi 1,000,000,000, nayo tuitekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani wakati tunaendelea na miradi mikubwa Wizara kupitia tume ifanye miradi midogo midogo. Hiyo ndiyo nia njema ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha Tume inamsadia mkulima wa kawaida katika kuongeza tija. Tuna mradi wa uchimbaji wa visima zaidi ya 67,000 ambavyo tutafika katika halmashauri zote. Ninavyozungumza sasa hivi tayari Tume ya Umwagiliaji ina magari 19 ya uchimbaji visima ambavyo tutawachimbia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo tutakaowachimbia bure kabisa kwa ruzuku ya 100% wapo tukaowachimbia kwa 50% watachangia 50% na wale wenye kipato kikubwa watachangia takribani 75% na 25% Serikali itatoa. Lengo ni kusaidia sekta ya kilimo kwenye eneo la umwagiliaji ili wananchi wafanye kazi ya kilimo muda wote katika msimu wa mwaka. Kwa hiyo, utaona kwenye hilo eneo peke yake la umwagiliaji Mheshimiwa Rais amewekeza nguvu kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ninataka nilitolee ufafanuzi ni kwenye matumizi ya zana bora ambayo wenzetu walifanya na Mheshimiwa Rais sasa anafanya. Tunakwenda kuwekeza matrekta zaidi ya 10,000 kwa kujenga vituo vya zana za kilimo kwenye halmashauri zote nchini zaidi ya 1,000. Hadi sasa hivi tumekwishafungua vituo 79 kwenye halmashauri 25 nchini. Vyote tunataka mkulima wa kawaida aweze kupata zana za kilimo; yaani matrekta, pawatila; ili yaweze kumsaidia katika kulima na kuongeza tija katika mashamba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya yote unayoyaona tu ni jitihada za Serikali,. Katika eneo la matumizi sahihi ya mbolea, ninyi wote ni mashahidi; wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani, nchi yetu hii matumizi ya mbolea peke yake yalikuwa chini ya tani 400,000. Leo matumizi yameongezeka kiasi kwamba tija imekuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatolea mfano tu wa zao la mahindi peke yake, miaka mitano iliyopita hatukuwepo hata kwenye tatu bora, waliokuwa wanaongoza ni South Afrika, Nigeria pamoja na Nchi kama Ethiopia. Mwaka jana Tanzania

tulikuwa nchi ya pili kwa uzalishaji wa mahindi tukifuatiwa na South Afrika. Tumezalisha takribani tani 11,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa fikiri watu ambao tulikuwa hatupo kwenye *records*; tija imeongezeka kiasi kwamba haya mazao yaliyokuwa yanaonekana mazao ya chakula, ukiangalia thamani ya mazao, *export value* yake, yameleta fedha nyingi za kigeni. Kwa mfano, mahindi peke yake yameingizia Taifa letu karibu bilioni 684.9, mchele umeingizia bilioni 619.4, maharage imeingiza bilioni 304.2. Ukienda kwenye ufuta utakuta trilioni mbili, mbaazi utakuta zaidi ya bilioni 824. Hayo ni mazao ambayo yalikuwa yamezoeleka ni mazao ya asili na si ya kibiashara, lakini leo yana tija kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko kwenye *track* sahihi. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge tupitishe hii bajeti na nimwombe hata ndugu yetu Mheshimiwa Ado alikuwa anataka Mheshimiwa Waziri amtembelee, lakini mwisho wa siku anasema tusipitishe bajeti, tusipopitisha bajeti Mheshimiwa Waziri hawezi kufika katika eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge tupitishe bajeti hii. Ninaamini tuko kwenye *track* sahihi na tutamsaidia Mheshimiwa Rais na hii nchi itasonga mbele na kilimo ndiyo mkombozi wa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ernest Silinde, Mheshimiwa Naibu Waziri wetu wa Kilimo. Sasa ninamwita Mheshimiwa Daniel Chongolo, Waziri wa Kilimo na mtoa hoja. Karibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabla sijaanza kujibu hoja za msingi sana ambazo zimezotolewa na Waheshimiwa Wabunge; mtakubaliana nami kwamba hali ya hewa jana na leo ilikuwa inaonesha dhahiri kwamba inasindikiza shughuli ya kilimo humu ndani. Tumepata mvua ya kutosha jana

na tumepata mvua ya kutosha leo. Dalili njema kwamba Mwenyezi Mungu ameweka mkono wake kwenye kilimo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwepo hapa leo tena kutekeleza majukumu yetu ya Kibunge. Nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi na Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia mjadala wa hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2026/2027 ambao tunauhitimisha leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara Kilimo na Mifugo kwa maoni na ushauri wao ambao umelenga kuboresha utekelezaji wa shughuli za kilimo kwenye eneo la umwagiliaji, huduma za ugani, masoko ya mazao ya kilimo, vituo vya huduma za zana za kilimo, utafiti na uzalishaji wa mbegu bora na ulinzi wa mbegu za asili. Vilevile kujenga miundombinu ya uhifadhi pamoja kuimarisha maendeleo ya ushiriki. Wizara itazingatia maoni na ushauri wao kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji. Aidha, ninaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wote katika kutekeleza malengo ya Taifa ya kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kutoa hoja nzuri sana zinazolenga kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo na kujenga Sekta ya Kilimo endelevu na yenye ushindani ili kukuza uchumi shirikishi, kuboresha maisha ya mkulima na Taifa lenye utajiri. Hii inaonesha wazi umuhimu mkubwa wa Sekta ya Kilimo katika uchumi wa nchi hususani katika kuimarisha usalama wa chakula, lishe, maendeleo ya viwanda, ajira na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, kwa kuchangia hoja hii na kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali zilizojitokeza wakati wa majadiliano. Wakati anazungumza wote watakuwa mashahidi watafikiri ndiyo amekaimu kabisa na nafasi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Bwana Gerald Geofrey Mweli, Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Athumani Juma Kilundumya anayeshughulikia umwagiliaji na zana za kilimo, pamoja na Profesa Peter Laurence Makenga Msofe anayeshughulikia maendeleo ya mazao na usalama wa chakula kwa kuendelea kunisaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile ninawashukuru Wakuu wa Idara Na Vitengo, Wakuu wa Taasisi, Bodi, Wakala zilizo chini ya Wizara, na watumishi kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ninaomba nirudie kusema maneno niliyoyasema jana wakati ninatoa hoja kwa sababu ndiyo msingi wa bajeti hii na mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027, lakini pia ndiyo msingi wa mwelekeo kwenda 2030. Maneno haya yalisemwa na mzee mmoja aliyekuwa akitoa urithi wakati anakaribia kufariki kwa wanawe alisema, *"Kama mnataka mali mtaipata shambani"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ninaomba sasa niwatambue Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuongea na kwa maandishi. Hoja yangu imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 70. Ninapenda kuwahakikishia kuwa majibu ya hoja zote zilizotolewa kwa kauli na maandishi yataandaliwa na kuwasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuhitimisha Mkutano huu wa Bunge la Bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa nitoe ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yafuatayo: Hoja ya kwanza ni eneo la Jenga Kesho Iliyo Bora kwenye *program* ya *BBT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afrika na Dunia kwa miaka mingi tumekuwa na maswali mengi ya namna ya kupunguza changamoto ya ajira kwa vijana. Kwa mfano Afrika ambayo ina zaidi ya 60% ya ardhi inayofaa kwa kilimo hilo swali tumekuwa nalo kwa muda mrefu sana. Serikali ya Awamu ya Sita chini ya

Uongozi wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan iliamua kuja na mpango wa kutatua changamoto ya ajira kwa vijana kwa kuanzisha Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora hivyo hiyo program haikuwa na haijaja kwa bahati mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutambua kwamba vijana waliopo wana jukumu la pamoja la kutengeneza kesho yao iliyo bora kupitia kilimo. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa nia ya dhati aliamua kuwezesha vijana na wanawake kupata ajira zenye staha, kuwezesha upatikanaji wa mitaji, ardhi, ujuzi na masoko kupitia programu hii ya *BBT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia *BBT* wengi wanaichukulia kama ni *project* na siyo *program* na hili ninataka angalau kwa dakika mbili nilieleze kwa kina. Tukisema *BBT* ni *project* tutaangalia mashamba ya Ndogoye na tutaangalia mashamba ya Chinangali kwa sababu watu wote wanaamini hapo ndipo mwisho wa programu hii muhimu ya *BBT,* lakini ukienda kwa upana *BBT* ni zaidi ya miradi ambayo tunaizungumzia (miradi miwili mikubwa) ambayo ndiyo inayobeba sura nzima ya *project* pana ya Jenga Kesho Iliyo Bora kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge programu hii imefanyika kwenye haya maeneo mawili kama *pilot study* kwa sababu kwa uhalisia ukiangalia Afrika hamna *project* au *program* kubwa ambayo ilibeba dhamira ya kujielekeza kuhamasisha vijana kwenda kuingia kwenye kilimo na kutafuta fursa na kutumia fursa za kilimo kujikwamua na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania sisi ndiyo tumeanza tutafute programu nyingine ambayo iko Afrika ambayo inatekelezwa kwa vijana ambayo imefikia hata kuwa na uwezo wa kutambulika na vijana na Watanzania na wananchi kama ilivyo *program* ya *BBT* kwa Watanzania. Baada ya majaribio ya maeneo hayo mawili kwetu tumejifunza kwanza tumefanikiwa, lakini pia kuna changamoto ambazo zimetupa nguvu ya kutengeneza mazingira ya kuweka msukumo wa kwenda mbele tukiwa imara zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakwenda kwenye wilaya na majimbo yetu nchini. Kwa kuanza tunaanza na halmashauri 18 na nitazitaja ya kwanza ni Chemba, Bahi, Kisarawe, Kibaha, Kilolo, Njombe, Manyoni, Musoma, Ikungi, Kaliua, Kakonko, Nkasi, Muleba, Missenyi, Njombe Mji, Manispaa za Geita na Mpanda. Lengo ni kuhakikisha tunawapa vijana kule kule kwenye maeneo wanakoishi sasa nyenzo za msingi za kuwafanya waendeshe kilimo kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaanza pia ujenzi wa miundombinu kwenye shamba lenye ukubwa wa ekari 20,000 katika Halmashauri ya Chunya kwa ajili ya vijana kama inavyofanyika katika mashamba ya Kapunga na *Highland Estate*. Lengo ni kuhakikisha vijana wanapata ardhi ya kilimo ambayo ilibainishwa kuwa ni hitaji kubwa wakati wa tathmini ya kuanzishwa kwa programu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo *BBT* imefanikiwa sana kwenye upande wa majaribio na changamoto chache zilizojitokeza ni sehemu ya kujifunza. Niwahakikishie huko tunakokwenda sasa tutaona tunavyogusa vijana. Lakini niseme hatutaishia kwenye hiyo tu tuna mradi wa visima, tuna magari 19 ya visima sasa hivi tunayo. Tuna vijana ambao sasa hivi wanalima kwenye maeneo wanayolima wana changamoto ya uhaba wa maji, wana changamoto ya uhaba wa miundombinu ya umwagiliaji. Waheshimiwa Wabunge wakitusaidia kuwapata tukawatambua tukawatengenezea miundombinu ndiyo jenga kesho iliyo bora itakuwa inatekelezwa kwa utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya mazao ya kimkakati. Tuna mazao ya kipaumbele 13 ambayo yapo katika ajenda *10/30* au *ten thirty* na mpango kabambe wa maendeleo ya kilimo 2050. Baadhi ya mazao hayo tumeshaanza kuyafanyia kazi na katika mwaka wa fedha 2026/2027 tumepanga kuendelea na mazao matano ya alizeti, chikichi, ngano, tufaa *(apple)* na viazi mviringo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haimaanishi kwamba mazao mengine hatuendelei nayo au hatutaendelea nayo. Tutaweka nguvu kwenye mazao hayo ili kupunguza uingizaji wa mafuta ya

kula, kupunguza uingizaji wa ngano na kuhakikisha tunaongeza ajira na kuwa na usalama wa chakula nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uzalishaji wa mazao hayo ya kipaumbele, Serikali itaendelea kutumia vyama vya ushirika katika kuanzisha viwanda vidogo vya kukamua alizeti na usindikaji wa ngano badala ya kutegemea viwanda vikubwa pekee. Pia, kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu, Serikali itaimarisha uzalishaji wa zao la Chikichi ili kupunguza matumizi ya fedha za kigeni katika uagizaji wa mafuta ya kula nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viazi mviringo Waheshimiwa Wabunge wanafahamu zao hili ni moja ya mazao muhimu kwa ajili ya chakula na mhimili mkubwa wa uchumi wa vijana hususan katika Kanda za Nyanda za Juu Kusini na Kaskazini, hata hivyo kumekuwa na tatizo kubwa la uhaba wa mbegu. Sasa eneo tunaloliwekea msukumo ni kuhakikisha tunaweka msukumo kwenye utafiti wa mbegu na upatikanaji wa mbegu za uhakika kupitia taasisi yetu ya utafiti ya *TARI.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *TFC*. Mwaka 2021 wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anaapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, *TFC* ilikuwa imekufa. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuipatia *TFC* mtaji wa shilingi bilioni 116 ambao umeiwezesha kuwa miongoni mwa kampuni kubwa katika biashara ya mbolea nchini ikishika nafasi ya nne kati ya kampuni 32.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kufufuliwa kwa kampuni hiyo imeweza kuuza jumla ya tani 299,787 zenye thamani ya shilingi 544,000,180,000. Katika msimu wa 2025/2026 unaoendelea mathalani Oktoba, 2025 ilipojitokeza changamoto kubwa ya mbolea ya *DAP* katika maeneo ya uzalishaji, *TFC* ndiyo kampuni pekee iliyonunua na kusambaza mbolea ya *DAP* tani 50,000 kwa kipindi ambacho kampuni nyingine binafsi hazikuleta na kuwasaidia wakulima kuwa na mbolea ya kupandia na tukavuka salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua kuna maeneo ilichelewa na hayo ndiyo malalamiko makubwa ya Waheshimiwa Wabunge lakini kwa sababu tumejifunza tutahakikisha msimu ujao wa kilimo tunawahisha mbolea kwa sababu tumejua kutegemea kampuni binafsi pekee tunaweza tukakwamisha jitihada za wananchi wetu kwenye kilimo hasa kwa kukosa pembejeo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hilo tumelichukua na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tutaliwekea msukumo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hoja ya ushirika mwaka huu Waheshimiwa Wabunge wanafahamu, tumeuza mazao ya kahawa, korosho, tumbaku, chai, pamba, ufuta, kakau, soya, mbaazi, dengu, mkonge, choroko, pareto, maharage na miwa tani 1,719,219.77 kwa thamani ya shilingi trilioni 4.048 kupitia ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ushirika kuna watu wema na wabaya kama ilivyo kwenye maeneo yote ya kazi. Ninakiri na ninafahamu kuhusu mnada Na.6 wa Tandahimba ambao ulitokea changamoto ambayo tayari imetatuliwa pamoja na kwamba hiyo ni chini ya 0.01% ya jumla ya biashara iliyofanyika kupitia ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni, ushirika unafanya vizuri na unaendelea kuimarishwa. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuboresha ushirika kuwa nyenzo muhimu ya kuleta mageuzi ya kiuchumi. Sisi ambao tumepewa dhamana ya kusimamia Wizara ya Kilimo tutaweka udhibiti mahususi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana kupitia *program* ya "Linda Ushirika Chagua Uadilifu" sasa kuwa na chombo kitakachohusisha vyombo vyote vinavyohusika na *enforcement*, udhibiti na mambo kama hayo ikiwemo Polisi, TAKUKURU, *DPP* na ofisi nyingine za udhibiti ili kwenda kufanya ufuatiliaji kwenye

maeneo yaliyofanyiwa ufujaji au ubadhirifu, lakini kubwa kutengeneza udhibiti ili pesa ya mwanaushirika isiliwe tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masoko kwa kiasi kikubwa tumefanyia kazi changamoto zilizokuwepo huko nyuma. Tumefungua masoko mapya, tumevutia wanunuzi na kuimarisha mifumo ya uuzaji wa mazao ya kilimo. Kwa upande wa mazao mbalimbali imebainika kuwa pale bei inaposhuka wakulima wanaona kama ni changamoto ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeamua kuingia kwenye biashara ya Kimataifa. Kama wanavyofahamu kwenye kufanya biashara kuna kupanda na kushuka kwa bei kutegemea nguvu ya soko. Mazao mengi ya biashara yanategemea soko la nje na Tanzania siyo nchi pekee inayozalisha mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tunaendelea na jitihada za kufungua masoko, tutakuwa tukifuatilia bei ya masoko kama walivyoshauri kwa sehemu kubwa huko huko ambapo yapo masoko husika ili wakulima wetu wapate uhakika na wapate bei ya uhakika tofauti na kuruhusu watu wa katikati kuendelea kutumia mwanya wa kutojua bei halisi ya soko kwa bidhaa tunazolima nchini kuwanyonya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hoja ya bima ya afya kwa wakulima wa zao la korosho, ushauri umepokelewa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka kwenye eneo tunalolima zao la korosho tutafanya tathmini ya kina kujua namna gani tunaweza tukafanikisha hili kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakapokamilisha tutakaa na kuwashirikisha wote ili tuone namna bora ya kulitekeleza. Hili hatutalifanya kwa korosho tu, tutalifanya kwenye maeneo ya mazao mengine kama pamba, tumbaku na maeneo mengine ambayo yana mazao yanayolimwa kwa ukubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa zao la chai ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya kiwanda cha *DL*

kwa muda mrefu nyuma, lakini hivi leo tunavyozungumza tumefanya majadiliano ya pamoja na mwekezaji pamoja na *financier* wa mwekezaji ambaye ni *CRDB Bank*. Mwekezaji huyo ameonesha nia na ninawaahidi ndani ya miezi sita kama *DL* hataweza kutekeleza tuliyokubaliana tutatafuta mwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba katika hili uruhusu baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wa maeneo ya chai pamoja na Kamati inayosimamia Sekta ya Kilimo kwa lengo la kupata uelewa wa pamoja tufanye ziara kule uwandani kwenye eneo la mradi. Twende wote tusikilize tuone lakini tujiridhishe na kile ambacho kinazungumzwa kwamba ni uwekezaji wenye lengo la kuanza uzalishaji wa chai bila usumbufu kwa wakulima lakini na kwa wadau wote wanaozunguka mashamba husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini tukienda tukarudi wote kwa pamoja tukijadiliana tutakuwa na jambo la msingi la kushauriana ili kutafuta hoja pana. Hiyo ni pamoja na kwenye uwekezaji wa kiwanda cha *WATCO, (Wakulima Tea Company Limited)* lakini pia na yale mashamba yaliyopo na uwekezaji unaoendelea kule *East Usambara* pamoja na Korogwe na Bumbuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kiwanda cha Mbolea kujengwa Tabora msimamo wa Serikali haujabadilika. Hata hivyo, mwekezaji ambaye tunamkusudia au tulimkusudia ajenge kiwanda husika ni mwekezaji binafsi na Wizara inatamani uwekezaji huo ufanyike nchini na ukifanyika Tabora ingekuwa baraka zaidi kwa sababu ni karibu na eneo ambalo uzalishaji mkubwa na watumiaji wakubwa wa mbolea hiyo wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mwekezaji ni mtu binafsi, sisi tungetamani. lakini na yeye ni lazima tumpe nafasi ya kuangalia namna anavyoweza kutengeneza biashara kupitia kile anachokusudia kukifanya. Hata hivyo, nisitize msukumo wa Wizara na msukumo wa Serikali ni kiwanda kijengwe Tabora ili kiwe karibu na wahitaji wa mbolea husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya pia vikao na Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye maeneo yanayolima tumbaku, yanayolima pamba pamoja na korosho. Niwahakikishie yale yote tuliyokubaliana tutahakikisha tunayawekea msukumo kuyatafutia matokeo. Sasa nishukuru tena kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi wa maeneo machache kuhusu hoja hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*……….….…Sh. 7,831,382,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hili ndiyo fungu ambalo lina mshahara wa Mheshimiwa Waziri na tunaye Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ninahitaji tu *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kwamba kama nilivyochangia kwenye mchango wangu wa muda mfupi Tarime mazao ya wananchi wangu yanapotelea Kenya, hatuna soko katika eneo lile na wamepeleka fedha zaidi ya shilingi bilioni moja, lakini ujenzi wa soko umesimama sasa ni takribani miezi nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba tu *commitment* ya Mheshimiwa Waziri kwamba ni lini hilo soko litafanya kazi pale Remagwe ili wananchi wangu wanapokuwa na mazao ya mihogo niliyosema, ndizi, viazi na mahindi yakusanywe eneo moja na wale wateja kutoka Kenya waje kununua hapa Tanzania, watu wetu wapate usalama lakini pia na soko zuri la mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu, sina nia ya kuendelea kumsumbua *Comrade* na Katibu Mkuu Mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi wa hoja hiyo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli eneo la Sirari, Tarime wamekuwa wakiuza mazao upande wa Kenya na ni kwa sababu tulikuwa hatuna soko pale mpakani, lakini hivi sasa tuna soko ambalo tunaendelea na ujenzi pale Sirari ambalo sasa hivi lipo kama 80%. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutakwenda kulimaliza kwa mwaka ujao wa fedha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*...............Sh.1,609,169,148

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……............… Sh.4,740,226,000
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*……….Sh.13,134,413,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*……………...............Sh.868,827,772
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*…...Sh.1,057,736,822
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*……………..............……………Sh.670,139,000
Kifungu 1008 – *Legal Service Unit*……………………......Sh.839,584,000
Kifungu 1009 – *Management Information System Unit*……………....………………..........Sh.924,295,000
Kifungu 1010 – *Environment Management Unit*…………………....………………........Sh.560,347,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*....................................................Sh.1,060,926,000
Kifungu 2001 – *Crop Development*……….........……Sh.76,335,844,000
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization*……......…Sh.7,115,618,000
Kifungu 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Management*…….................…… Sh.1,217,938,258
Kifungu 2004 – *Plant Breeders' Unit*…………………….Sh.444,914,000
Kifungu 3001 – *Research Development*……………………………Sh. 0
Kifungu 5001 – *National Food Security*..................….Sh.13,228,494,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh.4,352,026,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…...........Sh.1,173,574,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*................................Sh.1,042,200,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*…..Sh.360,380,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*.........Sh.659,645,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*……………………..…Sh.688,240,000
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*…….........….…..…....Sh.659,510,500
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*……………………Sh.1,059,875,000
Kifungu 1009 – *Environmental and Social Management Unit*…………..........…………………Sh.1,219,090,000

Kifungu 2001 – *Design and Research Division*……...........……………………Sh.54,630,379,300
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*……………………….…Sh.5,142,948,200
Kifungu 2004 – *Operations Division* ……………..........Sh.2,857,530,000
Kifungu 2005 – *Compliance and Quality Assurance Section*............................Sh.1,723,402,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu1001 – *Administration and Human Resources Management*…..................................Sh.2,091,633,647
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*................Shs.402,196,130
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*……………….................Sh.446,440,430
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*…..Sh.333,268,310
Kifungu 1005 – *Legal Service Unit*.................................Sh.231,680,745
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*.........Sh.226,288,745
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology*…......................................Sh.888,385,745
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*………………...........Sh.269,705,318
Kifungu 1009 – *Research and Training*..........................Sh.292,072,310
Kifungu 4001 – *Cooperative Promotion and Coordination Section*..........................Sh.412,416,900
Kifungu 4002 – *Cooperative Microfinance Section*.....Sh.429,750,900
Kifungu 4003 – *Regional Cooperative Offices*..........Sh.7,659,894,000
Kifungu 4004 – *Cooperate Marketing and Investment Section*..............................Sh.641,997,720
Kifungu 4005 – *Registration Service Section*.................Sh.294,892,720
Kifungu 4006 – *Inspection and Supervision Services Section*.................................Sh.7,355,970,380

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*......................................................Sh. 0
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*................Sh.384,845,730,000
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*..............Sh.5,700,000,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*.....................Sh.0
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*..........Sh.500,000,000
Kifungu 2001 – *Crop Development*.....................Sh.114,500,000,000
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization*..............Sh.3,000,000,000
Kifungu 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Management*..........................Sh.3,800,000,000
Kifungu 5001 – *National Food Security*....................Sh.55,000,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*...........................................Sh. 895,100,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*...................................Sh.150,000,000
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*..................................Sh.588,900,000
Kifungu 1009 - *Environment and Social Management*.....................................Sh.1,179,600,000
Kifungu 2001 – *Design and Research Division*........Sh.54,787,000,000
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*...............................Sh.249,826,361,000
Kifungu 2004 – *Operations Division*.........................Sh.1,045,000,000
Kifungu 2005 – *Compliance and Quality Assurance*........................................Sh.250,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu 4001 – *Cooperative Promotion and Coordination*................................Sh.418,305,600
Kifungu 4006 – *Inspection and Supervision Services Section*...................................Sh.278,870,400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara ya Kilimo, Fungu 43, 24, na Fungu Na.5 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, ninaomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeunga mkono. Sasa nitawahoji kuhusiana na Hoja ya kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, imepitishwa rasmi na Bunge. Hivyo nichukue nafasi hii kupongeza Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii. Tuwatakie kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ambayo imeajiri Watanzania wengi lakini inachangia pia pato la Taifa kwa kiwango kikubwa.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuipongeza Kamati yetu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pamoja na Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Wabunge wote ambao wamepata nafasi ya kuchangia Wizara, hii tunawapongezeni wote kwa kazi nzuri iliyofanyika.

Mheshimiwa Wabunge, nina tangazo moja, Katibu wetu wa Wabunge wote wa CCM anawatangazia Wabunge wote wa CCM kuwa kesho saa saba mchana mara baada ya kusitishwa shughuli za Bunge, kutakuwa na *party caucus* katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete. Wabunge wote mnatakiwa kuhudhuria bila kukosa. Tangazo kutoka kwa Katibu wa *Caucus* Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi.

Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru wote na baada ya maneno haya machache, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi

*(Saa 1.33 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 30 Aprili, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*